

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Ishirini – Tarehe 4 Julai, 2005

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

DUA

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):

Taarifa ya Mwaka ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha kwa Mwaka 2003/2004
(The Annual Report of the Institute of Finance Management for the Year 2003/2004)

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mfuko wa Ukusanyaji Madeni Sugu ya Mashirika ya Umma kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 June, 2004 *(The Annual Report and Accounts of the Loans and Advancers Realization Trust for the year ended 30th June, 2004)*

NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO :

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

MHE. SOPHIA M. SIMBA – MWENYEKITI KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:

Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

MHE. TEDDY L. KASELA – BANTU MSEMAJI WA UPINZANIA KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO:

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 186

Taarifa Sahihi za Mtumishi Anayestaafu

MHE. MWANNE I. MCHEMBA aliuliza:-

Kwa kuwa, Mtumishi wa Serikali anapofikia umri wa kustaaafu, taarifa za utumishi wake hutayarishwa na mwajiri wake na kuwasilishwa hazina kwa ajili ya kuandaa malipo ya pensheni na stahili nyingine zote na kwa kuwa, taarifa hizo huandaliwa kwa urahisi na mwajiri kwa wale Watumishi ambao taarifa zao zinaeleweka kama tarehe, mwezi na mwaka ambao mtumishi amezaliwa na taarifa za utumishi wake kwa ujumla:-

(a) Kwa wale Watumishi ambao hawajui tarehe na miezi waliyozaaliwa, pengine wanafahamu mwaka tu. Je, taarifa za Watumishi wa aina hiyo zinaandaliwa kwa kuzingatia kigezo gani?

(b) Kabla ya kuandaliwa kwa taarifa za Watumishi hao je, wahusika wanapewa taarifa ya awali juu ya tarehe na mwezi wanaotakiwa kustaaafu kabla taarifa zao hazijapelekwa hazina ili wajiandae. Kama wanapewa taarifa hizo zinatolewa miezi mingapi kabla ya kuzipeleka Hazina?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum - Tabora, naomba kwanza kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, toleo la pili la mwaka 1994, mtumishi akiajiriwa kwa mara ya kwanza katika Utumishi wa Umma anapaswa kutoa taarifa zifuatazo:-

Kwanza, Kanuni ya Namba D.18 inamwelekeza kupima afya yake ili kumwezesha mwajiri kutambua kama atafaa kwa kazi aliyoomba.

Pili, Kanuni ya D.30 inamwelekeza kutoa taarifa kuhusu warithi wake kwa kujaza kadi maalum ya *Next of Kin Card*.

Tatu, Kanuni ya D.31 inamwelekeza kutoa taarifa binafsi katika fomu maalum inayoitwa *Personal Record Form* ambapo pamoja na mambo mengine mtumishi

atatakiwa kujaza tarehe, mwezi na mwaka wa kuzaliwa na kiwango cha Elimu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi ni za muhimu sana kwa kuwa zinamsaidia mwajiri na mtumishi mwenyewe katika masuala mbalimbali ya kiutumishi ikiwa ni pamoa na kutambua muda wa kustaafu kazi. Kwa hiyo, zinapaswa kujazwa kwa usahihi na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swal la Mheshimiwa Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya F.47 ya Kanuni nilizozitaja hapo juu wakati wa kutambua muda wa kustaafu kazi wa mtumishi iwapo *form* ya taarifa binafsi itaonekana kuwa alijaza mwaka peke yake wa kuzaliwa bila tarehe wala mwezi mtumishi huyo atatambulika kuwa alizaliwa tarehe 1 Julai, ya mwaka ule alioutaja. Na ikiwa atakuwa alijaza mwezi na mwaka tu bila tarehe basi atatambulika kuwa alizaliwa tarehe 16 ya mwezi na mwaka ule alioutaja na taarifa zake zote za kiutumishi zitaandaliwa kwa kuzingatia tarehe hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za F.48 (a) na F.50 (b) ya Kanuni nilizozitaja hapo juu watumishi wanatakiwa kutoa taarifa kwa waajiri wao kwa maandishi miezi 6 kabla ya tarehe ya kustaafu. Aidha kwa Kanuni ya F.50 (e) inamwelekeza mwajiri vilevile kufuatilia kwa karibu na kumfahamisha mtumishi kuhusu tarehe ya kustaafu kwake na kuhakikisha kuwa mtumishi haendelei kufanya kazi baada ya kufikia umri wa kustaafu kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuzingatia Kanuni hizo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa barua yake yenye Kumb. Na. MUF/3/33/464/A/117 ya tarehe 27 Oktoba, 1997 iliwakumbusha waajiri wote na kuwataka wazingatie Kanuni hizo kikamilifu na wajibu wao wa kuwakumbusha watumishi.

Na. 187

Upandishaji Vyeo Watumishi wa Serikali

MHE. HAMIS J. NGULI (K.n.y. MHE. MGANA I. MSINDAI) aliuliza:-

Je, Serikali imefikia wapi katika kupandisha vyeo Watumishi wa Serikali wakiwemo:-

(a) Walimu wale wa zamani na hawa wapya ambao wanajikuta wamelundikana sehemu moja bila kujali waliotangulia kuajiriwa, elimu na kadhalika?

(b) Je, ni kitu gani kilisababisha msongamano huo na Serikali imechukua hatua gani kuondokana na hali hiyo isije kurudia tena?

(c) Kwa kuwa, Serikali imebadilisha utaratibu wake wakuwapandisha vyeo Watumishi wake kwa kuingia mkataba kati ya Mwajiri na Mwajiriwa na wakati huo huo vitendea kazi bado ni duni na haba mpango wenyewe haueleweki kama vile walimu kukosa vitabu na vifaa vingine vya kufundishia. Je, utaratibu huo utafanikiwa kwa kutumia vigezo gani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha Utumishi wa Umma Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kufanya zoezi la tathmini ya kazi ambapo miundo ya Utumishi ilipunguzwa kutoka 260 hadi 163 zoezi hilo lilifanyika kwa kuunganisha kada zinazofanana kimajukumu na kielimu, matokeo yake ikiwa ni kupunguza ngazi zilizopo katika miundo ya Utumishi ili zilingane na ngazi mpya za mishahara zoezi hili ambalo lilikamilika mwaka 2003 limesaidia sana kuboresha mfumo wa mishahara katika Utumishi wa Umma kwa kupunguza ngazi za kupanda hivyo watumishi kuchukua muda mfupi kupanda kama atakuwa na sifa stahili na bidii kazini.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa zoezi hili na tathmini ya kazi yamejitokeza matatizo hususan ya mlundikano wa Watumishi wa muundo tofauti katika kazi. Sababu ya msingi ikiwa ni watumishi waliocheleweshwa kupandishwa vyeo kujikuta wamekuwa ngazi moja na wale walioajiriwa nyuma. Serikali inatambua kuwepo kwa tatizo hili na imechukua hatua kwa kuwaagiza waajiri mbalimbali kukamilisha zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi kabla ya kuanza utekelezaji wa zoezi hili la tathmini ya kazi.

Pamoja na hatua hiyo, Serikali imetoa Waraka Na. C/CB/178/123/01/17 wa tarehe 10/3/2005 kwenda kwa waajiri wote kuwataka wawasilishe katika Ofisi yangu taarifa kuhusu Watumishi wote walolundikana katika cheo kimoja kwa madhumuni ya kuelewa ukubwa wa tatizo na kisha kuchukua hatua nyingine za lazima.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kifungu Na. 6 (1) (a) na (b) mamlaka kuhusu ajira, upandishwaji vyeo na uthibitishwaji kazini kwa Watumishi, yamepelekwa kwa waajiri. Aidha, ni kweli pia kwamba, upandishwaji vyeo utazingatia matokeo ya kazi na kwamba, mwajiri na mtumishi watawekeana mkataba wa kazi ambaa upimaji wake utafanyika kwa uwazi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli vilevile kwamba mkataba huu wa kazi unamatamka mtumishi na mwajiriwa kuzingatia suala la vitendea kazi vitakazohitajika katika kufikia makubaliano hayo. Ninapenda kuwaondoa hofu watumishi kuwa kukosekana kwa

vitendea kazi hakutegemewi kuathiri utendaji kazi kwa watumishi kwani atakuwa na nafasi ya kueleza sababu zilizomfanya asitekeleze malengo yake ikiwa ni pamoja na suala la vitendea kazi. Mtumishi hawezi kuadhibiwa kutokana na mwajiri kushindwa kumpatia vitendea kazi.

MHE. HAMIS J. NGULI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Lakini je, kwa kuwa wapo watumishi wengine ambaao wamesimama kwa muda mrefu kupandishwa vyeo na sasa hivi wako karibu hata kustaafu. Na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anasema mpaka taarifa zipelekwe kwake ili aweze kutathimini ni ukubwa kiasi gani ambaao watumishi hao wapo.

Je, atawahi kiasi gani kuweza kuwapandisha hao watumishi vyeo ambaao wengine tayari sasa hivi wamekaribia kustaafu?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu huu wa kuwapandisha watumishi vyeo kulingana na kazi wanazozifanya bado mpya ni kiasi gani elimu imetolewa kwa ajili ya kuelimisha kwanza waajiri pamoja na watumishi wenyewe hasa vijijini? Ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali miwili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nguli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kati ya wale ambaao wameathirika na utekelezaji wa tathmini ya kazi ni pamoja na wale ambaao karibu wanastaafu na kwa mujibu wa barua tuliotuma au waraka tuliotuma tumewaomba waajiri wahakikishe wanazifikisha taarifa hizo mapema na Ofisi yangu itahakikisha kwamba inachukua hatua ya kuwakumbusha ili walete taarifa.

Lakini endapo mtumishi amefkia wakati wa kustaafu na anaona haki haitazingatiwa basi vilevile anaruhusiwa ye ye mwenyewe kuleta taarifa hiyo na watumishi wanajua taratibu za kufuata. Kuhusu swali la pili, ni kwa kiasi gani tumetoa elimu kuhusu utekelezaji wa sheria Na.8 ya mwaka 2002 Naomba niwakumbushe watumishi wote na waajiri wote kwamba hili ni suala la sheria na Ofisi yangu itajitahidi sana kuwaelimisha watu na imeshaanza kuelimisha na itaendelea kuelimisha lakini watumishi na waajiri vilevile wanapaswa kupata sheria hiyo na kuisoma vizuri na kuielewa pale ambapo hawaelewi basi Ofisi iko tayari kutoa ufanuzi wowote.

MHE. PAUL E. NTWINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali inafanya zoezi katika kuboresha watumishi wake walioko kwenye msongamano na kadhalika na kwa kuwa upo upungufu mkubwa wa walimu nchini na juzi wamefanya *interview* pale Chuo cha Kigurunyembe wamejitokeza vijana zaidi ya 4000 lakini wanaochukuliwa ni 300 tu.

Je, Serikali ina mpango gani sasa kuboresha na hilo?

SPIKA: Ni swali jipya lakini Waziri sijui kama una majibu? Haya jaribu Mheshimiwa Waziri..

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ntwina, kama ifuatavyo:-

Ni kweli Waheshimiwa Wabunge na wananchi wengi wanajua kwamba katika kutekeleza MMEM tumeongeza shule nyingi na tumeongeza madarasa mengi na kwa hivyo watoto walioandikishwa shule wamekuwa wengi sana. Wingi huu wa wanafunzi unapaswa uende sambamba na wingi wa walimu lakini ni kweli kwamba kuna upungufu hata hivyo Serikali inajitahidi sana kuona kwamba ingawa wote wanaotaka kuwa walimu hawapati nafasi lakini kila mwaka tunajitahidi kuongeza idadi ya walimu ambao watapelekwa mafunzoni na kuongeza Bajeti ya Serikali lakini nina hakika Waziri wa Elimu anayekuja kujibu swali baada yangu atalijibu hili vizuri zaidi.

Lakini kwa upande wa watumishi na hasa walimu, Serikali inajitahidi kuitia waajiri mbalimbali kuboresha hali ya wale ambao wanafundisha kusudi mradi huu wa MMEM uwe na matokeo mazuri zaidi.

Na. 188

Shule ya Sekondari ya Matanda.

MHE. OMARY MOHAMMED MWENDA aliuliza:-

Kwa kuwa Shule ya Sekondari ya Matanda ina Waalimu wawili tu hivyo kufanya wanafunzi waliopo shulenai hapo kushindwa kupata elimu inayotakiwa na kwa kuwa katika wanafunzi wa kidato cha pili na cha nne ambao wanatarajia kufanya mitihani yao ya mwisho wa mwaka huu:-

- (a) Je, ni nini matarajio ya Serikali kwa wanafunzi hao?
- (b) Je, Serikali haioni kwa hali hiyo inachangia kufeli kwa wanafunzi hao, na inachukua hatua gani za makusudi kuondoa tatizo hilo?

WAZIRI WA ELIMU UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Mohammed Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2003-2005 walimu 6 wa masomo ya Sanaa na walimu 3 wa masomo ya Sayansi, jumla walimu 9 walipangwa katika Shule ya Sekondari Matanda. Matarajio yetu yalikuwa walimu hao watasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa

walimu katika shule hiyo, na hivyo kuwasaidia wanafunzi wa Kidato cha Pili, na cha Nne kufanya vizuri katika mitihani yao. Hata hivyo, walimu wote hao hawakuripoti katika shule hiyo isipokuwa Mwalimu Urban Lucas pekee ndiye aliyeripoti na kubakia kituoni. Nimeagiza walimu hao ambao hawakuripoti waandikiwe ili kujieleza kwa nini wasifukuzwe kazi na ualimu.

(b) Mheshimiwa Spika, hatua za haraka zilizochukuliwa kuwasaidia wanafunzi wote wakiwemo wa K.2 na cha K.4 wa shule hiyo ni kuazima walimu wenye Stashahada wanaofundisha katika shule za Msingi walioko katika Wilaya hiyo. Jumla ya walimu 2 wamepatikana ili kusaidia kupunguza makali ya tatizo hili na kufanya idadi ya walimu katika shule hiyo kuwa watano akiwemo mmoja wa kujitolea. Serikali pia imetoa ruzuku ya shilingi milioni 9 isaidie kujenga nyumba ya mwalimu. Juhudi zinaendelea kutafuta walimu zaidi kwa ajili ya shule hiyo na nyininge zenye uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Spika, juhudi hizo ni pamoja na zifuatazo:-

Kwanza, Kuajiri waliofaulu kidato cha 6 na wahitimu wa Chuo Kikuu wasio na vyetu vya ualimu ambao wanapatiwa mafunzo ya muda mfupi (*Induction Course*) kuhusu mbinu za kufundisha. Kwa mfano tarehe 9/6/2005 tukiwa hapa Bungeni, Wizara yangu imetangaza nafasi 374 kwa wahitimu wa K.6 kutuma maombi yao katika Chuo cha Ualimu cha Morogoro pale Kigurunyembe na Butimba, Mwanza ili waweze kupatiwa mafunzo ya mwezi mmoja na kisha kupangiwa vituo vya kazi. Mafunzo hayo yameanza tarehe 4/7/2005.

Mbili, Kuajiri walimu wote wenye Stashahada ya ualimu.

Tatu, Kuongeza nafasi katika Vyuo vya Ualimu vilivyopo ili kuchukua waalimu tarajali wengi zaidi.

Nne Kubadilisha Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam na Shule ya Sekondari ya Mkwawa kuwa Vyuo Vikuu vishiriki vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo cha Ualimu na cha Ufundı Mtwara kuwa Chuo Kikuu ambata cha Chuo Kikuu Dar es Salaam vitakavyotoa Shahada ya Elimu ya Ualimu kwa ajili walimu wa shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

MHE. OMARI MOHAMMED MWENDA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kumuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, shule hiyo ina uhaba wa walimu na tunauhakika baadhi ya masomo wanayakosa wanafunzi hao kama vile masomo ya sayansi na masomo hayo yatajitokeza katika mtihani wao na kama yatajitokeza kwa vyovyyote vile watafeli.

(a) Je, Serikali inaasemaje kwa wanafunzi hawa?

(b) Kwa kuwa, walimu walipangwa kwenda huko na wao hawakuripoti na Serikali imesuasua kuwachukulia hatua, Je, Serikali itakuwa tayari kuwalipa fidia wanafunzi hao watakapofeli?

WAZIRI WA ELIMU UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Omar Mwenda maswali yake miwili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda nikubaliane naye kabisa katika lile swal la kwanza kwamba kama hatukuwa na walimu wa kutosha katika shule ni lazima wanafunzi wataathirika kwa hiyo huo ni upungufu ambao napenda kukiri siyo katika shule hiyo moja tu iko katika shule kadhaa.

Tunachojitahidi kufanya ni kwamba tukijua kuna matatizo na tukijua mapema zaidi tunachukua hatua ya haraka zaidi.

La pili kwamba je wanafunzi hao wakifeli kwa sababu hatukupanga walimu je tunaweza kuwafidia. Utaratibu huo haupo tunaendesa elimu katika nchi kwa kufuata sheria ya elimu. Mimi ninachotaka kusema ni kwamba tumeliona na niseme kama Waziri nimeliona tatizo la usimamiaji wa shule zetu za Sekondari kwamba ule utaratibu uliokuwepo wakati tuna shule chini ya 100 leo hii hautufai wakati tuna shule zaidi kidogo ya 1700 kwa hiyo tuma katika kutekeleza utaratibu mpya kwanza tumetoa madaraka, bodi za shule ziteuliwe na wakuu wa mikoa, lakini pia tuko katika mchakato wa kutoa madaraka zaidi ya usimamiaji wa waajiri na uhamishaji wa walimu katika shule za Sekondari kuhamisha kutoka Wizarani kwa Mkurugenzi wa Sekondari kwenda mikoani na zoezi hili nina hakika nitalikamilisha kabla ya Uchaguzi Mkuu na itaongeza ufanisi. (*Makofî*)

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Kwa kuwa kosa la kutokuwa na walimu kwa skuli ya sekondari ya Matanda ni kosa la Serikali na siyo kosa la wanafunzi na kwa kuwa kuna utaratibu kwa akima mama katika shughuli zao kupunguza *marks* zao kwa kupasi kuendelea mbele.

Je, Serikali iko tayari kufanya upendeleo maalum kwa skuli ya Sekondari ya Matanda na hiyo kuishusha *marks* zao ili kuweza kufanikisha kuendelea mbele?

WAZIRI WA ELIMU UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, swal lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Napenda nirudie nilichosema tunaendesa elimu kwa kufuata sheria ya elimu na sheria iliyounda Baraza la Mitihani, sasa utaratibu wa kusema kwamba kwa sababu kuweka walimu hawakuwepo wa kutosha utateremsha *marks* kwenye hiyo sheria ya Baraza la Mitihani kipengele hicho hakipo kwa hiyo hatuwezi kukitunga lakini zipo njia zingine ambazo kisheria tunayo madaraka ya kuweza kuzifanya kama mahali kwa mfano wameathirika kwa kiwango kikubwa na Mwalimu Mkuu pamoja na Bodi yake wakaleta maombi Wizarani kwamba wanafunzi wale hawajaandaliwa kiasi cha kutosha Waziri

akiridhika kwa madaraka aliyonayo anaweza akasema wale wanafunzi wangojee wasifanye mtihani wafanye mtihani mwaka unaofuata hilo linawezakana. Lakini kusema uteremshe *marks* utakuwa umeingilia kabisa utaratibu wa sheria.

Na. 189

Utekelezaji wa Mpango wa MMES

MHE. LUCAS L. SELELII aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imedhamiria kuunga mkono nguvu za wananchi pale wanapoamua kufanya shughuli za maendeleo yao kama ujenzi wa nyumba za walimu, vyoo na madarasa na kwa kuwa Mpango wa MMES ni mionganini mwa juhudi hizo za Serikali; na kwa kuwa katika Wilaya ya Nzega, fedha za Serikali zinaleta matatizo kufanya utekelezaji wake uwe na usumbufu:-

- (a) Je, kama ujenzi wa nyumba za walimu, vyoo na madarasa; na kwa kuwa Mpango wa MMES ni mionganini mwa juhudi hizo za Serikali na kwa kuwa katika Wilaya ya Nzega, fedha za Serikali zinaleta matatizo kufanya utekelezaji wake uwe na usumbufu:-
- (b) Je, Serikali iko tayari kutuma fedha za MMES moja kwa moja kwenye shule kuititia Halmashauri ya Wilaya?
- (c) Je, ni fedha kiasi gani zilipangwa katika Bajeti ya 2004/2005?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Lucas Selelili Mbunge wa Nzega lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari 2004-2009, Msimamiaji Mkuu wa Mpango huo ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kuititia Idara ya Elimu ya Sekondari. Mkuu wa Shule akishirikiana na Bodi ya Shule na Kamati ya Ujenzi wa Shule ni Msimamiaji Mkuu katika utekelezaji wa mpango huu katika ngazi ya shule.

Mpango huu umebuniwa na kuandaliwa kwa utaratibu huo ili kuzipunguzia Halmashauri mzigo wa kusimamia mipango yote miwili ya MMEM na MMES.

Kwa hiyo fedha za MMES zinatumwa moja kwa moja kwenye Akaunti za shule husika ambako zinatumika kwa hundi inayotolewa na Hazina ndogo kwa utaratibu wa sasa. Aidha, utaratibu wa kutuma fedha katika shule za sekondari ndiyo unaotumika katika kutuma fedha nyingine za uendeshaji wa shule hata kabla ya MMES kuanza.

Wizara yangu imeshauri kuwa mkataba wa mkopo urekebishwe ili Hazina Ndogo isihusike tena na fedha za MMES baada ya Hazina Kuu (*Treasury*) kuzitoa kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu ili ye ye awajibike bila kisingizio cha kucheleweshwa na Hazina Ndogo, naye pia aweze kuwawayibisha vizuri Wakuu wa Shule.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza MMES jumla ya shilingi bilioni 53.8 zilitengwa katika bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2004/2005. Hadi sasa jumla ya shilingi bilioni 43.1 zimetumwa shulenii kwa ajili ya shughuli mbalimbali za MMES, kama nitakavyofafanua katika hotuba yangu ya Bajeti kesho.

Aidha Wilaya ya Nzega imepewa Ruzuku ya Maendeleo ya shilingi Milioni 198 zikiwemo shilingi milioni 126 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 18 na shilingi milioni 72 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 8 za walimu.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri na kumpongeza kwamba sasa yuko tayari kubadilisha utaratibu ambao umekuwa ni usumbufu kwa ujenzi wa shule za Sekondari. Lakini nina maswali miwili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Sekondari inajumuisha madarasa, nyumba za walimu pamoja na majengo mengine ya maktaba, maabara na kadhalika, na kwa kuwa Serikali ilituma pesa za madarasa na nyumba za walimu pekee bila pesa za maabara na maktaba na vyoo.

Je, Serikali iko tayari kutuma pesa nyingine kwa ajili ya majengo ambayo yamesalia ya madarasa, maabara, maktaba pamoja na vyoo?

Pili, kwa kuwa wananchi hawa waliokuwa wanajenga wameathirika kwa sababu walikuwa wanatumia pesa zao kwa ajili ya nauli, wanatumia pesa zao kwa ajili ya malazi kufuata mkoani. Je, Serikali iko tayari kuagiza kwamba hizo pesa zilizoko mkoani zirudi wilayani mara moja kwenye *TRA* ili iwe karibu kufuatilia kwa urahisi zaidi?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali miwili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selelii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ruzuku ya maendeleo ambayo imetolewa katika mwaka wa kwanza wa Mpango huu wa MMES umelenga nyumba za walimu na madarasa. Lakini ningependa kukumbusha kwamba kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka jana ujenzi wa maabara tumeona kwamba ni jambo ambalo wananchi hawana uzoefu na ujuzi nalo wa kutosha. Kwa hiyo, tumeamua kwamba maabara zijengwe na Serikali. Kwa hiyo, katika shule zote ambazo zimeanzishwa tunacho kiporo cha kujenga maabara na katika Bajeti nitakayoiwasilisha kesho nitaeleza maabara ambazo tayari tumekwishazipatia fedha na nitaeleza pengo ambalo tunaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa maabara. Lakini jukumu hili tumeamua liwe ni la Serikali.

Sasa kuhusu majengo mengine kwa mfano, majengo ya maliwato na majengo ya utawala kusema kweli inawezekana kujenga majengo hayo kwa kutumia ruzuku hii ya maendeleo inayotolewa kwa ajili ya madarasa na nyumba za walimu. Kwa sababu ukiangalia na kila mmoja wetu akifanya hesabu kama ruzuku hii itatumika kama inavyotakiwa kwa maana ya kununulia vifaa vya ujenzi vinavyotengenezwa viwandani milioni 7 haimaliziki kwenye darasa moja popote katika Tanzania. Kwa hiyo, kinachohitajika ni kupanga fedha hizo ziende na kwenye majengo mengine na ndivyo ilivyotarajiwa na ndivyo ambavyo tunawaeleza ma-*headmaster* na viongozi wengine wanaosimamia utekelezaji wa mipango hiyo. Hili ninalolisema kwenye madarasa ndivyo lilivyo kwenye nyumba za walimu. Hata mimi kama Mbunge kwenye Jimbo langu naelewa kabisa milioni 7, milioni 9 zinaweza zikafikisha madarasa mawili pamoja na ziada kusaidia majengo hayo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa la pili, la kusema kufidia nauli kwa wale wanaofutilia. Utaratibu huo wa kufidia usuutiliaji haupo. Hiso ni shughuli ambazo zinaingia katika gharama zile za wananchi wanaojenga shule kujitolea wenyewe kama wanashindwa kupanga zile zinazobaki kama nilivyokwishaeleza kuweza kusaidia hapo, basi njia nyingine ni lile suala la *self help*.

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa kudumu ni kufanya marekebisho katika utaratibu ili fedha hizo ziende moja kwa moja kwenye akaunti ya shule wasilazimike tena kufutilia kwenda kwenye *Sub Treasury*. Mimi nina uhakika kwa ushirikiano na mwenzangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha tutakamilisha zoezi hili. (*Makofi*)

Na. 190

Mahitaji ya Maji – Kijiji cha Lwandai / Mlola

MHE. HENRY D. SHEKIFFU aliuliza:-

Kwa kuwa, Makao Makuu ya Tarafa ya Mlola yapo katika Kijiji cha Lwandai/Mlola na kwa kuwa Kijiji hicho kimepanuka kufikia hadhi ya kuwa Mji mdogo na hivyo kuwa na mahitaji makubwa ya maji; na kwa kuwa mfumo wa usambazaji wa maji katika Kijiji hicho ulijengwa kwenye miaka ya 1960 na kwa sasa hivi, Kijiji/ Mji huo mdogo umepanuka na kusababisha maji yanayopatikana sasa kutotosheleza hata kwa theluthi moja ya mahitaji ya maji kwa wakazi wake.

Je, Serikali itasaidiaje katika upanuzi wa usambazaji wa maji pamoja na kuimarisha chanzo cha maji ili kufikisha maji kwenye maeneo jirani ya Mazashai, Hugo na kadhalika?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Kijiji cha Lwandai/Mlola kina mradi wa maji uliojengwa mwaka 1955 kwa ajili ya kutoa huduma kwa wakazi 200 wakati huo. Mwaka 1991 vilichimbwa visima vifupi 5 ili kuimarisha huduma iliyokuwepo. Kijiji hiki kimepanuka kwa sasa na kunakadiriwa kuwa na wakazi 3,570 na hivyo kufanya mahitaji ya maji kuwa makubwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli maji yanayopatikana kwa sasa hayatoshelezi mahitaji ya wakazi wake kutokana na ongezeko kubwa la watu nililolitaja. Sababu nyingine zinazochangia kuwepo tatizo la upatikanaji wa maji ni pamoja na wananchi kulima kandokando ya vyanzo vya maji, kupungua kwa kipenyo cha mabomba kutokana na kujaa tope na kutu na uchakavu wa mradi huo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2004/2005 Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imeanza kufanya utafiti ili kuainisha mahitaji ya kuukarabati mradi uliopo ili uwezi kutoa huduma bora zaidi. Serikali pia inafanya uchunguzi wa nyanzo vingine vya maji ambavyo vinaweza kukidhi mahitaji ya maji kwa muda mrefu ujao. Kasi ya kufanya utafiti huo imekuwa ndogo kutokana na ukosefu wa fedha. Punde utafiti huo utakapokamilika, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto itafanya upembuzi yakinifu wa mradi huo ili kujua mahitaji halisi ya fedha kwa ajili ya kuukarabati na kuupanua mradi. Lengo la mpango huu ni kuimarisha huduma ya maji Kijijini Lwandai/Mlola pamoja na Vijiji jirani vya Mazashai na Hugo ili kuondoa kabisa tatizo la maji lililopo.

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza asiwe na *pressure*.

(a) Kwa kuwa katika eneo hili sasa kuna Taasisi mbili muhimu. Shule ya Sekondari ya Mlongwema na Kituo cha Afya na hapo kuna wananchi wengi ambao kwa kweli bila maji wanapata matatizo sana. Je, Serikali inahidi au itasaidiaje kuhakikisha kwamba Taasisi hizi angalau zinapata maji?

(b) Kwa kuwa upo mradi wa Benki ya Dunia ambapo Wilaya ya Lushoto pia ni mojawapo. Je, Serikali inatamka wazi kwamba itasaidia mradi huo wa maji ili wananchi wa vijiji vya Hugo, Lwandai pamoja Mazashai wapate maji?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO): Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba katika eneo hilo kuna hizo Taasisi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na ndiyo maana tumetaja hata idadi ya watumiaji wa maji imeongezeka katika eneo hilo kufikia 3,000 ukilinganisha na lengo la mradi lilivyojengwa na ndiyo maana sasa tunafanya upembuzi yakinifu kubainisha ukubwa wa tatizo hilo na hapo utakapokamilika upembuzi yakinifu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto inayohusika utafanywa utaratibu wa kutekeleza mradi huo kwa ushirikiano kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Wizara zinazohudumia Taasisi hizo kwa mfano, shule ya Sekondari inahudumiwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni na Kituo cha Afya hicho kinahudumiwa na Halmashauri bado ni jukumu la pale pale ndani Halmashauri kwa kushirikisha wadau wote wanaomiliki Taasisi hizo ili waweze kuchangia katika kutekeleza mradi huo utakapoanza. Juu ya Benki ya Dunia namwomba Mheshimiwa Henry Shekiffu kwenye hotuba yangu ya tarehe 15 Julai, mwaka huu tunayo maeleo ya kutosha juu ya mradi huo wa Benki ya Dunia. Naomba avute subira tutampa majibu ya kutosha tarehe 15 Julai, mwaka huu.

Na. 191

Umaskini kwa Wafugaji

MHE. GEORGE M. LUBELEJE (k.n.y. MHE. LEKULE M. LAIZER) aliuliza:-

Kwa kuwa umaskini umekithiri kwa wafugaji kutokana na ukame wa magonjwa ya mifugo ambayo yameathiri ustawi wa mifugo na wananchi wengi kubaki katika umaskini mkubwa na matokeo yake vijana wanakimbilia Mijini:-

(a) Je, Serikali itachukua hatua gani za makusudi kabisa za kusaidia wafugaji hao ili kuwawezesha wafugaji hao kujinasua na umaskini na vilevile kuwavutia vijana kubaki Vijijini na kuendeleza mifugo na hatimaye kujiongeza kipato?

(b) Kwa kuwa wafugaji wa Kenya ambao wamepakana nasi wanawezeshwa na Serikali yao kwa kuwanunulia madume ya kunenepesha na baadaye yanauzwa na kulipa deni na kubaki na fedha nyingi kwa wakopeshaji. Je, Serikali haiwezi kufanya hivyo kwa wafugaji wetu na hatimaye kuwavuta hao waliokimbilia Mjini warudi Vijijini ili kuendelea na shughuli za ufugaji?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, napenda jibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba uendelezaji wa ufugaji nchini unaathiriwa na kuwepo kwa ukame na kuenea kwa magonjwa ya mifugo na kuifanya Sekta ya Mifugo iwe na ustawi na tija ndogo na kusababisha wafugaji kubakia kwenye umaskini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliandaa mukutano wa Wadau wa Sekta ya Mifugo mwaka 2001, ambapo wadau waliainisha matatizo yanayoikabili Sekta hii kwa ujumla. Wadau hao pia waliweka dira ya Sekta ya Mifugo ambayo inaelekeza kwamba kuwe na ufugaji wa kisasa na wa kibiashara endelevu, wenye tija, utakaozalisha malighafi kwa usindikaji, na utakaoongeza pato la Taifa na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imezingatia sana maoni ya wadau na dira waliyoiweka kwa kuainisha mambo yote haya katika mipango na mikakati yake, ukiwemo MKUKUTA. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa na Wizara ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- Kujenga na kukarabati malambo 392 na majosho 804 kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Miji na wananchi;
- Kusambaza tani 19.3 za mbegu bora za malisho kwa wafugaji; na
- Kununua na kusambaza dozi 16,260,633 za chanjo dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu na dozi 175,000 dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha Mbwa. Juhudi kama hizi zimeiwesha nchi yetu kutokomeza ugonjwa wa Sotoka na kutambuliwa na Shirika la Afya la Mifugo Duniani, *OIE*.
- Kutoa mafunzo kwa wataalam 2,608 na wafugaji 4,615 katika Vyuo vya Mifugo na kuandaa makala 3,000 za vitabu kuhusu ufugaji bora.
- Kuzalisha na kusambaza mitamba 10,603 kutoka mashamba ya Mabuki, Nangaramo, *Sao Hill*, Ngerengere na Kitulo, na kuzalisha dozi 139,030 za mbegu bora katika Kituo cha *NAIC*.
- Kuimarisha miundo mbinu ya masoko ya mifugo kwa kujenga na kukarabati minada 56 na vituo 113, kukarabati mabehewa 60 ya kusafirisha mifugo na kujenga machinjo ya Dodoma.
- Kupima na kugawa maeneo katika Ranchi za Taifa 8 na mashamba 6 ya ng'ombe wa maziwa ambapo wawekezaji 53 wako katika hatua mbalimbali za kumilikishwa maeneo.

- Kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufanya marekebisho ya sheria ya magonjwa ya Mifugo, Sheria ya Utabibu wa Mifugo na Sheria ya Maziwa hivi karibuni.
- (b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya utaratibu wa kuwapatia wafugaji madume kwa ajili ya kuyanenepesha na baadaye kuyauza. Wizara yangu imeanza kutekeleza mpango kama huo kwa kushirikana na Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa. Wafugaji jirani na kiwanda hicho hupewa mafunzo kuhusu unenepeshaji.

Lengo ni kusambaza teknolojia hii kote nchini na tayari wafugaji 60 wamepata mafunzo. Maombi ya Mheshimiwa Lekule Laizer yatazingatiwa wakati mpango huu utakapoanza kusambazwa katika nchi nzima na Loliondo utafika.

SPIKA: Sawa. Kama Mheshimiwa Lekule Laizer angekuwepo angeridhika kabisa na jibu hili. Kwa hiyo, tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Ujenzi. (*Kicheko*)

Na. 192

Ujenzi wa Barabara kwa STABEX

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkutano wa Bajeti 2004/2005 Waziri wa Kilimo na Chakula alilieleza Bunge kuwa wataalamu wa kukagua barabara zinazostahili kujengwa kwa fedha za STABEX walikuwa wanamalizia kukagua barabara hizo na kwamba ujenzi ungeanza mapema mwezi Septemba:-

- (a) Je, ni barabara zipi zitanufaika na fedha hizo katika Wilaya ya Karagwe na kwa Jimbo la Kyerwa ni barabara zipi?
- (b) Je, kwa ujumla Mikoa yote inayozalisha kahawa imetengewa fedha kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benedicto Mutachoka Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali la namba 45 katika Mkutano huu huu, lililoulizwa na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa kiasi cha *Euro* milioni 10 zimetengwa na Jamuiya ya Nchi za Ulaya chini ya utaratibu wa STABEX kwa ajili ya kugharamia ukarabati wa barabara katika maeneo yanayozalisha kahawa kwa wingi nchini.

Jumuiya ya Nchi za Ulaya *EU* imefanya tathmini ya barabara katika maeneo hayo na kuchagua barabara zinazostahili kufanyiwa ukarabati.

Kutokana na tathmini hiyo, barabara zifuatazo zimechaguliwa kukarabatiwa katika Wilaya ya Karagwe:-

- (i) Kagenyi hadi Kyerwa yenze urefu wa kilometra 12.95;
- (ii) Kakanya kupitia Kikukuru hadi Kitwe yenze kilometra 13.80;
- (iii) Rugu hadi Ruhita yenze kilometra 7.20;
- (iv) Nyakagoyegoye hadi Rwabwere yenze kilometra 9.50;
- (v) Kigarama kupitia Mabira hadi Kyerwa yenze urefu wa kilometra 5.1; na
- (vi) Kihanga – Rwambaizi yenze kilometra 10.0

Kati ya hizo, barabara kutoka Kagenyi hadi Kyerwa, Kakanja kupitia Kikukuru hadi Kitwe na Kigarama kupitia Mabira hadi Kyerwa zipo katika Jimbo la Kyerwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Mikoa yote inayozalisha kahawa imetengewa jumla ya *Euro 8,925,756* kwa ajili ya kugharamia ukarabati wa barabara katika maeneo yanayozalisha kahawa kwa wingi nchini.

Kati ya hizo, Mkoa wa Arusha umetengewa *Euro 990,000* kwa ajili ya kukanjira jumla ya kilometra 32, Ruvuma *Euro 1,035* kwa ajili ya kilometra 40, Mbeya *Euro 2,019,650* kwa ajili ya kilometra 81.3, Kigoma *Euro 939,000* kwa ajili ya kilometra 48.6, Tanga *Euro 1,122,300* kwa ajili ya kilometra 38.7, Mara *Euro 600,000* kwa ajili ya kilometra 20, Kilimanjaro *Euro 1,184,628* kwa ajili ya kilometra 77.5 na Kagera *Euro 1,035,178* kwa ajili ya kilometra 127.55.

Aidha jumla ya *Euro 1,074,244* zimetengwa kwa ajili ya kugharamia uchambuzi yakinifu na usimamizi na utekelezaji. Hivyo kufanya jumla ya fedha zote kwa mradi kuwa *Euro* milioni 10.

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa fedha za *STABEX* zilikuwa nyingi; na kwa kuwa tulikuwa tukidai wakulima wagawiwe hizo fedha mikononi na *European Union* na Serikali wakakataa; na kwa kuwa fedha hizi milioni 10 zilizotengewa ni kidogo ikilinganishwa na hali za barabara zilivyo mbaya. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba sasa kuna haja ya kudai fedha

nyingine za nyongeza kama bilioni 5 ili ziweze kusaidia ujenzi wa barabara kama Rukulejo kwenda Kitwechenkura hadi Kitoma, *Katera station* hadi Kihanga na barabara zingine ikizingatiwa kwamba barabara za Wilaya ya Karagwe ni mbaya?

Swali la pili, kwa kuwa *European Union* walikuwa wanataka kukataa kutengeneza barabara za Mkoa wa Kagera kwa kisingizio kwamba barabara za Mkoa wa Kagera ni nzuri. Lakini kwa kuwa barabara za Wilaya ya Karagwe ni mbaya na hasa zile za Kyerwa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba tuwasiliane na Wilaya pamoja na Mkoa waweze kuleta mapendekezo mengine ili waweze kuongezewa fedha nyingine? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali haikukataa utaratibu waliokuwa wanataka wakulima bali *European Union* imekataa kwa sababu wanataka kuhakikisha kwamba fedha zinakwenda mahali ambapo wao wanataka ziende. Kwa hiyo, utaratibu mzima huu sasa unasimamiwa na *European Union*. Kwa hiyo, suala si kwenda kudai tena kama ipo haja ni kuomba.

Pili, Serikali haiwezi tena kupeleka maombi kwa madhumuni ya Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Mheshimiwa Mbunge ili zipate fedha zaidi. Kama ni maombi basi Serikali itapeleka maombi kwa niaba ya nchi nzima ili kila mahali ambapo wananchi wanazalisha kahawa kwa wingi nao vilevile wafaidike kwa maombi hayo na sababu mojawapo ambayo ni kubwa sana kwa Mkoa wa Kagera na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi alifika Ofisini kwangu kwa nini ilikuwa ni vigumu sana kutengeneza barabara za Mkoa wa Kagera kwa sababu wenzetu Mkoa wa Kagera barabara zao mpaka za Wilaya ni nzuri. (*Makofi*)

MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja tu la nyongeza. Hivi hizo fedha za *STABEX* wakulima wamekuwa wakilalamika kwamba wapewe hizo fedha mkononi kwa sababu wana miche hiyo ya kahawa na wanafahamika.

Zoezi hilo limeshindikana na wanaendelea kulalamika. Sasa huo utaratibu wa kuwatengenezea barabara. Hivi anataka kuniambia kwamba hao wakulima wanahuishwa au ni mtu anaamua tu kwamba utatengenezewa barabara na pengine hajji kujitokeza tukakuta kwamba zile barabara ambazo zinawalenga wale wakulima wa kahawa hazitatengenezwa, zikatengenezwa barabara za sehemu nyingine tu Mheshimiwa Naibu Waziri anakubaliana na mimi kuhusu hilo.

Je, kuna mkutano mzuri unaofanyika kati ya wakulima hao na hao wanakuja kutengeneza hizo barabara au *European Union* wenyewe wanawahuishwa hao wakulima?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, *European Union* ilikataa kabisa kugawa fedha hizo kwa watu kwa kuwapa mkononi, hata kama wangekuwa waaminifu kwamba wangenunuliwa miche wapewe. Wao wamezingatia kwamba kitu muhimu kwao ni kuwatengenezea barabara ambazo watasafirishia kahawa zao na kule

kwenye sehemu ambapo wananchi wanazalisha kahawa kwa wingi. Maeno hayo ni ya muhimu sana, kule wakozalisha kahawa kwa wingi ndivyo walikopanga.

Jinsi gani wananchi wanahuishwa. Wananchi wana wawakilishi wao katika hatua mbalimbali na hii hatua ambayo *RAFTON International* ilikubaliana na *European Union* ni kwenda kwa wawakilishi wa wananchi amba ni Halmashauri na kuzungumza nazo.

Halmashauri zote nchini ambazo zinahusika kwenye suala hili na kupanga hizo barabara. Kwa hiyo, wamewakilishwa kwa aina moja ama nyingine kama sisi tunavyowakilisha wananchi hapa.

Na. 193

Rushwa katika Utoaji wa Mikopo

MHE. FRANK G. MAGHOBA (K.n.y. MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA) aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na tuhuma za rushwa katika utoaji wa mikopo katika Mabenki na Taasisi mbalimbali za fedha hapa nchini:-

- (a) Je, ni kweli kumekuwepo na rushwa katika utoaji wa mikopo kama inavyodaiwa?
- (b) Je, ni kweli kuwa kumekuwepo na rushwa katika utoaji wa mikopo ya *Japanese Import Support*?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA ((MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, naomba kutoa maelezo mafupi kwamba chini ya Sheria husika. Benki Kuu ya Tanzania ndiyo yenyenye mamlaka ya kudhibiti mienendo ya kicutendaji na kimaadili ya mabenki na Taasisi za Fedha nchini na kuchukua hatua pale inapobaini kasoro. Hadi sasa Benki kuu hajabaini vitendo vya rushwa katika utoaji wa mikopo kwenye benki na vyombo vya fedha kwa ujumla.

Aidha, Mfuko wa *Commodity Import Support (CIS)* ulianzishwa miaka ya 1980 na baadhi ya nchi wafadhili wa Tanzania ikiwemo Japani, kwa lengo la kuipatia fedha za kigeni za kununulia malighafi, vyombo vya usafiri wa barabara, vifaa vya kilimo, ujenzi na kadhalika. Wakati huo hali yetu ya uchumi hususan ya upatikanaji wa fedha za kigeni ilikuwa mbaya sana hivyo mpango huu ulikuwa usaidie kuinusuru hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa *CIS* ultawaliwa na Kamati Maalum kwa mujibu wa sheria ya mwaka 1993/1994, ilijojumuisha Wizara ya Fedha, iliyokuwa Idara ya Kodi ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania. Baadaye Wizara za Mipango, Viwanda na Biashara walijumuishwa.

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako litakavyokumbuka, mwaka 2002 lilipitisha sheria ya kurekebisha utaratibu wa kutoa mikopo ya *CIS* kwa kuhamishia madaraka hayo Benki ya Raslimali (*TIB*) kama Wakala wa Serikali. Tangu mwaka 2004 Japani ilisitisha utoaji wa misaada ya *CIS* na badala yake hutoa katika utaratibu wa wafadhili kuchangia bajeti ya Serikali kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ya bajeti. Hivi sasa *TIB* inaendelea kukusanya madeni ya waliokopa, ikisaidiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu sehemu (a) na (b) za swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haina taarifa kama kumekuwepo tuhuma za vitendo vya rushwa katika utoaji wa mikopo katika mabenki na Taasisi mbalimbali za fedha nchini. Kama Mheshimiwa Mgaywa au mtu mwingine ye yeyote anajua benki au Taasisi ya fedha yeyote nchini ambayo mikopo yake ilitolewa kwa kutoa na kupokea rushwa, tunamwomba apeleke taarifa hizo Polisi au Taasisi ya Kuzuia Rushwa au Wizara ya Fedha au Benki Kuu ili hatua zinazofaa ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msaada wa *Import Support* kutoka Japani Wizara yangu pia haifahamu kuwepo kwa vitendo vya rushwa katika utoaji wa mikopo chini ya mpango huo, hasa kwa sababu utoaji wa mikopo hiyo haukumruhusu Afisa mmoja kutoa uamuzi kama nilivyoeleza hapo awali.

Hata hivyo, kwa kuwa maombi yalikuwa mengi mno kulinganishwa na fedha zilizokuwepo, ni wachche waliofanikiwa kupata mikopo hiyo. Hali hiyo inaweza ikaleta hisia potofu kwamba, hao walifanikiwa, walifanikiwa kutokana na rushwa.

Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 1999/2000 maombi yaliyopokelewa yalikuwa zaidi ya 1000, wakati fedha zilizokuwepo zilitosha kutoa mikopo kwa waombaji wasiozidi 100. Hata hivyo nitafurahi kupata habari za rushwa husika kama zipo, ili nichukue hatua ipasavyo.

Na. 194

Mafao na Mizigo ya Marehemu Meja Sekiondo

MHE. HENRY D. SHEKIFFU (K.n.y. MHE. CHARLES H. KAGONJI)
aliuliza:-

Kwa kuwa familia ya Marehemu Meja Timothy K. Sekiondo aliyesariki dunia tarehe 30 Machi, 2003 huko Songea bado inaendelea kuteseka wakisubiri mafao

mengine na mizigo ya Marehemu kuletwa nyumbani kwao huko Mtae; na kwa kuwa hata pamoja na Mbunge wao kufuutilia suala hilo kwa barua ya tarehe 3 Novemba, 2004 kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara husika bado hakuna majibu wala hatua zozote zinazoonekana kuchukuliwa na Wizara juu ya tatizo hilo:-

(a) Je, kwa nini Serikali kupitia Wizara hii inadharau kazi halali za Kikatiba za Wabunge katika kufuutilia shida/ matatizo ya haki za msingi za wananchi wanaowawakilisha Bungeni?

(b) Je, kwa kutojibu barua ya Mbunge kwa muda wote huo mrefu, kunamaanisha nini. Je, huo ni Utawala Bora?

(c) Je, kwa swali hili, suala hilo limefikia wapi?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa haijawahi wala haina nia ya kudharau kazi halali za Kikatiba za Waheshimiwa Wabunge katika kufuutilia shida na matatizo ya haki za msingi za wananchi wanao wawakilishia Bungeni, bali Serikali imekuwa ikishirikiana na Waheshimiwa Wabunge katika kufuutilia na kushughulikia shida na matatizo ya haki za msingi za wananchi. Serikali inawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Kagonji kwa juhudui zao za kuwasaidia wananchi katika kutafuta haki zao.

(b) Mheshimiwa Spika, barua ya Mheshimiwa Mbunge ilinifikia Ofisini kwangu tarehe 8/12/2004 na kuanza kufanyiwa kazi kwa kushirikiana na Makao Makuu ya Jeshi. Nilimjibu Mheshimiwa Mbunge kwa barua Na.EA79/371/01 ya tarehe 9/5/2005 kumjulisha kuwa suala la mhusika linashughulikiwa. Hii ilitokana kwamba ilibidi kupata majibu sahihi kwa kuzingatia kuwa malipo ya mafao hupitia ngazi mbalimbali zikiwemo za kisheria. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge Kagonji na Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu inayoongozwa na Mheshimiwa Rais William Benjamin Mkapa inazingatia sana Utawala Bora na Haki za Binadamu. Mheshimiwa Kagonji na Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi.

(c) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeshughulikia mafao na usafirishaji wa mizigo ya Marehemu Meja Timothy Sekiondo ambayo yalikuwa yanafuutiliwa na msimamizi wa mirathi aliyeuleuliwa na familia na kuidhinishwa na Mahakama ya Mwanzo Mchungaji Zephania Kasinda. Tarehe 17/2/2005 Hazina ilitoa hundi ya mafao Tsh.15,260,266.65 na malipo ya watoto Tshs.82,044.40, jumla ni Tsh.15,342,311.05 ambazo alikabidhiwa msimamizi wa mirathi. Mwezi Juni, 2003 Makao Makuu ya Jeshi ilituma Tshs. 1,004,680/= Kikosini kwa Marehemu kwa ajili ya kusafirishia mizigo na familia. Msimamizi wa mirathi alijulishwa kwenda Songea kuchukua fedha hizo lakini hadi sasa bado hajaenda kuchukua.Napenda

kumpongeza Mheshimiwa Kagonji kama ilivyo kawaida yake kwa kufuatilia kwa karibu matatizo ya wapiga kura wake. Mimi ni shahidi jinsi alivyoshughulikia tatizo sugu la ugonjwa wa Tauni ambao sasa ni suala la historia katika Jimbo la Mlalo. Namwomba Mheshimiwa Charles Kagonji amfahamishe mke wa marehemu hali halisi ya mafao na fedha za usafiri na kwamba Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeshughulikia suala lake ipasavyo.

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kwamba tatizo hili sasa limepata ufumbuzi. Nina swal dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa tatizo hili lipo katika maeneo mengi na yeye mwenyewe ni shahidi kuna mama hapo awali aliwahi kuja analia na akamchukua kwa moyo na Mheshimiwa Waziri ana moyo sana kweli wa kusaidia. Je, ni hatua gani zinachukuliwa ili kuepukana na matatizo hayo yanayowasumbua Wanajeshi kwa sababu ni watu waliota nafsi zao kulitetea Taifa hili. (*Makofi*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, tatizo la mafao la wanajeshi waliokufa na waliohai ni tatizo sugu la muda mrefu. Kuanzia mwaka 2001 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wakishirikiana na Makao Makuu ya Jeshi wameanza utaratibu wa kuingiza katika kompyuta taarifa na kumbukumbu zote za wanajeshi. Kwa hiyo basi, wanajeshi ambao wamestaafu kuanzia mwaka 2001 tatizo hilo sasa halipo.

Tatizo lililopo ni kuhusu wanajeshi waliostaafu kuanzia mwaka 2001 na kurudi nyuma. Hata hivyo tatizo hili Wizara limelivalia njuga kama ifuatavyo. Kitengo cha Kushughulikia Mafao ya Wastaafu kimeanza utaratibu wa kuwatuma wanajeshi na wataalamu katika mikoa kufuatilia matatizo haya na mafanikio ni kama ifuatavyo. Kuanzia mwaka 2001 jumla ya wanajeshi 2,712 hasa wale ambao wametutangulia mbele ya haki mafaili yao yameshughulikiwa. Ni pamoja na huyo mama ambaye umemweleza na nilikutana naye. Kati ya hao 2,370 hundi zimeandaliwa ziko Hazina na waliobaki 342 tu hundi zinashughulikiwa na tatizo hili litakwisha punde. (*Makofi*)

Na. 195

Jeshi la Ulinzi Kutumia Eneo la Unguja Ukuu

MHE. YAHYA KASSIM ISSA aliuliza:-

Kwa kuwa, Jeshi la Ulinzi linatumia eneo la Unguja Ukuu kwa shughuli mbalimbali za kijeshi; na kwamba, inasemekana kuwa wanataka kuongeza hadi kufikia Kibonde Maji na Kijiji cha Ujamaa katika eneo la Cheju:-

- (a) Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hilo?
- (b) Kama jibu katika sehemu “a” ya swal hili ni “ndiyo”. Je, inawafikiria nini wakazi wa maeneo hayo hasa ikizingatiwa ukosefu wa ardhi kwa eneo la Zanzibar?

- (c) Kama jibu katika sehemu “a” ya swali hili ni “sivyo” Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa kijiji cha Kibonde Maji na Kijiji cha Ujamaa ili waondokane na wasi wasi juu ya jambo hilo?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania halijawahi kuvamia, halitavamia wala halina tabia ya kuvamia maeneo ya raia, kinyume chake maeneo mengi ya Jeshi yalivamiwa na raia na kuyafanya shughuli zao. Ili kujenga mazingira mazuri kati ya jeshi na wananchi wao, maeneo kadhaa ya Jeshi yakiwa ni pamoja na yale ya Makazi, makambi, maeneo ya mazoezi na maeneo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali yamekwisha pimwa.

Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na Changanyikeni, Kigamboni, Kimbiji, Kipunguni, Kunduchi, Mbagala, Mgulani – Mkoa wa Dar es Salaam. Pangawe na Wami/Mbiki – Dakawa – Morogoro. Ruvu, Kibaha na Msata – Pwani. Makidila Tanga. Bonde la Lulunde na Zanka – Dodoma/Kambi ya Sokoine – Arusha. Maeneo yote ya Jeshi Mtwara. Kaboya, Kyaka na Biharamulo – Kagera, kwa Wahaya.

Mheshimiwa Spika, ili kumaliza migogoro iliyokuwepo na iliyojitokeza kati ya Jeshi na wananchi, Serikali imekubali kulipa fidia kwa baadhi ya wananchi kwa ajili ya mali zao zilizokuwa kwenye maeneo ya Tondoroni – Kibaha, Welezo, Zanzibar na Oldonyo Sambu Arusha. Zoezi la ulipaji fidia linaendelea. Hata hivyo, iwapo Jeshi linataka kuongeza eneo kwa ajili ya shughuli za kijeshi, litafanya hivyo kwa kuzingatia sheria za nchi. (*Makofii*)

- (b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jibu la sehemu (a) ni sivyo, hivyo basi, Serikali haifikirii chochote kuhusiana na ukosefu wa ardhi kwa eneo la Zanzibar.

- (c) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa JWTZ halina mpango wa kuongeza eneo la mafunzo katika maeneo ya Kibonde Maji na Cheju, Serikali inapenda kuwahakikishia wananchi wa Kibonde Maji na eneo lote la Cheju kuwa eneo hilo halitachukuliwa na Serikali kwa matumizi ya kijeshi. Hivyo basi Serikali inawaomba wananchi wasiwe na wasiwasi wowote badala yake waendelee na shughuli zao za kujenga na kulinda Taifa letu la Tanzania. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yote ya msingi yamejibiwa. Kwa hiyo, unaendelea sasa na shughuli nyingine tukianza na matangazo ya vikao vya leo. Ni Kamati mbili zimejipangia kufanya mikutano. Kamati ya kwanza ni Kamati ya Huduma za Jamii. Mheshimiwa Omar Kwaangw’, Mwenyekiti anaomba Wajumbe wake wakutane leo tarehe 4 Julai, 2005 saa 5.00 asubuhi katika chumba na. 227. Kamati ya pili, ni Kamati ya Hesabu za Serikali

PAC. Makamu Mwenyekiti, Prof. Mwakyusa, anaomba Wajumbe wa PAC wakutane leo tarehe 4 Julai, 2005 saa 4.30 asubuhi hii katika chumba 231. Mwisho wa matangazo ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge napenda kuwaarifu kwamba mimi nimeombwa na Mheshimiwa Rais William Mkapa, nimwakilishe kama mgeni rasmi katika shughuli ambayo angeifanya ye ye kesho kule Dar es Salaam. Kwa hiyo, sitakuwepo Bungeni kwa ajili ya kutekeleza wajibu huo pamoja na kazi nyingine huko Dar es Salaam. Kwa hiyo, kwa wiki hii vikao vya Bunge vitaongozwa na Mheshimiwa Naibu Spika akisaidiwa na Wenyeviti wenzetu kama kawaida. (*Makofî*)

Tunaendelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2005/2006 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:

Mheshimiwa Spika, baada ya taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, iliyochambua Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tufuku lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze hotuba yangu kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa kuweza kuliongoza taifa letu kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 1995 hadi mwaka huu anapomaliza muda wake. Katika kipindi hiki, ameonyesha umahiri mkubwa wa uongozi katika nyanja zote za maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na mambo mengine, uongozi wake umewezesha uchumi wa nchi yetu kukua kutoka asilimia 4 mwaka 1995 hadi asilimia 6 mwaka huu, huduma za kijamii zimeendelea kuimarika na miundo mbini imekuwa bora zaidi. Hali kadhalika, kwa jitihada hizo hivi sasa nchi yetu ni moja ya nchi zilizo katika orodha ya kupunguziwa sehemu ya deni lake la nje kutohana na kuwepo kwa mfumo imara wa utawala bora.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa juhudzi zake kubwa za kumshauri Mheshimiwa Rais na za kuimarisha Muungano na kwa kuhamasisha utekelezaji wa Sera mbali mbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa uzito huo huo, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Waziri Mkuu na Mbunge wa Hanang, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na

Ubinafsishaji na Mbunge wa Handeni, na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha na Mbunge wa Rombo kwa hotuba zao nzuri zilizotoa mwelekeo wa hali ya uchumi na Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2005/2006. Malengo, maelekezo na vigezo vilivyomo kwenye Hotuba hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha miaka kumi, wewe, Mheshimiwa Spika, umeonyesha uhodari mkubwa katika kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge. Nachukua nafasi hii kukupongeza kwa kazi nzuri unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu tukufu kwa utulivu na hekima kubwa. Nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti kwa kuliongoza Bunge wakati ulipokuwa na majukumu mengine nje ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete (Mb.), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa kupitia CCM. Tunamtakia kila la kheri na wana-CCM tunamhakikisha ushindi mkubwa katika uchaguzi ujao. Vile vile nampongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kuwa mgombea kiti cha Urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Sophia Simba (Mb.), na Makamu wake Mheshimiwa Haroub Masoud, Mbunge wa Koani, kwa kutuongoza vizuri na kutushauri kwa makini katika kipindi chote cha miaka mitano. Tunaishukuru Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuichambua na kujadili kwa kina bajeti yetu ya mwaka 2005/2006 kabla ya kuiwasilishwa hapa Bungeni. Ushauri uliotolewa na Kamati hiyo umesaidia sana kuboresha bajeti hii. Tunaishukuru sana Kamati hii kwa kuiwezesha Wizara kuongezewa kiwango cha fedha ya bajeti. Haya ni matokeo ya jitihada na mchango wa mawazo na maelekezo yao.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuungana na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi na pole kutokana na vifo vya wabunge wenzetu kadhaa vilivyotokea katika kipindi kifupi kilichopita. Wabunge hao ni: Hayati Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Hayati Mheshimiwa Theodos James Kasapira (Mb.), aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Hayati Mheshimiwa Frank Michael Mussati (Mb.), aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki, Hayati Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria (Mb.), aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo, Hayati Mheshimiwa Abubakar Towegale Kiwanga (Mb.), aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na Hayati Mheshimiwa Margaret Bwana (Mb.), aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hawa mahali pema peponi. Amin. Aidha, natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliopatwa na misiba, waliouguliwa au waliopata matatizo mengine ya kijamii. Naomba Mwenyezi Mungu awape tahfifu. (*Amin*)

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kutoa maelezo ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu katika muktadha wa dhamana ya Wizara yangu, na baadaye kufanya mapitio ya utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2004/05, na makusudio ya utekelezaji katika kipindi cha mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, Wizara yangu imepata mafanikio makubwa chini ya uongozi wa Jemedari wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Mafanikio haya yanatokana na Ilani ya Uchaguzi za miaka ya 1995 na 2000, na utekelezaji wa Sera sahihi za Serikali ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya Serikali ya Awamu ya Tatu kuwa madarakani mwaka 1995, Wizara yangu ilikuwa na Sera moja ya Wanawake katika Maendeleo iliyopitishwa mwaka 1992. Katika kipindi cha Awamu ya Tatu, Wizara imefanikiwa kuandaa Sera nne ambazo ni:- Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996), Sera ya Maendeleo ya Mtoto (1996), na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) iliyochukua nafasi ya Sera ya Wanawake katika Maendeleo na hivi sasa Wizara imekamilisha maandalizi ya rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Familia (2005).

Mheshimiwa Spika, maudhui ya Sera ya Maendeleo ya Jamii ni ushiriki wa watu katika kuibua, kupanga, kutekeleza na kufanya tathmini ya mipango yao ya maendeleo. Aidha, Sera inasisitiza umuhimu wa kuwawezesha wananchi kupata maarifa na stadi mbali mbali zitakazowawezesha kushiriki kikamilifu katika kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi ili kuongeza tija na kujilettea maendeleo yao. Hali kadhalika Sera inatoa kipaumbele kwenye matumizi ya mbinu shirikishi na teknolojia sahihi kwa madhumuni ya kupunguza mzigo wa kazi, hasa kwa wanawake, na kuongeza tija kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, madhumuni makuu ya Sera ya Maendeleo ya Jamii ni kuwawezesha wananchi mmoja mmoja, katika familia, vikundi au jumuiya kuchangia zaidi katika azma ya Serikali ya kuleta maendeleo kwa njia ya kujitegemea kuanzia ngazi ya kijiji na mkoa, hatimaye Taifa kwa ujumla. Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii umeleta ongezeko la ushiriki wa wananchi katika kufanya maandalizi ya miradi na programu mbalimbali na kuzitekeleza. Kutokana na ushiriki wao, wananchi sasa wamejihusisha kikamilifu katika mchakato wa maendeleo, wanamiliki miradi inayotekelze na hivyo kuifanya kuwa endelevu. Hii imejidhihirisha katika utekelezaji wa programu na miradi ya sekta mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, programu zilizotekelze wa mafanikio ni pamoja na Mpango wa Afya kupitia Maji na Usafi wa Mazingira (*HESAWA*), Mpango wa Uhai, Ulinzi na Maendeleo ya Mtoto, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), miradi ya maji vijijini, ujenzi wa nyumba bora na utayarishaji wa programu za mafunzo na elimu ya Mipango Shirikishi jamii. Kutokana na mafanikio hayo Serikali za Mitaa zimeamua kutumia mbinu shirikishi katika kuandaa na kutekeleza mipango yote ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005, Wizara yangu imedurusu na kuongeza mitaala ya mafunzo yatolewayo katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na vya Maendeleo ya Wananchi ili kukidhi mahitaji ya soko na changamoto mbali mbali za maendeleo. Aidha Wizara imeendelea kuboresha majengo na miundo mbinu katika vyuo hivyo ili kuimarisha mazingira ya kujifunzia. Katika jitihada hizo, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kimepatiwa chanzo cha maji cha kuaminika zaidi.

Mheshimiwa Spika, ndani ya kipindi hiki, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya aina mbili katika vyuo vyake vya maendeleo ya jamii. Aina ya kwanza ni Vyuo vinavyotoa mafunzo ya Cheti na Stashahada ya Juu katika fani ya Maendeleo ya Jamii, na aina ya pili ni vile vinavyotoa mafunzo ya Maarifa na Stadi mbali mbali za kuwawezesha wananchi kujitegemea. Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kinatoa Stashahada za Juu katika fani za Maendeleo ya Jamii, Upangaji na Utekelezaji wa Mipango Shirikishi na Jinsia na Maendeleo. Chuo hicho kimesajili wanafunzi 228 mwaka 2003/2004 ikilinganishwa na wanafunzi 53 mwaka 1995/1996.

Vyuo vinavyotoa mafunzo ngazi ya Cheti ambavyo ni Buhare, Missungwi na Rungemba vimeweza kusajili wanafunzi 209 mwaka 2003/2004 ikilinganishwa na wanafunzi 71 mwaka 1995/96. Aidha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 58 vimeendelea kutoa mafunzo ya Maarifa na Stadi mbali mbali na viliweza kuwapatia mafunzo wananchi 23,086 mwaka 2003/2004 ikilinganishwa na wananchi 3,942 mwaka 1995/1996. Ongezeko hili linatokana na ari ya wananchi, hususan wanaoishi karibu na maeneo ya vyuo hivi, kutaka kupata elimu na ufahamu zaidi wa masuala ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeandaa na kuzindua Mkakati wa Kuwakinga Wanawake na Watoto Dhidi ya UKIMWI na Magonjwa ya Zinaa. Mkakati huo, unatekeleza na wataalam katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika Sekretarieti za Mikoa na katika Halmashauri kwa kushirikisha wananchi. Mkakati huu umeongeza uelewa wa masuala ya UKIMWI katika jamii, na hasa namna ya kuwakinga wanawake na watoto dhidi ya maambukizi. Aidha, Wizara imeunda kamati ya UKIMWI na kutoa mafunzo yanayohusu UKIMWI kwa watumishi 477 kutoka makao makuu ya Wizara na vyuo vya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000, ina madhumuni ya kutoa miongozo mbali mbali itakayohakikisha kuwa Sheria, Sera, Mikakati na Mipango ya maendeleo yote hapa nchini inazingatia usawa wa jinsia. Katika kutekeleza hilo, Wizara yangu ilianzisha Dawati la Jinsia (*Gender Desk*) katika kila Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri ili kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia siyo tu yanazingatiwa bali matokeo ya kuleta usawa yanapatikana.

Aidha Watendaji wa Dawati hilo wamepewa mafunzo ya mbinu na stadi za kuzingatia jinsia katika utayarishaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa sera, programu na miradi pamoja na Sera za kijumla kama vile Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Spika, katika kuwawezesha na kuwaimarisha wanawake kiuchumi, Wizara yangu imewezesha utoaji wa kutoa mikopo kwa makundi mbali mbali ya wanawake. Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, Wizara ilianzisha Mifuko miwili ijulikanayo kama Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (*WDF*) na Mtaji wa Uzalishaji Mali kwa Wanawake (*CREW-T*) kwa ajili ya kutoa mikopo nafuu na wanawake wengi wamejitokeza kuchukua mikopo hii. Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake umeweza kuwapatia mikopo wanawake 28,302 mwaka 2003, ikilinganishwa na wanawake 757 mwaka 1996/1997, hili ni ongezeko kubwa. Aidha mtaji wa WDF ulioanza na shilingi 241,400,000 mwaka 1996 ulifikia shilingi 1,499,925,000 mwaka 2004/05.

Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, kumewahamasisha wanawake wengi kujiunga katika vikundi vyta uzalishaji mali, ambavyo vimeongezeka kutoka 1,207 mwaka 2000 hadi kufikia 4,940 mwaka 2004. Vile vile wanawake wengi wamejiunga na Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa na *SACAS*. Aidha, mtaji wa Uzalishaji Mali kwa Wanawake Tanzania umewakopesha wanawake 6,002 mwaka 2003 ikilinganishwa na wanawake 1,551 waliokopeshwa katika kipindi cha mwaka 1995. Wizara pia kwa kushirikiana na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote na wadau wengine umewawezesha jumla ya wanawake 1,422 kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam. Mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa wanawake waliojishughulisha kiuchumi ni pamoja na kupata masoko, kuongeza ubora wa bidhaa zao na kupunguza umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, ili ziwape wanawake uwezo wa kisheria katika kupata na kutetea haki zao, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba pamoja na wadau wengine, ilibainisha sheria zilizoonekana kuwanyima wanawake na watoto haki, usawa na maendeleo kwa lengo la kuzifanya marekebisho. Sheria ya Makosa ya Kujamii ya mwaka 1998 imewawezesha wanawake kutumia sheria hiyo kudai haki zao na kujitokeza kutoa taarifa kwenye vyombo vyta dola mara wanapofanyiwa ukatili dhidi yao. Aidha baadhi ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake kwa mfano mauaji ya wanawake wazee yamepungua kutoka 371 mwaka 2000 kufikia 304 mwaka 2003. Marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi za Vijiji ya mwaka 1999 yamewawezesha wanawake kupata haki sawa katika milki na matumizi ya ardhi na kupata fursa za kiuchumi. Aidha sheria hizi zimeiwezesha jamii kuwa na mtazamo wa kuheshimu utu na haki za wanawake. Hivi sasa Serikali inaendelea na juhudzi zake za kupitia sheria mbalimbali kwa lengo la kuziboresha.

Mheshimiwa Spika, ingawaje kumekuwepo na mafanikio katika maeneo mbali mbali, bado kuna changamoto kubwa zinazotokana na kujikita kwa mfumo dume katika jamii unaosababisha jitihada za kuleta usawa wa jinsia zisifanikiwe. Kwa mfano kuwepo kwa mfumo dume katika baadhi ya mila na desturi kunadhoofisha haki za wanawake na watoto. Mfumo dume katika upatikanaji wa elimu, ajira, kupandishwa vyeo na katika kupunguza wafanyakazi, umeathiri ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi. Wanawake wengi wamejikuta wakikatishwa tamaa katika jitihada zao za kujikombua kutokana na athari za mfumo dume. Hili ni eneo mojawapo ambalo Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa aliagiza lifanyiwe kazi, akiwahutubia wanawake wapatao 10,000 walioandamana wakati wa kuadhimisha Miaka Kumi ya Azimio na Ulingo wa Beijing huko Dar es Salaam, Machi 8 mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha ushiriki wa wanawake katika vikao vya maamuzi na utendaji, idadi ya wanawake katika masuala ya siasa na katika ngazi za kutoa maamuzi imeongezeka. Uwakilishi wa wanawake Bungeni umeongezeka kutoka asilimia 17.5 mwaka 1995 hadi kufikia asilimia 22.5 mwaka 2004. Vile vile hadi mwaka 2004 uwakilishi katika Mabaraza ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji umefikia asilimia 33.0 kutoka asilimia 25 mwaka 1995 na idadi ya Mawaziri Wanawake imeongezeka kutoka asilimia 11.1 mwaka 1995 hadi kufikia asilimia 14.8 mwaka 2004. Katika ngazi ya utendaji idadi ya Makatibu Wakuu imeongezeka kutoka mmoja mwaka 1995 hadi kufikia saba mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matukio ya kimataifa, maadhisho ya miaka kumi ya Azimio na Ulingo wa Beijing ya mwaka 2005 yalifanyika kwa kishindo kikubwa ndani na nje ya nchi. Hapa Tanzania, maadhisho haya yalikuwa na umuhimu wa pekee, kwani yalitumika kufanya mapitio ya utekelezaji wa miaka kumi wa Azimio na Ulingo wa Beijing na tathmini ya utendaji wa Serikali ya Awamu ya Tatu katika kipindi cha miaka kumi. Aidha, wanawake wa Dar es Salaam walitumia fursa hiyo kumshukuru Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa jitihada zake za kuleta usawa wa jinsia katika kipindi chote cha uongozi wake kilichokwenda sambamba na miaka kumi ya utekelezaji wa Azimio hili. Nachukua nafasi hii kama Waziri mwenye dhamana ya Maendeleo ya Wanawake hapa nchini, kwa niaba ya wanawake wote wa Tanzania, kutoa shukrani za pekee kupitia Bunge lako tukufu kwa Mheshimiwa Rais. Jitihada zake za kuhakikisha kuwa kiwango cha usawa wa jinsia kimepanda katika maeneo yote ya kisiasa na kuitendaji katika kipindi chake zimeweka msingi mzuri kwa hatua zaidi kupigwa katika awamu ya nne ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhamasishaji uliofanyika wakati wa maandalizi na maadhisho ya miaka kumi ya Azimio na Ulingo wa Beijing, wadau mbali mbali walijitokeza kushirikiana na Serikali katika kushughulikia masuala ya wanawake. Chama cha Madaktari Wanawake (MEWATA) kiliendesha zoezi la kupima matiti ambapo jumla ya wanawake 7,259 walijitokeza na kati yao 757 walikutwa na uvimbe. Kati ya wale waliokutwa na uvimbe, 34 waligundulika kuwa na saratani ya matiti na hivi sasa wanapata matibabu zaidi. Shughuli nyingine katika maadhisho hayo ilikuwa ya kuwashaa mishumaa kama ishara ya kuwakumbuka wanawake walioathirika au kufa kutokana na UKIMWI. Shughuli hii iliongozwa na Chama cha Wanawake wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (*NETWORK*).

Vile vile yalifanyika maonesho ya biashara ya bidhaa zinazozalishwa na wanawake, makongamano mbali mbali yaliyoendeshwa na Wizara, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za elimu ya juu. Chama cha Wataalam wa Kilimo Wanawake kilisambaza mbegu za mihogo na kutoa elimu ya upandaji wa mbegu hizi kwa Wanawake wa Halmashauri ya Mkuranga. Hatimaye maandalamano ya wanawake yalifanyika siku ya kilele tarehe 8 Machi, 2005 na kupokewa na Mheshimiwa Rais. Nachukua nafasi hii kupitia Bunge lako tukufu kuwashukuru wale wote walioshirikiana nasi katika kufanikisha maadhisho haya. Kwa namna ya pekee nawashukuru sana wenyeji wa sherehe hizi kitaifa Mheshimiwa Luteni (Mstaifu) Yusuf Makamba na

viongozi wenzake wa Mkoa wa Dar Es Salaam na wananchi wote kwa mchango wao mkubwa katika maadhimisho hayo. Aidha naishukuru mikoa yote kwa kuadhimisha siku hii.

Mheshimiwa Spika, kimataifa maadhimisho haya yalifanyika tarehe 8 Mwezi Machi, 2005 huko New York Marekani wakati wa kikao cha Kamisheni ya Hali ya wanawake. Kikao hiki kilikuwa na ajenda moja kuu ya kutathmini utekelezaji wa Ulingo na Azimio la Beijing katika ngazi ya kimataifa na kupendekeza mipango ya baadaye ili kuleta usawa, amani na maendeleo. Tathmini hiyo imeonyesha kuwa bado kuna vikwazo vingi vya kimaendeleo kwa wanawake katika nchi nyingi. Kutokana na hali hii kikao kiliazimia kwamba utekelezaji wa Ulingo wa Beijing uendelee kwa kasi kubwa zaidi, na ufanyike kwa kuzingatia Mkataba wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (*CEDAW*), Malengo ya Maendeleo ya Millenia na Mipango inayohusu kupunguza maambukizi ya UKIMWI, hasa kwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, jitihada zinazofanywa za kuingiza masuala ya jinsia katika shughuli mbali mbali zimefanya harakati za kuleta uwiano wa kijinsia na masuala yanayohusu wanawake na jinsia kuwa ajenda muhimu katika mikutano ya kitaifa na kimataifa, Tanzania ikiwa mstari wa mbele. Mfano mzuri ni Mkutano wa Kimataifa wa Wakuu wa Nchi za Maziwa Makuu kuhusu Amani, Usalama, Demokrasia na Maendeleo uliyofanyika hapa nchini mwezi Novemba, 2004.

Katika kikao hicho Tanzania iliwezesha masuala ya jinsia kuingizwa katika Tamko la Dar es Salaam lililotolewa na Wakuu wa Nchi hizi. Tamko hilo lilizingatia Azimio la Umoja wa Mataifa Namba 1325 linalozitaka nchi za Umoja wa Mataifa kuendeleza amani na utulivu kwa kukomesha migogoro na vita kati ya nchi na nchi na katika familia. Kipengele muhimu cha Azimio hili ni ushiriki wa wanawake katika kusuluuhisha na kukomesha migogoro na vita. Sambamba na kikao hicho, Wake wa Marais wa Nchi za Maziwa Makuu walikutana na kubainisha nafasi zao katika kuleta amani na maendeleo. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mama Anna Mkapa kwa kuwa mwenyeji wa kikao hicho ambacho kiliwezesha Wake wa Marais kushiriki katika mchakato wa kuleta amani ndani ya nchi za Maziwa Makuu. Vile vile walipata nafasi ya kubadilishana usoefu katika kutekeleza miradi yenyе lengo la kuinua hali za wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kuratibu Mfuko wa Mafunzo kwa Wanawake Tanzania (*TFTW*) uliotekeliza kuanzia mwaka 1989 hadi 2003 kwa ushirikiano na Serikali ya Canada. Madhumuni ya Mfuko huo yalikuwa ni kuinua viwango vya elimu kwa wanawake ili waweze kuongeza uwezo wao na kushiriki katika siasa na vyombo vya kutoa maamuzi katika ngazi mbali mbali. Katika kipindi hicho Mfuko uliwasomesha jumla ya wanawake 2,076, kati ya hao, 309 katika masomo ya muda mrefu, 1,750 mafunzo ya muda mfupi, na 17 mafunzo ya kushikizwa.

Mheshimiwa Spika, kutafsiriwa kwa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 katika Kiswahili chepesi kumeongeza ufahamu na uelewa wa idadi kubwa ya jamii kuhusu masuala mbali mbali ya wanawake na jinsia kiuchumi, kijamii na

kisiasa. Aidha Wizara iliandaa Mpango wa Kitaifa kuhusu Kutokomeza Aina Zote za Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto na kuusambaza kwa wadau. Mpango huo unaendelea kutekelezwa ambapo jamii sasa imehamasika na kutoa taarifa za matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwenye vyombo vya sheria. Vile vile Tanzania imeridhia Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (*Optional Protocol to CEDAW*). Itifaki hii inatoa fursa kwa wanawake kutoa malalamiko yao moja kwa moja kwenye Kamati ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (*CEDAW*).

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 1996 inatoa dira kuhusu uhai, ulinzi na maendeleo ya mtoto. Aidha Sera inalenga kuwashirikisha watoto katika ujenzi wa Taifa pamoja na kuwakinga dhidi ya maradhi mbali mbali. Katika kutekeleza mpango wa uhai, ulinzi na maendeleo ya mtoto, jamii imehamasika na kuweza kujitokeza katika kuwapeleka watoto wao kliniki kupata chanjo za msingi. Chanjo hizo ni Polio, Surua, Pepopunda, *DPT/HB* na Kifua Kikuu. Aidha kumekuwa na ongezeko la watoto waliopata chanjo kwa ajili ya kinga ya magonjwa mbali mbali kwa kipindi cha mwaka 1995 – mwaka 2003 kama ifuatavyo:-

- (i) Polio kutoka asilimia 79 mwaka 1995 hadi asilimia 92 mwaka 2003;
- (ii) Surua kutoka asilimia 76 mwaka 1995 hadi asilimia 90 mwaka 2003;
- (iii) *DPT/HB* kutoka asilimia 82 mwaka 1995 hadi asilimia 88.5 mwaka 2003;
- (iv) Kifua Kikuu kutoka asilimia 88 mwaka 1995 hadi asilimia 94.5 mwaka 2003; na
- (v) Pepopunda kutoka asilimia 30 mwaka 1995 hadi asilimia 83 mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 1995 – 2004 Serikali iliridhia na kutekeleza Mikataba na Itifaki zifuatazo za kimataifa kuhusu Maendeleo ya Watoto:-

- (i) Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto;
- (ii) Itifaki za nyongeza ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto kuhusu Biashara ya Kuza Watoto na Upigaji Picha za Udhailishaji watoto.
- (iii) Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto kuhusu ushirikishwaji wa Watoto kwenye migogoro ya Kivita.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na hatua hii ni pamoja na kuweka mazingira mazuri kitaifa ya utoaji wa haki za watoto na kuhakikisha ustawi wao. Kwa kuridhia mikataba na Itifaki hizi Tanzania imeungana na nchi nyingine za Umoja wa Mataifa katika jitihada za kuwapatia watoto haki zao.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita haki za watoto zimefahamika zaidi kwa jamii na watoto wenyewe. Aidha vyombo vifuatavyo vimeanzishwa ili kuwashirikisha zaidi watoto katika kufanya maamuzi yanayogusa haki na maslahi yao:-

- (i) Mtandao wa Harakati za Watoto Tanzania (*Tanzania Movement for and with Children – TMC*) uliozinduliwa tarehe 28 Aprili, 2001.
- (ii) Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania Desemba, 2002.

Aidha mtandao wa Tanzania wa Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Utotoni (*Tanzania Early Childhood Development Network*) umeundwa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa watoto wadogo wanapata msingi mzuri wa malezi bora. Vile vile tawi la Tanzania la mtandao wa kutokomeza ukeketaji la Kanda ya Afrika Mashariki limeanzishwa ili kuimarisha mapambano dhidi ya mila zinazoleta madhara kwa watoto hususani ukeketaji. Taarifa tulizonazo ni kwamba ngariba wengi wameanza kuachana na mila hii yenye madhara.

Mheshimiwa Spika, katika kipinndi hicho Serikali ilianzisha Idara ya Maendeleo ya Mtoto katika Wizara kwa lengo la kutekeleza kikamilifu Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mtoto. Kuundwa kwa Idara hii kumeweza masuala yanayohusu maendeleo na ustawi wa mtoto kuangaliwa kwa umakini zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine ilifanya mapendekezo ya kurekebisha sheria mbali mbali zinazohusu haki za mtoto na kuweza kuingiza masuala ya watoto kwenye mwongozo wa MKUKUTA na maandalizi ya bajeti ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuzingatia misingi ya utawala bora katika uendeshaji na utoaji huduma zake kwa walengwa. Mpango Mkakati ulioandaliwa na Wizara yangu unahakikisha ubora wa huduma zinazotolewa na Wizara kwa kuzingatia nafasi na rasilimali zilizoainishwa. Aidha, watumishi wakiwemo viongozi wa ngazi za juu walipewa mafunzo kwa nia ya kuimarisha utawala na kuziba mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 1995 na 2005 Wizara yangu imewawezesha watumishi 398 kwa kuwapatia mafunzo ya kimenejimenti na kitaaluma. Kati ya watumishi hawa 31 wamepata stashahada ya uzamili na wawili wamepata udaktari wa falsafa. Aidha Maafisa Maendeleo ya Jamii 205 na waalimu 898 walipandishwa vyeo kwa utaratibu wa mserereko. Katika kipindi hicho Wizara ilipata nafasi 414 za ajira mpya. Hatua hizo zimewezesha Wizara yangu kujaza nafasi zilizokuwa wazi na pia kuimarisha utendaji kazi ndani ya Wizara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa maelezo ya mapitio ya utekelezaji wa Bajeti na mpango wa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieza Bunge lako tukufu kwamba Wizara yangu ingetathmini utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996 ili kubaini mafanikio na upungufu. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa tathmini hiyo imefanyika katika Mikoa ya Iringa, Kigoma, Manyara, Mwanza, Morogoro na Ruvuma. Masuala muhimu yaliyojitekeza kutokana na tathmini hiyo ni pamoja na yafuatayo:-

- (i) Dhana ya ushiriki wa wananchi na matumizi ya mbinu shirikishi (participatory approaches) katika shughuli za kujiletea maendeleo yao, ambayo ndiyo msingi wa Sera ya Maendeleo ya Jamii, imeeleweka vema zaidi kwa wananchi. Matokeo yake ni utekelezaji mzuri ambao umeleta mafanikio makubwa katika miradi ya maendeleo hasa katika ngazi ya kijiji. Hii inajidhihirisha katika utekelezaji wa programu na miradi mbali mbali kama *TASAF*, *MMEM*, *HESAWA*, miradi ya maji vijijini na ujenzi wa nyumba bora;
- (ii) Maudhui na maelekezo ya sera hii yameweza kutafsiriwa na wadau mbali mbali ili yaendane na hali halisi ya eneo ambako inatekelezwa. Hii inazingatia ukweli kuwa jamii hazifanani na wala haziishi katika maeneo ambayo yana fursa na vikwazo vyta maendeleo vinavyofanana. Matokeo ya tafsiri hizi yanaonekana katika tofauti ya mbinu shirikishi zinazotumika katika kila eneo;
- (iii) Upo upungufu mkubwa kwa watumishi wa Maendeleo ya Jamii hususan katika ngazi za kata na vijiji. Pamoja na Sera kuhimiza kila kata na kijiji kiwe na Afisa Maendeleo ya Jamii, waliopo sasa hivi wanakidhi asilimia 40 tu ya mahitaji. Kwa sababu hiyo Wizara inaendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya Cheti na kuhimiza Halmashauri ziwaajiri ili kukidhi mahitaji.
- (iv) Sera na mipango ya kisekta imezingatiwa vizuri na wananchi ambao wamevezeshwa kuimiliki na kuidumisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na. 7 wa mwaka 2002, Maafisa Maendeleo ya Jamii Wasaidizi wanaajiriwa katika ngazi ya kata na vijiji. Ili kufanikisha utekelezaji wa Waraka huu Vyuo vyta Maendeleo ya Jamii vyta Rungemba, Buhare na Missungwi viliendelea kufanyiwa ukarabati wa majengo na miundombinu ili kuvizeshesha kutoa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Cheti kwa waombaji wengi zaidi. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 idadi ya wanachuo waliosajiliwa katika vyuo hivi ilikuwa 454. Kati yao wanawake walikuwa 315 sawa na asilimia 69.4 na wanaume 139 ambayo ni asilimia 30.6. Hili ni ongezeko la asilimia 65.6 ikilinganishwa na idadi ya wanachuo 298 waliosajiliwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kutoa mafunzo ya taaluma katika ngazi ya Stashahada za juu, katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru. Katika mwaka wa fedha 2004/2005. Jumla ya wanachuo 513 walipata mafunzo, kati yao wanawake ni 278 ambao ni sawa na asilimia 54.2 na wanaume ni 235 ikiwa ni sawa na asilimia 45.8. Idadi ya wanachuo imeongezeka kwa asilimia 31.5 ikilinganishwa na waliopatiwa mafunzo mwaka 2003/04. Vile vile Chuo kimeboreshwa kwa kufanya ukarabati wa mabweni, vyoo, mfumo wa maji na kimenunua vitanda, viti na magodoro.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieza Bunge lako tukufu kwamba Wizara yangu, inaendelea kuratibu shughuli za Vikosi vyta Ujenzi na programu ya Mafunzo ya Ufundis Vijijini ili visaidie jitihada za Serikali na za wananchi katika utekelezaji wa miradi ya kujitegemea inayohitaji ufundi. Nafurahi kuliarifu Bunge hili kuwa Wizara yangu kwa ushirikiano mzuri na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imewezesha Vikosi hivyo

kubaki katika Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri ili kutoa nafasi kwa Wizara yangu kuwawezesha mafundi hawa. Katika kipindi cha 2004/05 jumla ya mafundi 40 kutoka Halmashauri 20 za Dodoma Mjini, Hai, Ifakara, Kilosa, Kondoa, Kongwa, Mahenge, Mbinga, Mjini, Morogoro Mjini, Morogoro vijijini, Moshi Mjini, Moshi Vijijini, Mpwapwa, Mwanga, Namtumbo, Rombo, Same, Songea Mjini, Songea Vijijini na Tunduru walipatiwa mafunzo kazini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara yangu iliedelea na utekelezaji wa Mpango wa kutoa elimu, ujuzi na stadi mbali mbali za maendeleo katika vyuo 58 vya Maendeleo ya Wananchi. Jumla ya wananchi 24,658 wakiwemo wanawake 13,085 na wanaume 11,573 walipatiwa mafunzo, ikilinganishwa na wananchi 23,086 waliopatiwa mafunzo mwaka 2003/04. Hili ni ongezeko la asilimia 6.8. Mafunzo haya yalijumuisha ufugaji bora, ushonaji, useremala, ujasiriamali, hifadhi ya mazingira, mbinu za kudhibiti maambukizi ya virusi vya UKIMWI pamoja na nyinginezo za kuwawezesha wananchi kufanya kazi zao kwa ufanisi, kujiajiri na kujitegemea kama mkakati muhimu wa kuwawezesha kujipunguzia umaskini. Aidha, kutokana na ushirikiano mzuri na Halmashauri, vyuo hivi sasa vimeanza kuwa vitovu vya maendeleo katika maeneo yanayovizunguka. Nachukua nafasi hii kuzishukuru sana Bodi za Vyuo zinazoongozwa na Wakurugenzi wa Halmashauri, na kutambua mchango muhimu kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge amba ni wajumbe. Kutokana na umakini wao, Bodi hizi zimeweza kubuni mbinu mbali mbali za kujiimarisha Vyuo hivi, ikiwa ni pamoja na kuboresha majengo, miundombinu na kuvipatia kazi mbali mbali za Halmashauri. Hatua hizi zimeviwezesha vyuo kujitegemea kwa kiwango kikubwa na kujiimarisha kimafunzo na kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/05 Wizara yangu ilianza kufanya ukarabati mkubwa wa majengo na miundombinu katika vyuo sita (6) vya Maendeleo ya Wananchi kwa utaratibu wa Chuo kimoja kila Kanda. Ukarabati huu ulifanyika katika Vyuo vya Gera (Kagera), Kisarawe (Pwani), Mbinga (Ruvuma), Msinga (Kilimanjaro), Ruaha (Iringa) na Urambo (Tabora). Aidha, vyuo vinane (8) vilifanyiwa ukarabati mdogo wa majengo na miundombinu. Vyuo hivyo ni Chala (Rukwa), Katumba (Mbeya), Kilosa (Morogoro), Kiwanda (Tanga), Mabughai (Tanga), Monduli (Arusha), Munguri (Dodoma) na Same (Kilimanjaro). Jithada hizi za Wizara yangu zinadhahirisha azma ya Serikali ya kujiimarisha vyuo hivi kama chachu ya maendeleo. Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika maeneo ya vyuo hivi tayari wameanza kuona matokeo ya kazi zilizofanyika. Kwa kuwa majengo na miundombinu muhimu ya vyuo hivyo imekarabatiwa, hivi sasa wananchi wengi wamevutiwa na mazingira mazuri yaliyopo na wameanza kujiunga na vyuo hivyo kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza matatizo ya uvamizi wa maeneo ya vyuo na kuondoa migogoro ya ardhi inayovikabili, Wizara yangu ilipima maeneo ya vyuo kumi na moja (11) vya Bigwa (Morogoro), Handeni (Tanga), Kilwa Masoko (Lindi), Kiwanda (Tanga), Mabughai (Tanga), Malampaka (Shinyanga), Mbinga (Ruvuma), Munguri (Dodoma), Mwanva (Shinyanga), Same (Kilimanjaro) na Sengerema (Mwanza) ili viweze kupatiwa hati miliki. Mafanikio haya yametokana na ushirikiano mkubwa uliopo

kati ya Wizara yangu na Halmashauri za Wilaya. Ni matumaini yangu kuwa vyuo hivi vitapata hati miliki hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, takwimu za watu katika jamii nyingi zinaonyesha kuwa idadi ya wanawake ni kubwa kuliko ya wanaume, na ndio wenye jukumu kubwa la uzazi na kulea familia. Kutokana na ukweli huu, kuna kila haja kwa jamii kuwa na sera na mipango mahsusini ya kuwawezesha wanawake kutekeleza majukumu yao ya msingi katika nyanja mbali mbali za kiuchumi na kijamii ili kuhakikisha kuwa wanapata fursa za kimaendeleo na hali zao za maisha zinaboreshwani.

Mheshimiwa Spika, katika utayarishaji wa MKUKUTA, Wizara yangu iliteua Kamati maalumu ambayo ilipewa jukumu la kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanafafanuliwa wazi na kuingizwa katika Mkakati huo. Vile vile Wizara iliendesha mkutano wa wanawake wadau mwezi Februari, 2005 Dar es Salaam ambao pia ulihakikisha kuwa masuala ya jinsia yamezingatiwa katika MKUKUTA. Hata hivyo wadau hao walitoa angalizo kuwa haitoshi kuzingatia tu masuala ya jinsia katika MKUKUTA bali muhimu zaidi uwekwe katika utekelezaji wa maeneo hayo ili kuleta maendeleo ya wanawake na usawa wa jinsia unaokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa Dawati la Jinsia katika miundo ya Wizara, Mikoa na Halmashauri na Idara zinazojitegemea umeanza kuleta matokeo mazuri kwa kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanazingatiwa na kutekelezwa kama sehemu muhimu ya mchakato wa kuleta usawa wa jinsia na maendeleo. Ili kuboresha utendaji kazi wa Dawati la Jinsia, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilitoa mafunzo kwa baadhi ya Watendaji wa Dawati la Jinsia kuhusu namna ya kutathmini utekelezaji wa Ulingo wa Beijing na Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (*CEDAW*).

Matokeo ya mafunzo haya yaliwezesha Dawati hizi kutoa mchango mkubwa katika kuandaa taarifa ya miaka kumi ya utekelezaji wa Ulingo wa Beijing na taarifa ya tano ya nchi kuhusu *CEDAW*. Ili kupanua zaidi uelewa na ufahamu wa masuala hayo, Wizara iliwezesha ushiriki wa Watendaji wa Dawati la Jinsia katika mikutano ya kikanda na ya kimataifa. Kwa utaratibu huu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Ikulu zilishiriki katika kikao cha 49 cha Kamisheni ya Hali ya Wanawake kilichofanyika New York, Marekani mwezi Machi, 2005.

Aidha, baadhi ya Wizara zimeunda kamati za masuala ya jinsia ndani ya Wizara zao. Kamati hizo zimeweza watumishi wa Wizara kufahamu zaidi dhana ya usawa wa jinsia na kuweza kuandaa na kutekeleza mipango inayozingatia jinsia. Huu ni mwitikio mzuri wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu Maazimio mbali mbali ya kitaifa na kimataifa yanahimiza ushiriki wa wanawake katika vikao vya maamuzi ya kisiasa na vya utendaji katika ngazi zote za maamuzi. Kwa mfano, lengo la Umoja wa Afrika ni kufikia

uwakilishi wa asilimia 50 na la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) ni asilimia 30 hadi mwaka 2005. Mwaka huu, Bunge lako tukufu lilipitisha mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ambapo idadi ya viti maalum vya wanawake Bungeni inatarajiwa kufikia asilimia 30 mwishoni mwa mwaka huu.

Kwa viti vya kuteuliwa na Rais uwiano utafikia kiwango cha Umoja wa Afrika cha asilimia 50 yaani, wanawake watano na wanaume watano. Mafanikio haya siyo madogo kwa kuwa yamedhihirisha wazi azma ya Serikali ya awamu ya Tatu chini ya uongozi wa Rais Benjamin William Mkapa, ya kuleta usawa wa jinsia katika vikao vya maamuzi. Aidha mwaka jana nilitoa rai kwa Wizara zote, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya kuhusu utekelezaji wa Azimio la *SADC* linalohusu Jinsia na Maendeleo ambalo pamoja na mambo mengine, linahimiza ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi usiwe chini ya asilimia 30. Rai hiyo ilizingatia kupitishwa kwa Sheria ya Utumishi wa Umma namba 8 ya mwaka 2002 iliyokasimia mamlaka ya ajira kwa Watendaji Wakuu na hivyo kutoa fursa kwa Kamati za Ajira kuzingatia uwiano mzuri wa jinsia katika kutoa ajira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 Wizara yangu iliahidi kufuatilia uanzishaji wa Chombo kitakachowaunganisha wanawake bila kujali itikadi za kisiasa na tofauti nyinginezo kama ilivyoainishwa katika Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba Mwezi Oktoba, 2004 Baraza la Mawaziri lilielekeza kwamba uanzishaji wa Chombo usubiri matokeo ya shauri la Baraza la Wanawake Tanzania (BAWATA) lililopo mahakamani. Aidha agizo lilitolewa la kuhakikisha kuwa Wizara iimarishwe.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeshirikiana na Asasi zisizo za Kiserikali (*AZISE*) na wanaharakati mbali mbali wanaoshughulikia masuala ya jinsia katika kuandaa taarifa ya tano ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake. Taarifa hii itawasilishwa katika Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia masuala ya Maendeleo ya

- (i) Utekelezaji wa *CEDAW* umezingatia misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, maazimio ya kikanda, sera za jumla na za kisekta. Kutokana na hali hii imekuwa rahisi kwa wadau mbali mbali kuzingatia utekelezaji wa Mkataba huu katika mipango yao;
- (ii) Jitihada zinazofanywa na wanaharakati wa masuala ya jinsia za kupiga vita ubaguzi dhidi ya wanawake zimeifanya jamii kuwa na uelewa mkubwa kuhusu masuala hayo na kushiriki kikamilifu katika kuleta usawa wa jinsia. Aidha jitihada hizo zimeonyesha haja ya kuwa na ushirikiano baina ya Serikali na wadau mbali mbali ili kuleta maendeleo stahimilivu yanayozingatia usawa wa jinsia katika jamii;
- (iii) Sheria mbali mbali zilizotungwa na kudurusiwu katika kipindi cha miaka kumi ya Beijing zimezingatia utekelezaji wa Mkataba huu kwa misingi ya kuweka sheria

- zinazotetea usawa wa jinsia kwa kuondoa vipengele vinavyoashiria ubaguzi, unyanyasaji na ukatili dhidi ya wanawake;
- (iv) Jitihada zimefanywa na Serikali, *AZISE* mbali mbali na Mabenki za kuwezesha wanawake kiuchumi ili waweze kuinua hali zao za maisha na kupunguza umaskini wa kipato unaowafanya washindwe kushiriki kikamilifu katika jitihada za kujenga uchumi;
 - (v) Wananchi kwa ujumla wamekuwa na mwamko na uelewa mkubwa kuhusu ubaguzi wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake na wamekuwa wakichukua hatua pale tabia za namna hiyo zinapojitokeza katika jamii;
 - (vi) Ukatili dhidi ya wanawake katika ngazi ya kaya hususan kupiga wanawake na mauaji ya wanawake wazee yamepungua;
 - (vii) Mila zenye madhara kama vile ukeketaji, kuoza watoto wa kike mapema na tabia nyingine zimeanza kupungua.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana niliahidi kuandaa na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Azimio na Ulingo wa Beijing kwa kipindi cha 1995 – 2005. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa taarifa hiyo iliandaliwa na kuzinduliwa rasmi na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya miaka kumi ya Azimio na Ulingo wa Beijing tarehe 2 Machi, 2005. Taarifa hiyo pamoja na kipeperushi ambacho kimeeleza kwa lugha ya Kiswahili utekelezaji huo, vimetawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge. Katika utekelezaji wa Azimio na Ulingo huu uliokuwa na maeneo 12, Tanzania ilitoa kipaumbele kwa maeneo manne makuu ambayo ni:- kuwawezesha wanawake kiuchumi na kuondoa umaskini; kuwapa wanawake haki na kuwaongezea uwezo kisheria; kuwapatia wanawake elimu, mafunzo na ajira; na kuwawezesha wanawake kushiriki katika ngazi za maamuzi. Katika maeneo yote haya kumekuwa na mafanikio makubwa na bado jitihada zinaendelea kufanywa na Wizara nyingine za kisekta.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la kuwawezesha wanawake kujikwamua kiuchumi, Wizara yangu iliendelea na jitihada zake za kuratibu shughuli za utoaji wa mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (WDF). Aidha Wizara yangu ilitoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri 75 kuhusu mbinu na stadi za kuwashamasisha wanawake kuijunga na Vyama vya Kuweka na Kukopa (*SACCOS*). Vyama hivyo vinatarajiwा kwa kiasi kikubwa kuwawezesha wanawake kujivekea akiba na kupata huduma za kifedha.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 Wizara yangu iliendelea kushirikiana na Asasi mbalimbali Zisizo za Serikali (*AZISE*) kuwawezesha wanawake kushiriki katika maonesho ya biashara ndani na nje ya nchi ili kuboresha bidhaa zao na kutafuta masoko. *AZISE* hizi ni pamoja na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote unaoendeshwa chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Mama Anna Mkapa na Shirikisho la Vyama Vya Wanawake Wafanyabiashara (*FAWETA*). Katika ushirikiano huu wanawake 130 waliwezesha

kushiriki katika maonesho ya 28 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar Es Salaam mwaka 2004. Vile vile wanawake 254 wakiwakilisha vikundi 135 walishiriki maonesho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika mwezi Machi 2005 jijini Dar es Salaam. Aidha wanawake 6 walishiriki katika maonesho ya kimataifa huko Botswana na mmoja aliweza kwenda Marekani kutafuta soko la bidhaa anazozalisha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mama Anna Mkapa, Mwenyekiti wa Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote, kwa kuwa mstari wa mbele katika kutekeleza Ulingo na Azimio la Beijing. Mheshimiwa Mama Mkapa kwa kipindi chote cha miaka kumi alipania kuhakikisha kuwa Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote unachangia kuwaimarisha wanawake kiuchumi, kuongeza kipato na hivyo kukidhi mahitaji yao ya msingi. Ninamtakia heri katika maisha yake ya baadaye na ninaahidi kuwa Wizara yangu itaendelea kushirikiana naye kikamilifu katika mipango yote yenye lengo la kuleta maendeleo ya wanawake na usawa wa jinsia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalo jukumu la kuhakikisha kuwepo kwa mazingira mazuri yanayowafanya watoto kukua na kupata ustawi kulingana na malezi bora ya familia na jamii. Katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Wizara yangu iliendelea na jitihada za kuratibu utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto inayotekelizwa na wadau mbali mbali. Vile vile Wizara imeendelea kuelimisha jamii kupitia kaulimbiu mbali mbali za maadhimisho kama vile siku ya Mtoto wa Afrika, Siku ya Familia Duniani, Siku ya Unyonyeshaji Duniani, Siku ya UKIMWI Duniani, Siku ya Kudhibiti Ukeketaji Duniani na Siku ya kukomesha utumikishwaji wa watoto Duniani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kama Mratibu wa Mtandao wa watoto chini ya miaka minane (*Tanzania Early Childhood Development Network*), kwa kushirikiana na wadau wengine, imefanya uchunguzi wa awali wa hali halisi ya watoto. Uchunguzi huu unaonyesha kuwa watoto walio katika umri wa awali wanakabiliwa na matatizo mengi ambayo ni pamoja na maambukizi ya UKIMWI, kubakwa, kutupwa, kutelekezwa na kukosa malezi mazuri na lishe bora. Kutokana na kutambua tatizo hili Tanzania iliungana na nchi nyiningine nne za Afrika kuandaa mpango maalum wa kuwasaidia watoto walio chini ya umri wa miaka minane walioathiriwa au kuathirika na virusi vya UKIMWI na UKIMWI. Nchi hizo ni Ghana, Malawi, Namibia na Zambia. Aidha, Tanzania ilihudhuria mukutano wa tatu wa Kimataifa Barani Afrika kuhusu Maendeleo na Makuzi ya Awali ya Utotoni uliofanyika Ghana mwezi Juni, 2005. Katika mukutano yote hiyo iliazimiwa kuwa masuala ya maendeleo na makuzi ya awali ya utotoni yapewe kipaumbele katika maeneo yanayolenga kuimarisha maisha ya watoto, hususani wale walio katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, utumikishwaji wa watoto bado unaendelea kuwa tatizo la kijamii. Ili kulitafutia ufumbuzi tatizo hili, Wizara yangu inashirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) katika kuratibu utekelezaji wa Programu ya Taifa ya muda maalum ya kukomesha Utumikishwaji wa Watoto katika kazi za hatari. Aidha katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilikamilisha mradi wa kuingiza masuala haya katika mitaala ya Mafunzo ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Lengo ni kuhakikisha kuwa

wahitimu wa vyuo hivi wanakuwa na mbinu na stadi za kuihamasisha jamii kupambana na utumikishwaji wa watoto.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mkataba wa Haki za Mtoto unaendelea kwa kushirikiana na wadau zikiwemo sekta za Serikali na AZISE mbali mbali kama KULEANA, KIWOHED, Kituo cha Watoto Wadogo, *Plan (T)* na *Save the Children*, zinazoshughulikia masuala ya watoto. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba taarifa ya utekelezaji ya Tanzania imetayarishwa na kupelekwa kwenye Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Mtoto.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2004/05 nililiarifu Bunge lako tukufu kwamba ziko mila na desturi zinazoleta madhara kwa jamii na hasa wanawake na watoto ambazo zinahitaji kutokomezwa, mojawapo ikiwa ni ya ukeketaji. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kupitia mikutano ya Mtandao wa Kutokomeza Ukeketaji, katika Kanda ya Afrika Mashariki Tawi la Tanzania na wanaharakati mbalimbali, Wizara imeboresha mbinu za kuondokana na mila hii zikiwemo kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya ukeketaji na kuwapa ngariba mafunzo ya kuwawezesha kufanya shughuli nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya jitihada hizi ni kupungua kwa kiwango cha ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike hapa nchini. Utafiti uliofanywa mwaka 2003/2004 na Mtandao wa Kupambana na Ukeketaji (*Anti-Female Genital Mutilation - AFNET*) unaonyesha kuwa katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Manyara, Morogoro na Singida, ngariba 2026 walitangaza hadharani kuacha kazi ya ukeketaji. Wizara yangu inafuatilia kwa karibu matokeo haya ili yawe ya kudumu. Wizara yangu kama Mwenyekiti wa Mtandao wa Kudhibiti Ukeketaji Kanda ya Afrika Mashariki Tawi la Tanzania inaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji hapa nchini kwa kushirikiana na asasi zisizo za serikali. Nachukua nafasi hii kuzipongeza asasi hizo kwa jitihada wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala na Utumishi ina jukumu la kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma mahala pa kazi unaimarishwa. Jukumu hili linatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya mwaka 2002, Sheria ya Fedha Namba 6 ya mwaka 2001 na Sheria ya Ununuzi Namba 4 ya mwaka 2001. Kupitia sheria hizi mwaka 2004/2005 Kamati ya Ajira ya Wizara iliweza kuajiri watumishi 72, kutangaza tenda 3 na kusimamia kazi na manunuzi mbali mbali. Aidha, Wizara ilipata shs. 164,000,000 za ununuzi wa vifaa vya ofisi kutoka Mfuko wa Kuongeza Ufanisi unaosimamiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa idadi ya kutosha ya watumishi wenye sifa na uwezo unaotakiwa ni suala muhimu katika kufikia malengo ya Mpango Mkakati wa Wizara (*Strategic Plan*). Katika kipindi hicho watumishi 56 wa Wizara yangu walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa lengo la kukidhi mahitaji ya kazi na matakwa ya miundo yao ya utumishi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 iliendelea kuwaelimisha watumishi wake juu ya mapambano dhidi ya rushwa kupitia vikao mbali mbali nya kazi. Wananchi nao wameelimishwa kupitia maadhisho mbali mbali ya kitaifa yanayoratibiwa na Wizara hii. Aidha, mpango wa utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa wa mwaka 2002 ni mionganoni mwa maeneo yaliyo katika MKUKUTA ambayo utekelezaji wake unaanza katika mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na UKIMWI mahali pa kazi, Wizara iliendelea kutoa elimu kuhusiana na masuala ya UKIMWI. Jumla ya watumishi 48 walipatiwa mafunzo hayo katika warsha iliyofanyika Mkoani Morogoro tarehe 17 hadi 21 Februari, 2005, na watumishi 250 katika warsha iliyofanyika Iringa kuanzia tarehe 30 Mei, 2005 hadi 03 Juni, 2005.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara yangu iliendelea kutekeleza programu ya kuboresha Utumishi wa Umma kwa kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma za usafi wa ofisi na mazingira na ulinzi na usalama kwenye ofisi za Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2004/2005, niliahidi kuwa Wizara ingeimarisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ya Umma kwa kununua vifaa mbali mbali pamoja na kuongeza wataalam. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba kupitia Mfuko wa Kuongeza Ufanisi (*Performance Improvement Fund*), Kitengo kimetengewa fedha zitakazotumika kununulia vifaa nya kisasa. Lengo ni kuhakikisha kuwa majukumu ya Kitengo hiki yanatekelezwa ikiwa ni pamoja na utoaji wa habari zinazohusu utekelezaji wa Sera za Wizara kwa umma. Aidha watumishi wa Kitengo hiki wamekwisha ajiriwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu iliandaa mpango wa mwaka mmoja (*Interim Plan*) ili kutoa nafasi ya kukamilisha taratibu za kupata ufadhilli wa pamoja wa wahisani. Taratibu hizi zimekamilika na utayarishaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitatu umeanza.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanza maandalizi ya uwekaji wa kumbukumbu zinazohusu wanawake katika kompyuta (*Women's Database*). Hatua zifuatazo zimefikiwa katika kutekeleza mradi huu:-

- (i) Fomu za kukusanya kumbukumbu zinazohusu wanawake zimeandaliwa na kujaribiwa kwa baadhi ya watumishi wa Wizara;
- (ii) Mfumo wa kompyuta wa kuhifadhi kumbukumbu hizo umebuniwa na kujaribiwa kwa mafanikio; na
- (iii) Fomu za kukusanya kumbukumbu hizo zimeanza kusambazwa katika taasisi mbali mbali ili waajiriwa wanawake wazijaze na kuzirudisha Wizarani.

Kumbukumbu hizo zitaisaidia Serikali kufahamu wasifu wa wanawake waliopo katika maeneo mbali mbali ya utumishi na kuzifanya kazi, ikiwa ni pamoja na kupendeleza majina ya wanawake wenye sifa za kushika nafasi za uongozi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo wa ufuutiliaji na tathmini unaozingatia jinsia (*Computerized Gender Sensitive Monitoring and Evaluation system*), takwimu kutoka kwenye Wizara, Idara za Serikali, Halmashauri za Miji, Manispaa na wilaya zimeanza kukusanywa. Kazi hii imeshaanza kufanyika katika Wizara yangu, na inaendelea kufanyika katika Wizara na Taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini hiyo, sasa naomba kutoa taarifa ya mipango na malengo ya Wizara yangu kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) umeleta mabadiliko makubwa katika mgawanyo wa majukumu na kufanya kila sekta ihusike moja kwa moja katika utekelezaji wa malengo makuu ya MKUKUTA yafuatayo:-

- (i) Kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato;
- (ii) Kuimarisha hali za maisha; na
- (iii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.

Malengo haya yamenyumbuliwa kwa kuzingatia mchango wa kila sekta ambapo Wizara yangu ina jukumu la kutekeleza malengo 34 yanayohusu masuala ya maendeleo ya jamii, maendeleo ya wanawake, jinsia na watoto.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa bila ushiriki wa jamii katika kutekeleza MKUKUTA malengo yaliyowekwa hayataweza kufikiwa na kudumishwa. Kutokana na ukweli huu, Wizara yangu itaendelea na jukumu lake la kuhakikisha kuwa wananchi wanahamasishwa ili wajitokeze kushiriki kikamilifu katika kutekeleza MKUKUTA. Ili kufikia lengo hili Wizara itaendelea kutoa wataalam wa maendeleo ya jamii, kuhamasisha jamii kushiriki katika kutekeleza MKUKUTA. Aidha, kwa Chuo cha Tengeru, Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira kwa kujenga ukumbi wa mihadhara, kuweka intaneti, huduma ya usafiri na kuunda Bodi ya Uendeshaji itakayosimamia Chuo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya wananchi, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo ya ndani na nje katika vyuo 58 vya maendeleo ya wananchi ili kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi. Jumla ya wananchi 25,000 wanatarajiwa kupata mafunzo mwaka huu. Mafunzo na stadi mbali mbali zitakazotolewa Vyoni na nje ya Vyuo zitawawezesha wananchi kujitegemea na kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na tija zaidi. Mafunzo hayo yatatolewa kwa kuzingatia maeneo yafuatayo ya MKUKUTA:-

- (i) Kuwezesha mafunzo ya stadi za maisha na ujasiriamali kwa ajili ya wananchi vijijini hususan wanawake na vijana;

- (ii) Kuongeza mafunzo ya stadi za kisomo chenye manufaa kwa wanawake na wanaume watu wazima ili kuwawezesha kufanya shughuli mpya kwa kadri umri unavyoongezeka;
- (iii) Kuelimisha jamii kuhusu haki za msingi za mtoto, pamoja na mapambano dhidi ya ajira mbaya, kuandaa na kutekeleza mipango inayolenga kuondoa ajira kwa watoto;
- (iv) Kuinua matumizi ya habari, mawasiliano na teknolojia katika Taasisi za Serikali na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;
- (v) Kuweka misingi imara inayolenga watu wenyе ulemavu, watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, wagonjwa, wazee pamoja na watoto, kupata huduma za jamii, misaada, mikopo na misamaha ya uchangiaji gharama mbali mbali vyuoni na katika sekta mbali mbali zinazotoa huduma;
- (vi) Kuwawezesha watoto wa kike wanaokatisha masomo kutokana na kupata mimba kumaliza masomo yao au kuwapatia stadi za ufundi; na
- (vii) Kusaidia kaya zilizoathiriwa na UKIMWI ambazo zinaongozwa na vijana wa kike, watoto na wazee kwa kuwawezesha kupata huduma za kijamii, zikiwemo misamaha katika uchangiaji gharama za huduma mbali mbali, utunzaji wa wagonjwa nyumbani na utoaji wa mafunzo ya stadi.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya maeneo haya, Wizara yangu inakusudia kukamilisha ukarabati mkubwa wa majengo na miundombinu ulioanza mwaka jana. Aidha, Wizara inakusudia kuweka mitambo ya umeme inayotumia nguvu ya jua kwenye vyuo vinane (8) ambavyo havijafikiwa na umeme wa gridi. Vile vile, Wizara itawezesha upimaji wa maeneo ya Vyuo vinane (8) vya Maendeleo ya Wananchi ili kuvipatia hati miliki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/06, Wizara yangu inakusudia kufuatilia hali ya Majumba ya Maendeleo (*Community Centres*) yaliyokuwa yanasi mamiwa na Mabibi na Mabwana Maendeleo yaliyojengwa zamani, kwa madhumuni ya kuyafufua ili kuwawezesha wananchi kupata habari kuhusu maendeleo kubadilishana uzoefu kutoka ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara inakusudia kuyapatia majumba hayo vifaa na nyenzo muhimu kama majorida, luninga, kanda na kompyuta zitakazowawezesha wananchi kupata na kupashana habari za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa ushiriki wa jamii katika jitihada mbali mbali za hifadhi ya mazingira. Kwa kuanzia, Wizara yangu itashirikiana na mikoa ya Iringa na Mbeya kuhamasisha wananchi kushiriki katika kampeni dhidi ya uharibifu wa mazingira katika maeneo ambayo ni vyanzo vya mto Ruaha. Maeneo haya yamepewa kipaumbele kwa kuwa sehemu kubwa ya umeme wa

gridi nchini huzalishwa katika mabwawa ya Kidatu na Mtera ambayo yote yamejengwa katika mto huo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna ongezeko la wasichana na wavulana wanaoishi katika mazingira magumu, wengi wao wakiwa wameshindwa kumaliza elimu ya msingi au ya sekondari. Katika kuchangia kupunguza ukubwa wa tatizo hili, Wizara yangu itawahamasisha na kuwawezesha wanafunzi katika mikoa saba waliokatisha masomo kushiriki katika shughuli zitakazowaongezea kipato. Aidha, Wizara itatoa fursa maalumu za mafunzo ya stadi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa watoto yatima na walio katika mazingira magumu na hatimaye kuwapatia vifaa vitakavyowawezesha kujaajiri baada ya kufuzu mafunzo hayo. Hii itakuwa hatua maalumu (*Affirmative Action*) kwa walengwa hawa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa inapata majanga mbali mbali kama vile mafuriko, njaa na magonjwa ya milipuko. Wananchi wengi wanashindwa kukabiliana nayo ipasavyo kutokana na ukosefu wa mbinu shirikishi za kuwawezesha kumudu hali inayotokana na maafa hayo. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara yangu itatoa elimu kwa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri kuhusu mbinu shirikishi za kukabiliana na maafa. Mbinu hizo zitawawezesha wananchi kushiriki katika kukabiliana na maafa pindi yanapotokea na kumudu matokeo ya maafa hayo.

Mheshimiwa Spika, UKIMWI umesababisha familia nyingi kuongozwa na wanawake, vijana, watoto au wazee wenye uwezo mdogo wa kujitunza wao wenyewe na familia zao. Ili kuchangia ufumbuzi wa tatizo hili, Wizara yangu itatoa mafunzo kwa wataalamu wa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ili waweze kuandaa mipango ya kupambana na UKIMWI kwa kushirikiana na jamii katika ngazi ya kijiji. Aidha, wataalam watatumika katika kubaini wajibu na majukumu ya wadau mbali mbali katika kutekeleza mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia MKUKUTA, Wizara yangu itawawezesha kinyenzo baadhi ya Maafisa wa Maendeleo ya Jamii kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Kwa mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaanza kwa kuwapatia pikipiki moja moja Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri 20. Hali kadhalika Wizara itawapa mafunzo ya kuongeza elimu ili waweze kukidhi matakwa ya miundo yao mipy ya utumishi kama sheria ya Utumishi wa Umma inavyoelekeza. Aidha, uwezo wa wakufunzi wa vyuo utaboreshwaa kwa kuwapa mafunzo kazini, mafunzo ya kompyuta na ya menejimenti.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza MKUKUTA, Wizara yangu itaandaa mwongozo utakaohakikisha kuwa maeneo yanayohusu jinsia yanatekelezwa kikamilifu. Mafunzo ya matumizi ya mwongozo huo yatatolewa kwa watendaji mia moja (100) wa Dawati la jinsia, katika ngazi za Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri na sekta nyingine. Aidha, mwongozo huo utakuwa ni sehemu ya mfumo mzima wa kitaifa wa ufuutiliaji wa utekelezaji wa MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza jitihada za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake Wizara yangu katika mwaka 2005/2006 itachapisha nakala 2,000 za Mpango wa Taifa wa kuondoa aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na kuzisambaza. Vile vile, Maafisa Maendeleo ya Jamii na Wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na vya Maendeleo ya Jamii wataelimishwa kuhusu mpango huu ili waweze kuanza kutoa elimu kuhusu athari za ukatili dhidi ya wanawake na jinsi ya kuutokomeza kwa jamii inayozunguka Vyuo hivyo. Pamoja na hatua hii, Wizara itaendesha mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii 114 ili wapate mbinu na stadi za kutoa ushauri nasaha kwa waliodhurika na vitendo vya ukatili. Aidha, jitihada zitafanywa kuwaelekeza na kuwawezesha wanawake kupata msaada wa kisheria pale inapobidi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, sheria kadhaa hapa nchini zimerekebishwa au kupitishwa kwa lengo la kuleta haki na usawa wa jinsia. Sheria hizi ni pamoja na Sheria ya Makosa ya Kujamiihana ya mwaka 1998, Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999. Kwa kuwa wananchi wengi hawayafahamu maudhui ya sheria hizi, Wizara yangu itaandaa majarida na vipeperushi kwa lugha nyepesi kwa ajili ya kuelimisha jamii kuhusu mabadiliko hayo yenye lengo la kutoa haki kwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuiwakilisha nchi katika mikutano ya kikanda na kimataifa inayohusu maendeleo ya wanawake na jinsia, kama ile ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi Kusini mwa Afrika (*SADC*), Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (*EAC*), Kamisheni ya Hali ya Wanawake (*CSW*), Nchi za Maziwa Makuu, Kamisheni ya Uchumi ya Afrika (*ECA*) na Jumuiya ya Madola (*Commonwealth*) kwa madhumuni ya kuweka mikakati ya pamoja na kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa maazimio mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza umaskini wa kipato na kuwzesha Wanawake kiuchumi, na kama ilivyoelekezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu utekelezaji wa mpango wa kupanua huduma za fedha vijijini, Wizara yangu itaendelea kuwzesha wanawake kuijunga na Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa (*SACCOS*) na vile visivyo vya Ushirika (*SACAS*). Aidha, mafunzo ya mbinu na stadi za kuhamasisha wanawake yatatolewa kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri. Pamoja na hatua hizi, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Ndogo Ndogo Tanzania (*MKURABITA*) unategemewa kuwawezesha wanawake kutumia mali zilizorasimishwa kama dhamana ya mikopo kutoka Benki mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa mwaka 2005/2006 itaendelea kuratibu, kusimamia na kufuutilia uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya jamii ambao katika semina ya mikakati ya kuboresha Mfuko huu waliweza kutoa mapendekezo ya kuuiamarisha. Mapendekezo yao yatazingatiwa. Ni lengo la Wizara yangu kufanya tathmini ya kina kuhusu uendeshaji wa Mfuko huu, hasa kwa kutia maanani tatizo kubwa la marejesho. Tathmini hiyo italenga kutumia Mfuko huu kuziimarisha *SACCOS* na *SACAS* na hatimaye kuwzesha kuundwa kwa Benki Kata.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha jitihada zilizopo za kuwawezesha wanawake wajasiriamali kupata masoko ya ndani na nje, Wizara yangu katika mwaka 2005/2006 itaendelea kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na mashirika mengine kuwawezesha wanawake kushiriki katika maonyesho ya kimataifa ya ndani na ya nje ya nchi ili kupanua wigo wa masoko ya bidhaa zao. Msisitizo utakuwa katika kuboresha na kunakshi bidhaa zao. Aidha, Wizara yangu itaendelea na jukumu la kuratibu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa madhumuni ya kuongeza ufahamu wa jamii kuhusu umuhimu wa usawa wa jinsia katika kuleta maendeleo stahimilivu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalo jukumu la kutathmini utekelezaji wa programu na miradi mbali mbali ya maendeleo ili kuona ni kwa jinsi gani inazingatia masuala ya jinsia. Ufuatiliaji na ukusanyaji wa takwimu za jinsia utafanywa kwa kutumia miongozo iliyotolewa na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia; Mkakati wa Maendeleo ya Jinsia na MKUKUTA.

Katika mwaka wa fedha 2005/06, Wizara itaanza kukusanya takwimu kutoka sekta sita za kijamii kwa kutumia maafisa wa Dawati la Jinsia. Matokeo ya zoezi hili yatawekwa katika mfumo wa Wizara unaochanganua takwimu kijinsia (*Gender Disaggregated Data*).

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na *TACAIDS* umeonyesha kuwa kasi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa Watanzania ni asilimia 7. Hata hivyo wanawake wako katika kasi kubwa zaidi ya kuambukizwa ya asilimia 7.7, ikilinganishwa na wanaume ambao wapo kwenye kasi ya asilimia 6.3. Msemo kuwa UKIMWI umechukua sura ya mwanamke unatokana na takwimu hizi, na jukumu kubwa walilonalo la kulea wagonjwa na yatima. Kwa kuititia MKUKUTA, Wizara yangu itashirikiana na *TACAIDS* kuihamasisha jamii hususan wanaume ili washiriki kikamilifu katika kuchukua hatua za pamoja za kushughulikia masuala ya kijinsia yanayosababisha kasi ya maambukizi kuongezeka kwa wanawake na wasichana. Aidha Wizara yangu itabainisha mahitaji ya kijamii na kuwaelekeza kwenda kwenye asasi mbali mbali zinazotoa misaada ikiwa ni pamoja na kuvitungia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kupata mafunzo kuhusu mbinu na stadi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kusambaza Sera ya Maendeleo ya Mtoto hasa kwa watoto ambao ni wadau wakubwa, ili waielewe Sera hiyo. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara yangu itakamilisha zoezi la kuiweka Sera hiyo katika lugha nyepesi kabla ya kuisambaza kwa wadau mbali mbali kwa kuwa jukumu la kulea watoto ni letu sote.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2004/2005, nililieza Bunge lako tukufu kuhusu umuhimu wa kuelimisha jamii ili kuongeza uelewa wao wa Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia (*Population and Family Life Education - POFLEP*). Kwa kuzingatia hali hiyo, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka huu, itadurusu mtaala wa mafunzo katika ngazi ya jamii na itaendelea na hatua ya kutoa elimu kuhusu Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya majukumu yaliyotolewa kwa Wizara yangu kupitia MKUKUTA, ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa makubaliano yaliyomo katika mikataba ya kimataifa kuhusu haki na ustawi wa mtoto.

Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau, inatarajia kutayarisha taarifa ya kwanza ya utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto na kuiwasilisha Umoja wa Afrika Addis Ababa, Ethiopia. Aidha Wizara yangu kwa kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi itaelimisha jamii inayozunguka Vyuo hivyo kuhusu haki za msingi za mtoto, zikiwemo haki ya kuendelezwa, kulindwa na kutotumikishwa katika kazi za hatari.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara yangu itatoa elimu ya malezi na maendeleo ya awali ya mtoto kwa jamii zinazozunguka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya Ilula, Mamtukuna, Nzovwe na Ulembwe. Aidha, Wizara yangu itaviwezesha Vyuo hivyo kuendelea kutoa mafunzo ya majoribio (*pilot*) kwa ajili ya kuratibu utekelezaji wa programu inayohusu wasichana waliokatisha masomo yao, kama wale waliojifungua katika umri mdogo.

Eneo jingine ni kufanya utafiti ili kuweza kushughulikia matatizo ya watoto wanaozaliwa magerezani au wanaolazimika kuandamana na mama zao magerezani. Mwaka huu, Wizara yangu itaziwezesha jamii zilizoathirika zaidi na ongezeko la watoto yatima kutayarisha mipango shirkishi jamii itakayobaini maeneo mbali mbali ya kufanyiwa kazi, na wajibu wa makundi yanayowasaidia watoto yatima na walio katika mazingira magumu.

Mikoa itakayohusika na zoezi hili kwa mwaka huu ni Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Ruvuma na Singida. Mipango hii itaziwezesha jamii kufahamu fursa zilizopo katika jamii za kuwawezesha kupambana na tatizo hili. Aidha nafasi ya wadau mbali mbali na Serikali katika kutekeleza mipango hii zitafahamika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara yangu itatayarisha programu ya kupunguza utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari. Hivyo Wizara yangu inakusudia kufanya utafiti wa awali kuhusu usafirishaji wa watoto ndani na nje ya nchi (*human trafficking*). Vile vile, Wizara itaendesha zoezi la kuelimisha jamii dhidi ya utumikishwaji wa watoto kwa kutumia vyombo vya habari kama radio, magazeti na televisheni kwa kushirikiana na wanaharakati katika mikoa ya Singida na Iringa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Wizara yangu itatekeleza lengo la MKUKUTA la kutayarisha mpango wa kitaifa wa elimu ya malezi ya watoto wadogo chini ya umri wa miaka mitano kwa kushirikiana na wadau mbali mbali. Madhumuni ya hatua hii ni kuimarisha malezi na makuzi ya watoto wachanga na wadogo nchini. Aidha Wizara yangu itakusanya na kusambaza zana za ushawishi jamii kuhusu ubora wa maziwa ya mama na hatari za ulikizaji pale mtoto anapoacha kunyonya ziwa la mama.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Wizara yangu itabaini matatizo yanayozikabili kaya zinazoongozwa na watoto yatima na walioathirika kwa UKIMWI katika maeneo yanayozunguka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Matokeo ya utafiti huo yataziwezesha jamii kuandaa mipango shirikishi jamii ya kuwasaidia watoto hawa.

Mheshimiwa Spika, ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu itaendelea na majukumu ya kuajiri, kuwezesha utendaji kazi katika idara mbali mbali, kutoa mafunzo ya kimenejimenti na taaluma, kuendeleza utawala bora, kupambana na rushwa pamoja na kukabiliana na janga la UKIMWI mahala pa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu itazindua na kuanza rasmi utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Mkataba huu unaainisha viwango vya huduma ambavyo umma unavitarajia na umeweka miundo ya ufuatiliaji na utatuzi wa matatizo pale yanapojitokeza. Aidha, watumishi wote wa Wizara yangu watakamilisha zoezi la kutathmini Mpango Mkakati wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliwaagiza waajiri kuwaendeleza watumishi wote ambao hawana sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo yao ya utumishi ili kuhakikisha wanapata sifa hizo katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai, 2004. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea kuwaimarisha watumishi ili wafanye kazi zao kwa ustadi na maarifa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoleza katika mapitio ya utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara kwa mwaka 2004/2005, Wizara yangu inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi ikilinganishwa na wingi wa majukumu yanayopaswa kutekelezwa hasa katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu inatarajia kuajiri watumishi wapya 50 kama tulivyoidhinishiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa mwongozo kuhusu masuala ya ajira katika Utumishi wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu itaboresha utendaji wa Kamati ya Ajira ya Wizara ili iweze kuutumia kikamilifu mwongozo wa ajira unaosisitiza ushindani na kuhakikisha kuwa wote wanaoajiriwa katika Utumishi wa Umma wana taaluma, ujuzi na sifa zinazotakiwa.

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya rushwa yamepewa msukumo mpya kwa kuingizwa kwenye maeneo muhimu yanayotarajiwu kutekelezwa chini ya MKUKUTA.

Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa watumishi na kusambaza miongozo ya maadili, sheria, kanuni na taratibu zinazohusu mapambano dhidi ya rushwa sambamba na utoaji mafunzo kwa watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa UKIMWI sehemu za kazi una lengo la kuhakikisha kuwa watumishi wana afya njema inayowawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kutimiza lengo hili Wizara yangu imeunda Kamati ambapo katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara itawawezesha wafanyakazi kubaini masuala yanayochochea maambukizi ya UKIMWI. Utambuzi huu utasaidia kuwaelimisha wafanyakazi na kuwatia hamasa wabadili tabia. Kuhusu watumishi walioathirika, Wizara itaendelea kutoa baadhi ya misaada kama vile dawa na ushauri nasaha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu itaendelea kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji kati yake, Wizara na taasisi mbali mbali pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali amba ni wadau wetu kwa kupitia Mkutano Mkuu wa Mwaka. Vile vile tutaendelea na mikutano miwili kwa mwaka ya Mashirikiano kati ya Wizara yangu na Wizara ya Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Zanzibar. Aidha, mahusiano kati ya Menejimenti na watumishi yataimariswa kupitia Baraza la wafanyakazi litakalokutana mara mbili kwa mwaka. Ni jukumu la Wizara yangu kuwezesha taasisi na umma kwa ujumla kupata habari kuhusu masuala mbali mbali ya maendeleo ya jamii, jinsia na watoto kama yalivyofafanuliwa katika Sera za Wizara. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara yangu itaendelea kukitumia Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ya Umma kufanikisha azma hii. Aidha, Kituo cha Habari kuhusu wanawake kitakuwa sehemu ya kitengo hiki baada ya ufadhili wa *AIDOS* (Asasi isiyo ya kiserikali) iliyokuwa inaendesha kituo hiki kukamilisha mkataba na kukikabidhi Wizarani. Nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali ya Italia na uongozi wa *AIDOS* kwa kukifadhili na kukiendesha kituo hiki takriban kwa muda wa miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika Mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Majukumu ya Wizara kwa mwaka 2004/2005, Wizara imeanza utekelezaji wa tathmini ya utendaji kazi kwa mwaka. Utaratibu huu wa uwazi unakuwa mbadala wa taratibu nyingine zilizokuwa zikitumika katika utumishi wa umma. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara itaendelea na utaratibu huu kwa kuandaa na kuwekeana mikataba ya kazi na watumishi wake wote kwa lengo la kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma. Aidha, Wizara yangu itaendelea na utekelezaji wa programu ya kuboresha Utumishi wa Umma kwa kuishirikisha sekta binafsi katika usafi wa ofisi na mazingira yake pamoja na ulinzi wa mali za Serikali na kuendelea kuibua maeneo mengine ambayo sekta binafsi zinaweza kutoa huduma Wizarani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itafanya ukaguzi wa utekelezaji wa bajeti yake, ikiwa ni pamoja na ukaguzi katika vyuo vya Maendeleo ya Jamii na vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na shughuli mbali mbali zinazotekelzwa chini ya MKUKUTA ili kubaini maeneo yenye upungufu na kuurekebisha. Aidha Wizara itafuatilia utekelezaji wa sera

zake katika Asasi zisizo za kiserikali kwa ajili ya kutathmini mafanikio ya sera hizo na kuimarisha uhusiano na Asasi hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara itafanya utafiti kuona kama Sera zake mbali mbali zinawafikia wana-jamii, wanazielewa na kama zimeweza kubadilisha hali na mienendo ya maisha yao. Aidha Wizara itaangalia ni kwa kiwango gani jamii inaelewa Maazimio ya Beijing na Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (*CEDAW*).

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa Wizara kyangu iliandaa mnpango wa mwaka mmoja (*Interim Plan*) ili kutoa nafasi mpango wa miaka mitatu kukamilishwa. Kwa kushirikiana na m taalam, mpamngo huu wa mwaka mmoja utaendelea kutekelezwa wakati mpango wa miaka mitatu unakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la Wizara yangu ni kutayarisha sera na miongozo mbali mbali yenyе mwelekeo wa kuzihamasisha jamii kujiletea maendeleo kwa kuziwezesha kushiriki katika utekelezaji wa mikakati mbali mbali ya kukuza uchumi na hatimaye kupunguza umaskini. Majukumu haya ni mtambuka. Hivyo basi, utekelezaji wa malengo na mipango ya Wizara ya mwaka 2005/2006 bado utahitaji ushirikiano mkubwa zaidi wa wadau mbali mbali hasa Mikoa na Halmashauri. Tutaendelea kushirikiana na wadau hawa na vile vile kuziwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika maendeleo yao wenyewe na taifa zima kwa ujumla. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Shamim Parkar Khan (Mb.), Naibu Waziri, kwa ushirikiano na ushauri wake mkubwa alionipa katika kipindi chote cha uongozi wangu ndani ya Wizara hii.

Vile vile napenda kumshukuru Bibi Hilda Ausi Gondwe, Katibu Mkuu, kwa ushirikiano na msaada anaonipa katika kuimarisha misingi na mwelekeo mzuri wa Wizara yangu. Vile vile, napenda kuwashukuru Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara yangu katika ngazi zote na katika taasisi zetu zote kwa ushirikiano wao, hususan katika kutekeleza majukumu ya Wizara ambayo ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lakoTukufu. Ushirikiano wao wote hawa na michango yao imefanya uongozi wangu kuwa mwepesi na kutuwezesha kulitumikia taifa letu kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kutumia nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa washirika wa ndani ambao wameshirikiana nasi kwa namna moja au nyingine katika kutekeleza majukumu yetu. Washirika hao ni pamoja na; Mtando wa Kupambana na Ukeketaji (*AFNET*), Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*), Shirika la Mtando wa Jinsia Tanzania (*TGNP*), Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (*TAWLA*), Chama cha Wanawake Viongozi katika Kilimo na Mazingira (*TAWLAE*), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (*TAMWA*), Shirikisho la Vyama vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (*FAWETA*), *Plan International*, Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (*MEWATA*), mashirika mbali mbali pamoja na wale ambao wanafanya kazi kwa maslahi yetu kwa namna moja au nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara yangu imepata ushirikiano mzuri wa wadau mbali mbali pamoja na nchi rafiki na mashirika ya kimataifa. Napenda kuzishukuru Serikali za Canada, Ireland, Italia, Netherlands, Norway na Sweden kwa kukubali kuiwezesha Wizara hii. Aidha, nayashukuru mashirika ya kimataifa ambayo ni Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya watu (*UNFPA*), Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Maendeleo ya Wanawake (*UNIFEM*) pamoja na Mashirika mengine ya ndani na nje ya nchi ambayo tumekuwa nayo karibu katika kufuutilia utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake, kwa mwaka 2005/2006 sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Matumizi ya Shs. 8,426,084,000. Kati ya hizo Shs. 7,126,084,000 ni Matumizi ya Kawaida, ambapo Shs. 1,912,284,000 ni Mishahara (*PE*) na Sh.5,213,800,000 ni kwa Matumizi Mengineyo (*Other Charges(OC)*). Aidha, Sh. 1,300,000,000 ni kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mwisho kabisa, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba ya Wizara yangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia makadirio haya, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah. (*Makofî*)

MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH (k.n.y. MHE. SOPHIA M. SIMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII): Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2004/2005 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2005/2006

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 81 (1) Toleo la 2004, naomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2005/2006 ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukua fursa hii nimshukuru Mhesimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya Kamati kwa niaba yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu waliokuwa Waheshimiwa Wabunge ambao wamefariki dunia kwa kipindi hiki, nao ni Marehemu Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Rahaleo, Marehemu Mheshimiwa Frank Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mashariki, Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa. Vifo vyao ni msiba mkubwa kwa Bunge letu Tukufu, kwa familia zao na kwa Wananchi wa maeneo waliokuwa wakiwawakilisha. Mungu aziweke mahali pema peponi roho za marehemu. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii, nimpongeze kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira na Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, kwa kuteuliwa na Rais kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa MKURABITA. Aidha, nampongeza tena kwa kuchaguliwa na Mkutano wa SADC uliofanyika Juni, 2005 nchini Swaziland kuwa Mwenyekiti wa Wabunge Wanawake wote wa SADC. Kuteuliwa na kuchaguliwa katika nafasi hizo, kunaonesha uwezo mkubwa alionao wa kuongoza na pia ni ishara nzuri kuwa wanawake wanao uwezo wa kuongoza na kusimamia shughuli mbalimbali wakipewa nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukua fursa hii pia nimshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa maelezo yake makini aliyojatoa mbele ya Kamati yangu tarehe 26 Mei, 2005 Mjini Dar es Salaam wakati wa kuwasilisha mapendekezo ya Bajeti ya Wizara yake, kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa ushirikiano wao katika kujadili na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naomba niwatambue kwa kuwataja kama ifuatavyo: Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Omar M. Mwenda, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Ramadhan Nyonje Pandu, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Bakari M. Mbonde, Mheshimiwa Janeth E. Mashelle, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye na Mheshimiwa Kisyeri W. Chambiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilipokea maelezo ya taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2004/2005 pamoja na mapendekezo ya Bajeti ya mwaka 2005/2006 ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto tarehe 26 na 27 Mei, 2005 Jijini Dar es Salaam. Mambo yaliyojadiliwa katika taarifa hiyo ni pamoja na Dira

ya Wizara; majukumu ya Wizara; utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi cha mwaka 2004/2005; mapato na matumizi kwa kipindi cha mwaka 2004/2005; mafanikio na matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji; malengo na kazi zilizopangwa kufanywa kwa mwaka wa fedha 2005/2006 na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Kamati ilipokea maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kwa kiasi kikubwa Kamati iliridhika na utekelezaji uliofanywa na Wizara. Hata hivyo, Kamati imebaini mapungufu yafuatayo katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake:-

Moja, urejeshaji wa mikopo inayotolewa na Halmashauri na Wizara kwa Wanawake bado ni tatizo, hili linatokana na wakopaji kutopata mafunzo ya kutosha kuhusu rasilimali, akiba na mikopo na hivyo kukosa mbinu za biashara.

Pili, muundo wa Kamati za Halmashauri ambapo Mkurugenzi wa Halmashauri ndiye Mwenyekiti wa Kamati na huyo huyo ndiye mtekelezaji hautoi msukumo mkubwa katika kuhamasisha ukopaji na urejeshaji wa mikopo hiyo.

Tatu, vikundi vinavyoshindwa kurejesha mikopo havipewi adhabu, jambo ambalo linavifanya vikundi vingi kutoogopa, kwa vile vikundi vyenyewe ndivyo huji pangia adhabu.

Nne, Maafisa Maendeleo ya Jamii, wanaoendesha mikopo hawana taaluma ya akiba na mikopo hivyo kushindwa kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakopaji.

Tano, Maafisa hao hawana Miundombinu ya kuwawezesha kuwafikia walengwa mfano usafiri, hivyo ni wanawake wachache tu walio karibu na Halmashauri ndio wanaonufaika na Mfuko huo.

Sita, Mfuko huu unawafikia wanawake wachache sana kutokana na mafungu madogo yanayotolewa na Serikali Kuu na michango ya Halmashauri.

Saba, Mikopo inayotolewa ya shilingi 50,000/= hadi 100,000/= ni midogo kiasi kwamba, haichangii kukua kwa biashara na ajira. (*Makofi*)

Nane, Mfuko haumjengei mlengwa uwezo wa kujiveka akiba kwani unasisitiza mkopo na marejesho tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa kwa kipindi cha 2004/2005 na kuridhika na utekelezaji wake, Kamati inatoa ushauri ufuatao: Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Mfuko huu ni muhimu sana katika kupunguza umaskini kwa wanawake na kuwaletea maendeleo. Ili kuboresha mfuko huu, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

Moja, wanawake wanaokopa wajengewe uwezo mpana kwa kupatiwa elimu ya jamii na jinsia, stadi za kazi, ujasiliamali, akiba na mikopo, ili waweze kupata mbinu bora za kibashara.

Pili, wanavikundi wahamasishwe kuweka akiba mara kwa mara ili kuongeza uwezo wao wa kukopa. Pia wahamasishwe kujisajili kama vyama vyama akiba na mikopo.

Tatu, muundo wa Kamati za Halmashauri ambazo Wenye viti wake ni Wakurugenzi wa Halmashauri ufanyiwe marekebisho. Aidha, Wakuu wa Wilaya wawe Wajumbe katika Kamati hizo ambapo katika muundo wa sasa si Wajumbe. Hii itasaidia kuleta msukumo wa utendaji. (*Makofî*)

Nne, adhabu kwa vikundi vinavyoshindwa kurejesha mikopo ipangwe na Kamati ya Halmashauri na si vikundi kujipangia adhabu vyenyewe. Hii itasaidia wanavikundi kuwa makini katika kurejesha mikopo yao.

Tano, Maafisa Maendeleo ya Jamii, wanaoendesha mikopo wapatiwe elimu ya kutosha kuhusu akiba na mikopo, hii itasaidia maafisa hawa kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakopaji.

Sita, Maafisa Maendeleo ya Jamii wapatiwe usafiri ili waweze kuwafikia wanawake wengi zaidi hasa wa vijijini kwa ajili ya kutoa elimu juu ya mikopo na akiba, hii itasaidia wanawake wengi kutambua umuhimu wa kuchukua mikopo, kurejesha na kujiwekea akiba.

Saba, Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha kwa ajili ya Mfuko huu kwani kiasi cha fedha kinachotolewa ni kidogo na hivyo kuwanufaisha wanawake wachache tu wa mijini. Aidha, mikopo hii haichangii kukua kwa biashara na ajira hata kwa wale wanaokopa kwani viwango vyaa mikopo vinavyotolewa ni vidogo sana na haviongezeki. Mfano kwa zaidi ya miaka 10 viwango vyaa mikopo vimeduwa vikitolewa kati ya shilingi 50,000/= hadi 100,000/=. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya kuanzisha Benki ya Wanawake ni ya muda mrefu. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufikia uamuzi kuwa Benki hiyo ianzishwe sasa. Hata hivyo, Kamati inashauri Wizara ya Fedha kuharakisha katika kufanikisha uanzishaji wa Benki hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vyaa Maendeleo ya Jamii ni mkombozi wa vijana wengi wanaomaliza elimu ya msingi na kushindwa kuendelea na elimu ya juu. Kutohana na umuhimu wa vyuo hivi, Kamati inashauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, iendelee kuwa karibu na kuvifua tilia vyuo hivi ili kuhakikisha kwamba, vinatimiza malengo ya uanzishwaji wake nchini kote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia majukumu mengi ya Wizara hii, Kamati ilishauri Wizara iongezewa Bajeti. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia pendekemo hili na hivyo kuongeza Bajeti ya Wizara kutoka Shilingi 4,989,293,400/= kwa

Mwaka wa fedha 2004/2005 hadi kufikia Shilingi 8,426,084,000/= kwa Mwaka wa fedha 2005/2006. Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa majukumu ya MKUKUTA ambapo Wizara hii inatakiwa kutekeleza malengo 34, bado kiasi hiki hakitoshelezi. Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kuongeza bajeti zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2005/2006, baada ya maoni na ushauri wa Kamati, Kamati ya Maendeleo ya Jamii inayakubali mapendekezo ya Bajeti ya mapato na matumizi ya kawaida na maendeleo kwa fungu Na. 53 kama ifuatavyo:-

- Matumizi ya Kawaida	Sh. 7,126,084,000/=
- Miradi ya Maendeleo Sh.	1,300,000,000/=
Jumla	Sh. 8,426,084,000/=

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii tena nikushukuru wewe, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Napenda nimshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Mheshimiwa Shamim Khan, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Hilda Ausi Gondwe, pamoja na Maafisa wa Wizara wote, kwa ushirikiano wao katika kutoa maelezo ya ufanuzi wa Bajeti yao mbele ya Kamati pale walipohitajika kufanya hivyo. (*Makofit*)

Napenda niwashukuru tena Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa ushirikiano wao katika kuichambua Bajeti ya Wizara na kutoa maoni yao. Shukrani za pekee zimwendee Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kwa kuendesha vikao vya Kamati pale alipohitajika kufanya hivyo. Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Bwana Damian Foka, kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake bila kukwama. Mwisho, napenda kumshukuru Katibu wetu wa Kamati, Bibi Angelina Langisi Sanga, kwa kuihudumia Kamati na kutoa ushauri wa kitaalam pale alipohitajika kufanya hivyo ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa hii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, shukrani zangu ni kwa Waheshimiwa Wabunge wote, ninawashukuru kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na ninaomba kuwasilisha. (*Makofit*)

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii, nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa mwaka wa fedha wa 2005/2006, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 43(5) (b) na (c), toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba nitoe pole na salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Namwomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho za Marehemu hawa mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sote tunavyoolewa, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, inashughulikia masuala ya jamii na jinsia, kwani imetamkwa wazi wazi, hivyo, Wizara si ya wanawake tu ni yetu sote, kwani jamii ni wanawake, wanaume, watoto, wazee, vijana, walemavu, wakulima, wafanyakazi, wagonjwa na kadharika. Kwa msingi huo, naendelea kusisitiza ushauri wangu kwamba, ili kuonesha mfano thabiti kwa vitendo, Wizara hii iongozwe na jinsia zote, hasa katika ngazi za juu kwa Mfano, Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, ngazi hizi ziwe na wanawake na wanaume, angalau mwanaume mmoja kwa wanawake watatu (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imekumbatia sehemu muhimu ya jamii ya Watanzania, kwa msisitizo zaidi, Wanawake na Watoto. Wanawake ni zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania wote na wengi ni wakulima wa jembe la mkono huko vijijini. Wizara hii ndiyo inayoongoza na kuratibu harakati za kuwakomboa wanawake. Ni jambo la kushangaza kuona Wizara hii imetengewa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 1.3 tu kwa shughuli zake za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuleta maendeleo halisi ya wanawake, watoto na jamii kwa ujumla, Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba, Wizara hii iongezewe Bajeti yake ili iweze kutekeleza shughuli zake kikamilifu, vinginevyo tutakuwa tunatwanga maji ndani ya kinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*), vinaendelea kuwa na nafasi muhimu katika kuchochea maendeleo ya jamii. Vyuo hivi bado vinakabiliwa na matatizo mengi kwa miaka kadhaa sasa. Uchakavu wa majengo na vifaa duni vya kufundishia na kujifunzia ni kati ya matatizo sugu yanayovikabili vyuo hivyo. Kwa historia kidogo ni kwamba mwaka 1975/76, *Folk Development Centres (FDCs)*, vilikuwepo vyuo 47 na lengo lilikuwa ni kuwa na chuo kimoja kila Wilaya kwa Tanzania nzima. Madhumuni yake yalikuwa ni mazuri sana katika kubadili mtazamo wa Wananchi na kuleta maendeleo ya Wananchi waishio vijijini. Kwa miaka ya hivi karibuni ambapo Serikali inajitahidi kuondoa umaskini kwa mipango yake kadha wa kadha, vyuo hivyo ni muhimu sana kwa mikakati hiyo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iandae Mkakati Maalum wa kuimarisha eneo zima la vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Vyuo hivi ambavyo vipo jirani sana na Wananchi wa kawaada na hasa wale wa vijijini, ndio vitakuwa kichocheo muhimu katika harakati za kupunguza au kuondoa kabisa umaskini kwa kuhakikisha Sera na Mipango ya Serikali kiutendaji inawafikia walengwa, tofauti na ilivyo sasa. Aidha, tunaitaka Serikali kama inavyoimarisha eneo la shule za msingi na sekondari, kuititia mipango ya MMEM na MMES, basi ibuni pia mpango wa kuziendeleza na kuziimarisha *FDCs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado upo umuhimu wa Wizara hii kuhamasisha na kuratibu uanzishwaji wa benki maalum ambayo itasaidia sana kuchangamsha maendeleo ya kiuchumi ya wanawake na pia Watanzania wengine. Maendeleo ya kiuchumi ya jamii yetu yanategemea sana mchango wa wanawake katika shughuli zao mbalimbali za kiuchumi, benki ya Wanawake itaziba pengo la upungufu wa mitaji. Pamoja na hoja ya kuanzishwa kwa benki hiyo, matayarisho muhimu kama utolewaji wa elimu ya biashara na ujasiriamali kwa wanawake ni muhimu sana. Kabla ya kutoa mikopo ni lazima benki yoyote makini itahitaji kupewa mpango wa biashara (*Business Plan*), pamoja na michanganuo ya miradi (*Project Write-up*) na kadhalika. Natoa changamoto kwa vyuo vyetu mbalimbali kama Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*) na hata vyuo vyta maendeleo ya Wananchi, kuifanya kazi hii ya kuwatayarisha wanawake kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya mfumo huu wa Demokrasia ya Vyama Vingi, upo umuhimu mkubwa wa kuwa na chombo huru ambacho kitawaunganisha wanawake wote bila kujali itikadi zao. Chombo huru yaani Baraza cha wanawake wote, hakitazamiwi kufuta wala kukinzana na vyama au vikundi vyta wanawake ndani ya vyama vyta siasa kama UWT, *UWUDP* na kadhalika. Baraza Huru litatoa nafasi kubwa zaidi kwa wanawake kusimama kama kundi moja lililosikamana kwa lengo la kuwa na sauti moja na kauli moja katika kutetea na kupigania haki za wanawake. Baraza Huru linamaanisha nguvu zaidi kwa wanawake wote katika kupigania ukombozi kamili wa mwanamke. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia wasaa huu tena kutoa mwito kwa Rais ye yeyote atakayechaguliwa, kutoka chama chochote kile katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 30, 2005, kufikiria umuhimu wa nafasi ya mwanamke kuwa Waziri Mkuu, Waziri wa Mambo ya Nje, Waziri wa Ulinzi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Waziri wa Fedha, Jaji Mkuu, Gavana wa Benki Kuu, Katibu Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na nyadhifa nyingine za aina hiyo kuanza kushikwa na wanawake. Hizo si nafasi ambazo zipo kwa ajili ya wanaume tu, wapo wanawake wengi wenye uwezo wa kushika Wizara nyeti (*Key Ministries*) na taasisi nyingine nyeti. Tanzania inao akina *Condoreeza Rice*, wengi tu amba ni imara kiusomi, kiuzoefu, kimaadili, kimaamuzi na kadhalika. Taifa lifikie mahali ambapo litaamini kwamba, wapo wanawake wengi wenye uwezo wa kushika nafasi nyeti na nzito Serikalini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zilizofanyika mpaka sasa, Serikali ya Upinzani, pamoja na mambo mengine, itachukua hatua zifuatazo ili kuboresha mazingira ya kujenga usawa wa kijinsia katika uwiano unaofaa:-

(a) Itatunga Sheria itakayotoa adhabu kali kwa mtu ye yeyote, atakayetumia mamlaka yake kumdhaliisha kijinsia na kumsababishia madhara ya namna moja ama nyingine, Mtanzania mwenye jinsia tofauti na ya kwake, ili kujinufaisha binafsi kwa njia moja ama nyingine. Pamoja na manufaa ya Sheria hii katika maeneo mengine, Sheria hii itasaidia hasa katika suala zima la kupambana na rushwa ya ngono, hususan kwa wanafunzi na waajiriwa wa kike. (*Makofî*)

(b) Itauboresha utaratibu uliopo hivi sasa ambao unatoa nafasi maalum kwa wanawake ili kuongeza ushiriki wao katika ngazi mbalimbali za maamuzi ya kisiasa, utawala, menejimenti na uongozi.

(c) Ili kuwanyanya wanawake kiuchumi, Serikali ya Upinzani, itaiimarisha Mifuko mbalimbali ya mikopo na kuisimamia ipasavyo kusudi iwanufaishe wanawake walio wengi wa mijini na vijiji bila kujali itikadi zao.

(d) Serikali ya Upinzani itawaunganisha wanawake wote bila kujali itikadi zao na kuunda chombo chao huru ambacho kitasimamia maslahi yao.

(e) Hata hivyo, kwa kuwa Upinzani unaelewa fika kuwa suluhisho la kudumu la matatizo ya kijinsia nchini liko katika kubadilisha mtazamo wa jamii kuliko kuweka shinikizo la kisheria na kutoa upendeleo, basi hatua zifuatazo za ziada zitachukuliwa: Kwa kuwa tafiti zinaonesha kuwa mabinti wanaosoma katika shule za peke yao, mara nyingi wanajenga kujiamini kuliko wale wanaosoma katika shule mchanganyiko, Serikali itahakikisha kuwa, kunakuwa na marekebisho katika mashule, ambapo mkazo mkubwa utakuwa kulifundisha kila kundi peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaala ya somo la Uraia shulenii itafanyiwa marekebisho ili pamoja na mambo mengine, somo hilo lilenge katika kufifisha mitazamo ya vijana wa kiume dhidi ya wenzao wa kike kuwa ni viumbe duni vinavyodhalilika na wasio na mchangwo wote wa maana kifikra katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaanzisha na kuhimiza Mjadala wa kina na wa wazi Kitaifa katika ngazi mbali mbali za jamii kuhusu mgawanyo wa wajibu, majukumu na haki katika mahusiano ya kijinsia kwa nia ya kuboresha mahusiano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadri siku zinavyokwenda, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, kinazidi kuwa na sura ya chuo cha kitaaluma cha elimu ya juu, ambacho kinayo majukumu yanayozidi uandaaji wa watumishi wa Serikali katika fani ya Maendeleo ya Jamii. Inashauriwa chuo hiki sasa kihamishiwe Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, ili kutoa nafasi kubwa zaidi kwa Wizara hii kushughulikia ufanisi wa Vyuo kama Buhare, Rungemba na vyuo muhimu vya Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*). Inashauriwa pia Serikali itambue umuhimu wa kuunganisha Taasisi ya Ustawi wa Jamii (*Institute of Social Work*), iliyoko Kijitonyama Dar es Salaam na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, kilichopo Arusha na ikiwezekana hata Chuo cha Sayansi Jamii Kivukoni, Dar es Salaam na kutengeneza Chuo Kikuu kimoja kikubwa na imara chenye matawi matatu (Tengeru, Kijitonyama na Kivukoni). Jambo hili litapunguza uitirii mkubwa wa vyuo vyenye majukumu yanayofanana na gharama kubwa za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana pana ya Maendeleo ya jamii ni kuondoa umaskini katika jamii yote katika sura zake zote. Inashauriwa kwamba, Serikali ijayo, kutokea chama chochote kile, iondoe shughuli za utaratibu wa kuondoa umaskini kutoka kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais na ziletwe kwenye Wizara hii, ambayo jukumu moja

kubwa na muhimu ni Maendeleo ya Jamii. Wizara hii ndiyo ipewe jukumu zito la kusimamia harakati za kuondoa umaskini na kuchochea maendeleo ya jamii. Ofisi ya Makamu wa Rais, iendelee na majukumu ya kuratibu, kuimarisha shughuli za muungano, uratibu wa *NGOs*, mazingira na maendeleo endelevu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na semina, makongamano, warsha, mikutano, maazimio na kadhalika, kuhusu haki za watoto na maendeleo yao, bado lipo tatizo kubwa la watoto wasio na mwenyewe katika jamii zetu. Zipo sababu nyingi zinazoleta kundi hili kubwa la watoto ikiwa ni pamoja na gonjwa la UKIMWI, mifarakano katika ndoa, mfumuko wa nyumba ndogo, vitendo vya ubakaji, malezi duni ya wazazi, sheria legevu, umaskini uliokithiri na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima sasa Serikali ifanye maamuzi ya msingi kuhusu ustawi wa watoto, yajengwe mazingira yanayomlazimisha kila mzazi kumtunza mtoto aliyemzaa. Wote wanaotelekeza familia zao ni lazima waadhibiwe vikali, kusiwe na msalie Mtume wala suluhu kuhusiana na wote wanaopenda kuwapa mimba wasichana halafu hawako tayari kulea watoto wanaozaliwa. Kila anayesababisha mtoto kuzaliwa, mke na mume lazima wabanwe kisheria kutunza mtoto walijemzaa. Kuzuka kwa dhana ya nyumba ndogo pia kunachangia watoto kukosa matunzo bora kuanzia nyumba kubwa mpaka ndogo na kunapanua wigo wa Ugonjwa wa UKIMWI kutamba. Jamii yetu ishikamane kukemea vitendo vyote viovu, ambavyo vinazalisha mateso makubwa kwa watoto na kutishia uendelevu wa jamii yetu na Taifa kwa ujumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo mengi yanayozuia wanawake wa kawaida wa mitaani na vijijini kupatiwa mikopo kwa urahisi na taasisi mbalimbali za fedha, bado namna bora zaidi ya kusaidia ukombozi wa wanawake si utoaji wa mikopo. Ni muhimu kutengeneza mazingira yatakayotoa nafasi kwa wanawake wengi zaidi kupata elimu ya juu, hasa katika nyanja za sayansi na teknolojia, masuala ya menejimenti na uongozi, masuala ya biashara za kisasa, mambo ya kibenki, kifedha na kadhalika. Jambo hili litawezesha wanawake kunyakua nafasi za juu za kimaamuzi kwenye Serikali, mashirika ya umma na sekta binafsi. Ukombozi wa wanawake haupo katika kuwapatia mikopo midogo midogo tu. Jambo la maana zaidi ni nafasi zaidi za elimu ya juu kwa wanawake na kupata nafasi zaidi katika uendeshaji wa Serikali na menejimenti ya uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaume kwa nafasi zao za kijamii na kiutamaduni na hata kiuchumi, wanao wajibu mkubwa sana wa kuwalinda wanawake dhidi ya Virusi Vya Ukimwi na UKIMWI. Mfumo dume unawapa nafasi wanaume kuwaburuza wanawake katika maamuzi yanayohusu mahusiano ya kujamiiiana na mambo ya ngono. Ni vizuri wanaume wakaamua kwa busara, kwa manufaa ya wanawake na jamii nzima. Wanawake ni pamoja na mama zetu, dada zetu, shangazi zetu na bibi zetu na wote hao wanahitaji kulindwa dhidi ya Virusi Vya Ukimwi na UKIMWI. Maambukizi ya UKIMWI ni makubwa sana miongoni mwa wanawake na wasichana na kwa bahati mbaya sana, hali ni mbaya zaidi kwa wanandoa. Wanawake wengi wanaougua UKIMWI wameletewa na wanaume wasio makini katika mahusiano ya kimapenzi na

masuala ya kujamiihana na hasa wanaume wasio waaminifu katika ndoa zao au kwa wapenzi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo familia nyingi ambazo zimesambaratika kufuatia wazazi kufa kwa UKIMWI na watoto wasio na umri unawaowezesha kujitegemea wameachwa bila ya usaidizi wowote wala mwelekeo wowote. Ni jambo la msingi kwa Serikali yetu kuwajibika zaidi katika kuwasaidia yatima wanaotokana na janga la UKIMWI. Msaada usiwe katika viwango vya utani vya kuwagawia vipande vya sabuni za kufulia, bali uwe ni msaada wenyewe uwezo wa kuwafaa kwa muda mrefu. Zoezi la kuwasaidia yatima hao ni lazima liwe na sera makini na pia liwe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wizara hii kuwa na kundi kubwa la Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, waliosomeshwa kwa fedha nyingi na wanaoendelea kulipwa mishahara kila mwezi, kazi yao haionekani kwa Wananchi wengi wa kawaida. Maafisa hawa hawaonekani kuhamasisha maendeleo mionganoni mwa Wananchi wa ngazi za chini. Maafisa hawa wako jirani na meza zao za ofisini kuliko walivyo jirani na Wananchi. Hizi ni zama za *delivery*, yaani kile kinachofanywa na Mtendaji wa Serikali kionekane. Sasa hivi duniani kote watu wanazungumzia *results-oriented management* na siyo mambo ya kuendeleza urasimu na umangimeza wa kujijengea himaya maofisini. Maafisa Maendeleo ya Jamii, watoke maofisini waende kwa Wananchi, wakaishi nao, wawe sehemu ya Wananchi, ili wayajue matatizo halisi ya kimaendeleo ya Wananchi na wasaidiane kuyatatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Majumba ya Maendeleo ni vituo maalum katika maeneo mbalimbali mijini na hata vijijini, vinawakutanisha Wananchi na hasa kwa lengo la kubadilishana taarifa, kupata habari mpya na kujumuika pamoja, kama mkakati wa kuchochea maendeleo ya kijamii. Katika miaka ya sitini na sabini, dhana ya majumba ya maendeleo na hasa mijini ilikuwa na umaarufu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo umuhimu mkubwa wa kuanzisha upya majumba ya maendeleo mijini na vijijini ili yatumike kuhamasisha maendeleo ya jamii kuitia cinema, michezo ya kuigiza, mikutano, warsha, semina, midahalo, makongamano na kampeni mbalimbali za kuhamasisha jamii katika masuala ya kimaendeleo, pamoja na suala zima la utetezi, hasa wa haki za wanawake, watoto, walemavu, wajane, waathirika wa Virusi Vya UKIMWI au UKIMWI, watu maskini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna bora kabisa ya kuleta maendeleo ya jamii na hasa vijijini, ni kuhimiza utolewaji wa elimu bora na endelevu ya menejimenti ya mazingira. Kuongeza uwezo wa jamii kutunza mazingira kunaongeza uwezekano wa kuwepo kwa Maendeleo endelevu (*Sustainable Development*). Maendeleo endelevu ni chanzo kikubwa cha maendeleo ya kijamii na kupungua sana, kama si kufutika kabisa kwa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara hii inafanya kazi *globally*, yaani imtambuka, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, tunaishauri Serikali kuwa, Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*), unaosimamiwa na *First Lady*, mke wa Mheshimiwa

Rais wa sasa, uwe ni mali ya Serikali na uendelee kusimamiwa na mke wa Rais yeote atakayekuwa Ikulu kwa kuachiana kijiti, kwa faida ya Taifa zima na kuufanya endelevu. Pia usionekane kama ni wa mtu binafsi, kwani tunatambua kwamba, wengi huuchangia Mfuko huu, kwa kuheshimu nafasi aliyonayo Mke wa Rais (*First Lady*). kwa maendeleo ya Taifa. (*Makofi*)

Aidha, naomba kuchukua fursa hii, nimpongeze Mama Anna Mkapa, kwa ubunifu wake na jinsi alivyoweza kuuendeleza Mfuko huo mpaka kufikia hapo ulipo. Naomba anayefuata aendeleze kazi nzuri hii na abuni vingine zaidi kwa manufaa ya jamii nzima ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya kweli ya kijamii yatokane pia na kugawana keki ya Taifa, kwa usawa au kidemokrasia sio kidomokrasia. Watanzania wengi ni maskini sana na pato kubwa zaidi la Taifa ilekezwe kwao badala ya kuendelea kuwaneemesha watu wachache sana wenye nguvu za kitaarifa, kiuchumi, kisiasa na hata Kiserikali. Keki ya Taifa ilekezwe zaidi kwa watu maskini sana ambaa ndio wengi na ndiyo wenye Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kinachonisikitisha sana ni kiporo cha kutofikia muafaka wa hatma ya sheria zinazokidhi mahitaji ya Haki za Wanawake na Watoto katika maeneo matatu ya Haki za Watoto, Sheria za Ndoa na Sheria za Mirathi. Naamini awamu ijayo itazingatia hili ili haki itendeke kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie muda huu, nimshukuru kwanza, Mwenyezi Mungu, kwa kuniweka hai. Pia nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Uchaguzi Bukene, kwa kunipa kura ambazo kiutaratibu wa chama changu, zilinisaidia kunipa nafasi ya kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum. Nawashukuru sana kwani kura zao zilinionezea uzito na ndiyo zimenipa sauti hii niliyonayo. Napenda kutamka rasmi kwamba, wakati muafaka ukifika, nitakuja tena kwenye Jimbo hilo hilo la Bukene. Naomba mnipe sauti tena safari hii niwakilishe jimbo, sauti ya jimbo. Nawaomba sana tushirikiane kufikia lengo hilo, kwani nia ninayo, uwezo ninao na sababu ninayo ya kuwatumikia wote. (*Makofi*)

Napenda pia nimshukuru kwa namna ya pekee, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mwenyekiti wangu wa Taifa wa *UDP* na wanachama wote wa *UDP*, kwa kunitueua na kuniwezesha kuwa Mbunge wao wa Viti Maalum, kwa kipindi chote hiki cha miaka 10, yaani vipindi viwili mfululizo kuanzia 1995 mpaka 2005. Nasema asante sana. Naamini nimetimiza wajibu na kazi mliyonituma ipasavyo. Pia nawashukuru kwa kunichagua kuwa Katibu Mkuu wenu wa *UDP* na hivyo kuvunja *record* na kunitengenezea historia ya pekee ya kuwa mwanamke wa kwanza na pekee kushika wadhifa huu katika vyama vyote vyaya siasa. Nawashukuru sana kwa kunipa wadhifa huo. Asanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru Viongozi wa Upinzani wote, waliopitia wadhifa huu kwa miaka 10, walionichagua kuwa Msemaji Mkuu wa Wizara hii mfululizo (1995 - 2000), Mheshimiwa Fatma Maghimbiri (2000 - 2005), Mheshimiwa

Dr. Amani Walid Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini na Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare, kwa ushirikiano walionipa. Nasema Asante sana, kweli mmenipa ujuzi mkubwa wa Wizara hii, ambayo inaniongeza *CV* yangu. Pia ninaamini kabisa nimetimiza malengo yenu, kwa maendeleo ya Taifa hili.

Nawapongeza viongozi wote wa Upinzani kwa mafanikio yote tuliyoyapata kutokana na usimamizi wao. Sisi sote tunajua tulikotoka kabla ya kuingia katika Mfumo wa Vyama Vingi, hasa tulipoingia Bungeni. Mafanikio yameonekana makubwa sana ya Taifa hili. Tunajua shule zilivyokuwa mlango na dirisha havijulikani, tunajua kero za Wananchi na kadhalika na tunathamini kelele zilizofanyika kutoka Kambi ya Upinzani, ambazo Serikali imezisikia na kuzitekeleza. Naamini kama alivyosema kaka yangu, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, akitoa mfano wa ngoma ya mdundiko, nami nakubaliana naye kwamba, ngoma ya mdundiko inapotokea Mwanarumango inakuwa na watu wachache, lakini inapofika mjini katikati ya Jiji inakuwa na watu kibao, wanaojua na wasiojua. Ndipo tulipo sasa. Nawashukuru sana viongozi wetu wa Upinzani kwa kuona mbali na pia nawashukuru Serikali kwa kusikia na kutekeleza kwa manufaa ya Taifa. Hongereni sana wote. (*Makofi*)

Namshukuru pia Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kunipa maneno ya faraja siku zote, ninapomwambia mimi ni Waziri ninayemsubiri, alionesha furaha na kunijibu kwamba, kila anayesubiri yuko pamoa na Mwenyezi Mungu. Ni maneno ya faraja sana. Ni maneno yanayoonesha kwamba, ana busara. Namshukuru sana. (*Makofi*)

Namshukuru vilevile Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim Khan, kwa ushirikiano alionipa. Kwa kweli hakunibagua eti mimi natoka Kambi ya Upinzani, la hasha, tulishirikiana vizuri na hata mahali pengine tuliwaacha watu wakishangaa, wote tunaheshimiana, tunafanya kazi kwa furaha, Wanyamwezi wanasema *nseko du*, yaani kicheko tu furaha, hakuna kinyongo kwanza cha nini? Nakushukuru sana. Mambo yote haya tumeyafanya kwa manufaa ya jamii. Mungu atubariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kazi yangu imewapendeza Watanzania wa vyama vyote na itikadi mbalimbali na naamini pia kwamba, Wananchi na wapiga kura wangu, wanapenda niendelee kuwatumikia kwenye nafasi hii ya Ubunge, safari hii Ubunge wa jimbo. Nawapa changamoto wanawake wenzangu, wanaowania Ubunge kwamba, tusiogope kujitosa majimboni. Ni lazima wanawake tusimame kidete kuwania Ubunge majimboni. Katika hili tusisinzie wala kulala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawataja watakaochangia, ningependa tu kutoa taarifa kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu, yuko safarini Arusha na Manyara na amemteua Mheshimiwa Dr. Pius Y. Ng'wandu kuwa Kaimu wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni. (*Makofi*)

Baada ya tangazo hili, sasa tunao wachangiaji kadhaa kwenye orodha. Sasa nitawataja wale wa kwanza wanne; Mheshimiwa Sophia M. Simba, atafuatiwa na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Edson M. Halinga na Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri.

MHE. SOPHIA M. SIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kabisa ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba niungane na wenzangu katika kutoa salamu za rambirambi kwa mwenzetu, mpenzi wetu aliyetuaga, Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana. Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali mpema peponi. *Amina*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuipongeza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Taarifa yao ni nzuri, mimi nikiwa kama Mwenyekiti, tumeipitia na kwa kweli wamefanya kazi kubwa. Lakini nichukue nafasi hii nimpongeze Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro na Naibu Waziri, dada yangu, Mheshimiwa Shamim Parkar Khan, kwa kazi nzuri ambayo siku zote wamekuwa wakiifanya ya kuiongoza Wizara hii, pamoja na Wakurugenzi wa Idara zao mbalimbali na maofisa wao. Kwa kweli sisi katika Kamati, tumekuwa tukifanya nao kazi vizuri sana wakiongozwa na Katibu Mkuu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kabla sijaanza kuchangia, nimpongeze Waziri Kivuli, kwa nafasi aliyopata wa kuwa Katibu Mkuu wa Kwanza Mwanamke wa Chama Cha Upinzani cha *UDP*. Kwa usemi huo, naamini Vyama vingine navyo vinasikia kwamba, inawezekana nafasi kubwa kama hiyo kushikwa na mwanamke. Hongera sana Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuzungumzia kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Kwa kweli Vyuo hivi ni kichocheo kikubwa cha maendeleo katika ngazi ya jamii kule tunakotoka, lakini tuna tatizo kubwa la vyuo hivi kutotambulika na wengi. Kwa kweli vyuo hivi vinafanya kazi nzuri na Serikali inajitahidi lakini mpaka sasa havijafikia malengo yake kama vinavyohitajika. Laiti kama wangkuwa wanapata msaada mkubwa, hata sisi Wabunge kama tungkuwa tunawatafutia wafadhilli, ninaona tungefika mbali kwa sababu sisi Wabunge ni Wakurugenzi wa Vyuo hivi. Lakini Vyuo vina hali mbaya kiasi kwamba, hata mikutano ya Bodi za Vyuo hivi haifanyiki. Matokeo yake leo hapa hata ukimwuliza Mbunge yejote, wengi hawajui ni kitu gani kinachoendelea.

Waliopewa Uenyekiti wa Bodi hizo ni Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji huko tunakotokea. Hao Wakurugenzi wamechukulia hivi Vyuo kama *by the way*, hawana msisimko na hivyo kwa sababu hakuna mikutano yoyote, Wabunge hawapati hata nafasi ya kushughulikia Vyuo hivi. Jitihada kubwa inafanywa na Wizara lakini Wizara iko juu, inatakiwa Wananchi wenyewe wakiongozwa na Wabunge wao, wavishughulikie Vyuo hivi ili Wizara ipate msukumo mzuri na ushirikiano mzuri. Pia Wizara ya Fedha,

nitashukuru sana kama itaangalia Vyuo hivi kwa ukaribu sana. Kwa kweli wanahitaji majengo yaboreshwe, wanahitaji nyenzo za kufundishia ziboreshw.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni kuhusu hivi vyuo vyetu vya Maendeleo. Lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi, sasa hapo niko katika jinsia. Sasa hivi suala la ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi siyo Mjadala tena. Kila mmoja wetu analielewa na Bunge hili ndio linaelewa vizuri zaidi, kwani hata juzi tulipopitisha sheria ile, hatukupata matatizo makubwa isipokuwa kwa rabsha rabsha ndogo ndogo tu, lakini Wabunge wameelewa umuhimu wa akina mama na akina baba, kushirikiana katika kuongoza Idara mbalimbali na kuongoza nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nina wasi wasi kidogo, juzi tulipitisha tukasema asilimia 30. Kwa bahati mbaya sana ukikaa kwenye mahesabu, ukipiga yale mahesabu, utakuta wanawake ambao wataingia Bungeni watakuwa ni asilimia 22 tu. Ni kosa ambalo kwa kweli imekuwa bahati mbaya sana kwa sababu tulichukulia ile Ibara ya 66 ambayo inazungumzia Wabunge wa aina mbalimbali. Wabunge wale wote kama wangehesabiwa wawe ndiyo *seventy percent*, kwa hiyo, *thirty percent* ingetafutwa kutokana na wale *seventy percent* tungepata idadi ya akina mama asilimia 30 ipasavyo. Ni tatizo la kimahesabu, ambalo kwa kweli kwa wale wanaojua hesabu, wakiweka hesabu ambayo yale makundi wakihesabiwa wale wanakuwa 249 wote, ufanye 249 mara 60 chini ya sabini utapata Wabunge wanawake wangkuwa 106.5, ambayo ingekuwa 107.

Sasa tumekuja kugundua hiyo na sheria ndiyo tumeshaipitisha imeshasainiwa. Ombi langu, ili Tanzania ifikie asilimia 30, vyama vya siasa vina jukumu la kuhakikisha nao wanateua wanawake kwa kiwango kisichopungua asilimia 30 kugombea katika nafasi mbalimbali kuanzia Udiwani na Ubunge. Hili ni Azimio la *SADC*, wenzetu Bunge la Afrika, imeshafikia asilimia 50 kwa 50, hawana mjadala na hilo. Sisi Bunge la *SADC* ambalo Rais wetu ametia saini, limesema wanawake wawe asilimia 30, wasipungue asilimia 30 na kwa upendo mkubwa, amehamasisha Wabunge na kila mtu amekubali kwamba, iwe asilimia 30. Sasa tatizo hili limejitokeza hata tukirudi *SADC* au *African Union*, idadi yetu ikishahesabiwa, tutaonekana hatujakamilika, tuna wanawake katika Bunge letu asilimia 23.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini wote tunataka Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aondoke akiacha *legacy* yake kwamba, amehakikisha wanawake asilimia 30 wako Bungeni. Sasa kazi kwa vyama vya siasa, wasimamishe wanawake. Wanawake kote walikosimamishwa walishinda. Kwa hiyo, vyama vyote vijitutumue na akina mama wanaona wana uwezo wajitokeze, sisi tunahamasisha tunawaomba, tunawasihi. Sisi akina mama katika vyama idadi yetu ndiyo kubwa, lakini katika uongozi, idadi ya akina mama inakuwa ndogo. Kwa hiyo, safari hii vyama vioneshe mabadiliko. Huko majimboni tuonekane wanawake tunapambana. Yale maneno ya kusema wanawake hawapendani wenyewe kwa wenyewe si kweli, ni wanaume ndiyo huwa wanaenda wanachochea, wanawake wanapendana. Hebu wawekeni wanawake wagombee halafu muone. Wanawake wagombee halafu mtaona itakavyokuwa. Kwa

hiyo, narudia tena, vyama vya siasa vichukue jukumu la asilimia 30 kuteua akina mama wa kwenda kugombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini vyama vya siasa vinawahitaji wanawake sana, sisi ndiyo wahamasishaji wakubwa na naamini watakubaliana nasi na watakubaliana na *SADC* ilivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningependa kuzungumzia Mfuko wa Wanawake wa Mikopo. Kwanza, kabla sijafika huko, ningependa niwapongeze sana wale akina mama ambao wamejitokeza wako Dar es Salaam sasa hivi kwenye Maonesho ya Saba Saba. Shukrani za pekee kabisa ziende kwa Mama Anna Mkapa, kwa Mfuko wake wa *EOTP* kuwa-support akina mama kwenda kwenye maonesho. Mfuko huu umefanya makubwa, umekuwa mkombozi kwa akina mama, wengine walikuwa hata hawajui maonesho ya biashara ni kitu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, aliyezungumza kwamba, Mfuko huu urudi Serikalini. Hapana haiwezekani, Mfuko huu ni Mfuko kama Mifuko mingine. Mfuko huu una *Board of Trustees*, una viongozi wake na utaendelea. Siyo kama Mama Mkapa akiwa siyo tena *first lady* na Mfuko utakufa, hapana, Mfuko huu hauongozwi na yeye binafsi, yeye ni kiongozi wa *Board of Trustees* wa hiyo *EOTP*. Kwa hiyo, dhana kwamba pengine kila kilichopatikana katika hiyo *EOTP* ni chake, hapana, yeye ameanzisha na amehamasisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee na Mfuko wa Mikopo wa Akina Mama. Kwa kweli Mfuko huu ni mdogo, uangalie wanawake waliopo vijijini, wanapewa mikopo ya kufanya nini na siyo mkopo tu, wale wanawake ambao ni wakulima wanaweza wakakopeshwa matrektu au zana za kilimo, ambazo wao wanaweza wakazitumia kwa kukodisha na kwa kukodisha wataweza kulipa. Lakini kwa wale wa mijini, unapompa mkopo wa Sh.100,000/= au Sh.50,000/=, mwanamke wa Kata ya Jangwani, Kata ya Ilala, Mchikichini, Upanga Magharibi, Mchafukoge, Kisitu au Gerezani hautoshi.

Hawa wanawake wanahitaji mikopo inayoanzia Sh.500,000/=, kwa sababu wale biashara zao ni tofauti, msidhanie wote ni mama ntilie. Wale biashara zao zinataka waweze kununua *cooler* za kuweka vitu vipate baridi, maturubai, viti, wanatafuta vyombo vya *catering services*, wanunue viti, maua, hizo ndiyo biashara za wanawake wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, mikopo ya wanawake wa Dar es Salaam, ipande ianzie Sh.500,000/= na kuendelea juu ili waweze kujikimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimpa mwanamke mkopo wa Sh.50,000/=, kurudisha inakuwa tabu matokeo yake anahama na ule mtuu, kwa hiyo, sisi wafuatiliaji hatumpati tena. Anaweza kukopa akiwa Kariakoo, baada ya kukopa anaweza akahama akaenda zake Kigilagila, utamjuaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, atakapokopeshwa mkopo mkubwa, kwa kweli huyu mwanamke atafanya kazi na tutaona yuko mahali gani na anafanya kitu gani. Kwa hiyo, naomba mikopo iongezwe ili akinamama wajikwamue. Kama mnayvojua, akinamama ni

hodari wa kulipa, sisi ni waoga wa madeni na ni hodari wa kufanya kazi. Sisi ndiyo tunaosomesha watoto, sisi ndiyo tunaofanya kila kitu, akina baba ukimpa mkopo wa Sh.500,000/=, anaweza kwenda kuhonga, lakini mwanamke atahakikisha anarudisha na kweli anarudisha. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ningependa nizungumzie kidogo kuhusu watoto. Siku ya Jumamosi, Kamati tatu zilipata nafasi ya kukutana na Baraza la Watoto. Watoto walikuja wakaongea na sisi Wabunge, wamekuja kuongea wakidai haki zao. Ni kweli mpaka sasa watoto bado wanahitaji haki zao zitekelezwe. Si vizuri wakati wote kujifananisha enzi zetu sisi wakubwa na wao, kwa mfano, tunapozungumzia viboko, unasema bila kiboko mtoto hasikii. Hapana, ni lazima wazazi waende na wakati. Vijana wanahitaji malezi bora, watoto wa kike wanahitaji na wao wapate nafasi ya kujisomea, ule utaratibu wa watoto wengine wafanyishwe kazi na wengine wasifanyishwe kazi, kwa kweli sasa uishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira za watoto hasa mijini, mimi najua kuna ajira za watoto mbaya sana huko mashambani, lakini hii imekuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. AZIZA S. ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi hii ya leo. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mheshimiwa *Hajjat Dr. Aisha Migiro*, kwa kazi nzuri anazozifanya yeye na Naibu Waziri wake. Pia, nampongeza Katibu Mkuu na watendaji wake na hasa nampongeza mwalimu wangu wa Chuo cha Uhazili, Mama Msemakweli. Ahsante sana kwa kunifikisha hapa nilipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, nami naungana na wenzangu, kutoa rambirambi zangu kwa ndugu, jamaa na Wabunge wote, kwa kifo cha mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amina*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichangie katika maeneo machache tu katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri. Naomba nianze katika eneo la watoto. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nilichangia kuhusu suala la dawa ya UKIMWI kwa watoto wadogo. Mheshimiwa Waziri alijibu, lakini sikuridhika na majibu ambayo yalitolewa kwa sababu nina uhakika kuwa watoto wengi ambao wazazi wao wameathirika kwa UKIMWI, hawapati hizo dawa. Maeneo mengi tunaenda katika vituo vya watoto, tunajua kuwa watoto hawapati hizo dawa.

Mheshimiwa Spika, bado ninapata shida na ninaelewa hata Wizara yenyewe inapata shida, kwa sababu Wizara hii inaitwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, lakini bado kuna watoto yatima ambao wanaenda Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Hapa naelewa kuwa, hata Wizara yenyewe hii inapata shida sana katika utendaji kazi wake. Kwa hiyo, ni lazima Serikali wakati mwingine iwe inaangalia inapopanga Wizara zake. Tunaweza tukawapa lawama sana Wizara ya Maendeleo ya

Jamii, Jinsia na Watoto au tukawapa lawama Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, lakini ni lazima kuwe na Wizara ambayo inalingana na jina na Wizara kwa jinsi linavyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la dawa za watoto, itakuwa hatuwatendei haki sana watoto ambao wanaachwa na wazazi wao wakiwa nao wameathirika na hawapati dawa. Ni lazima tuamini kuwa, watoto nao wanahitaji haki yao ili wapate dawa. Hiki ni kitu ambacho tunajibiwa hapa, lakini hakitendeki sawa sawa. Kwa hiyo, naomba na watoto waaangaliwe hasa katika vile vituo vyta kulelea watoto yatima na wale ambao wameachwa na wazazi wao wakiwa wanajua kuwa wazazi wao wameathirika na UKIMWI nao pia ni lazima wapimwe kwanza kuja kama wameathirika au hawakuathirika ili wale walioathirika waweze kuanzishiwa dawa na wao waweze kuongeza muda wao wa kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba niongelee kuhusu suala la mikopo asilimia 10 za Halmashauri. Hii kwetu sasa hivi imekuwa ni kama wimbo au matangazo. Kwa muda wote wa miaka mitano niliyokaa hapa Bungeni, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alisema asilimia 10 isitishwe ili kuwepo na utaratibu mzuri ambao utawekwa. Asilimia hiyo imesitishwa au pengine bado inaendelea kutolewa, lakini huo utaratibu kwa muda wote wa miaka mitatu mpaka sasa hado haujawekwa. Sasa, hili suala la mikopo ni kwa nini tuseme kwamba, kutakuwa na mikopo kwa asilimia 10 kwa vijana na akinamama wakati hakuna?

Suala hili kwetu ni kitendawili, hivyo ninaomba hiki kitendawili kiweze kuteguliwa kwanza. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, afuatilie kwa Waziri wa Fedha, ule utaratibu ambao umewekwa au ndiyo hiyo mikakati iweze kuwa ni MIKUKUTA ambayo inatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni kuhusu Maafisa Maendeleo ya Jamii. Katika Mkoa wetu wa Tabora, hakuna Afisa Maendeleo ya Jamii. Ninapata kigugumizi kuelewa kuwa utakuwaje na Wizara ambayo hakuna Afisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoo? Utapata wapi taarifa kwa kuweka kaimu tu! Huo siyo utekelezaji. Afadhalii hata kwenye Wilaya unaweza kuweka kaimu, lakini siyo kwa Mkoo. Hiki si kitu ambacho kipo katika mategemeo ya Mkoo wetu kwamba, kuwe hakuna Afisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, alifanya ziara katika Mkoo wetu, tunashukuru kwani na taarifa ametupatia karibu Wabunge wote wilayani na mkoani na nilitegemea kwa urahisi zaidi kuwa suala hili litawenza kutekelezeka na kuweza kupata Afisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoo kwa haraka sana. Kwa hiyo, tunatumia nafasi hii, kuiomba Wizara iweze kutusaidia Wanawake wa Mkoo wa Tabora, tuweze kupata Afisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoo ili maendeleo ya wanawake yazidi kuendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu haki au maadili ya wanawake. Katika nafasi hii, ni lazima tuelewe kuwa tukisema Maendeleo ya Jamii,

Jinsia na Watoto, hasa jinsia ni lazima jinsia wenyewe waweze kuelewa haki ya wanawake ni nini. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu makubwa, Wizara kwa kutumia Maafisa Maendeleo wa Jamii wa Wilaya na Mikoa, watatumia nafasi hiyo kuwaelimisha wanawake haki zao ni nini ili waweze kuelewa, kwa sababu kuna sehemu nyingi au nafasi nyingi ambapo mwanamke anaweza kupata matatizo na kudhulumiwa haki yake kwa sababu haelewi haki yake ni kitu gani na maeneo yanayohusika ni yapi. Haya tunaweza tukayazungumzia kwenye redio na *TV*, lakini bado wale wa vijijini wengine huko hakuna hata umeme, ndiyo maana Wabunge wengi wanapigia kelele suala la umeme. Uki sema tunazungumzia kwenye *TV* huku hakuna umeme hiyo *TV* anaionea wapi! Redio Tanzania haisikiki kule vijijini, kwa hiyo, wao wana wajibu ni lazima waondoke waende kule katika maeneo ya Wananchi ili waende kuwaelimisha, lakini wakitumia nafasi hizi watapata wale wanaishi mijini na maeneo ambayo umeme unafika na Redio Tanzania inapofika. Lakini tunaomba zaidi kwamba, pamoja na hayo, hiyo Redio Tanzania iweze kuboreshwa ifike maeneo husika wanapoishi Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu suala hili hili la haki ya mwanamke. Huyu mwanamke tunamtegemea sana katika upigaji kura, lakini bado huyu huyu mwanamke wa kijijini anahitajika lazima aelimishwe na katika kuelimishwa ni lazima aondokane na ule utaratibu wa kuva miwani.

Ninazungumza hivyo kwa sababu kuna kitu wanasema kutokujua kusoma na kuandika. Ni lazima niwe mkweli tu, wengine hawajui kusoma na kuandika, lakini ana haki yake ya kwenda kupiga kura. Kama sisi wanawake na Wizara ya Maendeleo ya Jamii ipo, ni lazima Wizara hii itumie nafasi hiyo ya kuwatumbia hao hao watendaji wao, waweze kwenda kuwaelimisha wanawake, hata kama ni kwa elimu ya watu wazima, kwa sababu tunahitaji nafasi zetu na haki yetu ya kupiga kura. Wananchi wetu wa vijijini tuwape nafasi hiyo na tuna nafasi nzuri za kuwaelimisha kwa kiwango kikubwa ili nao wawe na haki ya kupiga kura kwa sababu siyo wote tuliohatika kwenda shule, wengine katika utaratibu mmoja au mwingine na mazingira hawakuweza kwenda shule, lakini bado tunahitaji tuwape haki zao za kupiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake hao wanaweza wakawa wanapenda kwenda kupiga kura na kwa utaratibu amba o umeletwa wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, wamejiandikisha, lakini bado mwanamke huyo anapata kigugumizi ataendaje kupiga kura wakati hajui kusoma na kuandika? Lakini bado tunaweza tukafanya utaratibu huo kusudi yule mwanamke aweze kupata haki yake na hakuna Wizara ambayo inaweza kuwasaidia wanawake hawa bali ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mikopo, kama Mheshimiwa Sophia Simba alivyozungumzia, mikopo ya Dar es Salaam ni tofauti na ya Nzega, Igunga, Sikonge, Urambo na Uyui, kwa sababu wale Wananchi wetu kule Tabora tunaoishinao siyo kama wanavyoishi Dar es Salaam. Kwanza, magari yako mengi na barabara ni nzuri, sisi kule hakuna. Maji tu wanayatafuta kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, ni mbali sana. Kwa hiyo, ni vigumu sana na wao kuweza kulinganisha mkopo amba o utampa mpika maandazi wa mjini. Mkopo amba o utampa yeye ni ule amba o utakuwa wa kumfaa yeye kule kijijini, amba o ni lazima aweze kulima muhogo, tumbaku au karanga ili aweze kunufaika au aweze kutengeneza mkokoteni wake uwe na matairi

mazuri ili amuweke punda mbele aweze kubeba ile mizigo ya kuni na iweze kufika kule anakokwenda na yule punda angalau aweze kuwa na uhai. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuwe tunatofautisha, wanawake wa vijiji hatuwaangalii sana, lakini hao ndiyo wanaotufikisha hapa tulipo na wao ndiyo wakweli kwa sababu wakiamua kufanya kazi, wanafanya kazi kwa upendo na wanafanya kazi kwa amani zaidi. Sasa ni lazima Serikali iweze kuwaangalia kwa nafasi kubwa zaidi wale wanawake wa vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Mfuko wa Mama Mkapa, napenda kumpongeza sana Mama Mkapa, kwa nafasi yake ya kuandaa Mfuko huu. Sisi Wabunge, tumeshaanza kuutolea macho kwa manufaa ambayo yamepatikana na Mama Mkapa, akiwa ni mke wa Mheshimiwa Rais, naye ni lazima atakuwa ni kiongozi. Uongozi wake umetuonesha matunda kuwa na sisi tuna wajibu wa kuwafanya Wananchi wetu kama alivyofanya yeye.

Wapi anakopata yeye na sisi tutafute kule anakopata au na sisi tubuni njia zetu ili tuweze kuwasaidia Wananchi wetu. Tusiwe na moyo wa kuangalia tu yeye kafanya nini au huyu kafanya nini, ndiyo maana wanasema tuna wivu, penye ukweli ni lazima pasemwe bwana, ule wivu tuuache, tuwe na wivu wa maendeleo na maendeleo yenye we ya kusema Mama Mkapa kaandaa huu Mfuko kwa Wananchi wa Tanzania na mimi niandae Mfuko wangu kama Mbunge wa Mkoa ili niwasaidie wale watu wa Mkoa wangu. Mwingine pia anasema na mimi niandae Mfuko wangu wa Jimbo ili kuwasaidia watu wa Jimbo langu. Huo ni mfano ambao ametuonesha, kwa hiyo, tuache hizi tamaa, wivu na fitina, hazitatusaidia, tuwe na wivu wa maendeleo ya maisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuongelea kuhusu vyama kuweza kuteua Wabunge Wanawake kama alivyoongelea Mheshimiwa Sophia Simba. Vyama hivyo viteue Wabunge Wanawake na pia viangalie Wabunge Wanawake Vijana na ambao wataweza kuwasaidia. Nashukuru sana Chama cha Mapinduzi, kwa kupitia UWT, kutenga nafasi yake moja ya vijana na kwa kweli nimebahatika kufanya kazi hiyo kwa muda wa miaka mitano katika Bunge hili na nimeona mafanikio na mawazo ya akinamama wa UWT. Kwa kweli nashukuru sana kwani nafasi hii nimeitumia vizuri sana na vyama vingine navyo vijitahidi kuandaa utaratibu kama huu ili ile haki ya wanawake inayoliliwa, basi walilie na haki ya wanawake vijana na vijana wengine ambao ni wanaume. Ni lazima vyama vitenge utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utaratibu huo, Chama cha Mapinduzi kupitia UWT, kimeandaa utaratibu ambao kwa kweli ninaupongeza na nimeufurahia sana, uzidi kuendelea kama ni nafasi moja basi nina imani kuwa wataandaa utaratibu wa kuongeza nafasi zitakuwa mbili na ni kutokana na kuongezeka kwa asilimia 30. Huu ni mfano wa kuigwa na vyama vyote na kama si chama basi hata nchi nyingine ambazo hazijaandaa utaratibu huo na wao waandae utaratibu huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninakushukuru sana wewe, Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa kushirikiana katika muda wetu wa

miaka mitano nikiwa kama Mbunge wa Vijana na sasa sitagombea tena katika Ubunge wa Vijana, nitaingia kwa akinamama kuweza kugombea Ubunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tabora. Lakini bado ninawahamasisha vijana wenzangu wa Chama cha Mapinduzi na wao waweze kujitokeza kugombea Ubunge wa Vijana kupitia Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. EDSON M. HALINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ninaloliona ni kwamba, sisi hapa tunakaa tunazungumza, lakini siku zote hatufikii uamuzi kwa sababu ya hali yetu ya kimaisha, tunaifanya kama ndiyo msingi wa mabadiliko na kwa hiyo tunakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama ni wasemaji wazuri na haya wanayoyasema, mimi nasema wanayaharibu wenyewe. Leo hii wanaolalamika sana kuwa wanaonewa ni wasomi, ni wale wanaokaa mijini. Kule vijijini akinamama wana matatizo makubwa sana, hawana mahali wanapokutana, hata wote wanaosema hawa hawajaenda vijijini. Sisi tunakaa vijijini bado akinamama wanaishi maisha ya kijima kabisa, hata ukiitisha mikutano hawafiki. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya ndiyo mambo ambayo nadhani ni lazima akinamama wawe macho na Wizara hii itusaidie kuanzisha utaratibu wa *Community Centers* kwa kila kijiji. Kila kijiji kiwe na mahali pa kuwakutanisha akinamama hata baada ya kazi za jioni, wakae wazungumze mambo ya pale wanapokaa, wababilishane mawazo. Lakini tukitegemea kuwa hawa akinamama watabadilika kwa mikutano ya hadhara hawataweza kubadilika, maana wengi kwanza hawana nafasi na sehemu za kutembea mpaka kwenye kata wakasilize mkutano muda huo haupo. Kwa hali hii ni ngumu sana kuweza kufanikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba, hata shughuli zingine hizi tunazowapa nadhani Wizara yetu ijaribu kuangalia majukumu yanayopaswa kuelekeza, hata watoto, kwani leo hii tunasema chekechea ziwe chini ya Shule za Msingi, hivi Shule za Msingi kweli zitawalea hawa watoto wawe na uwezo wa kuelewa hali ya maisha yao! Wizara hii ikishaanzisha hizi *Community Centers*, waanzishe na Shule za Chekechea kwa kila kijiji. Pale ingekuwa ni jambo la msingi kabisa na Wizara hii ndiyo yenye malezi ya watoto na siyo Wizara ya Elimu. Hivi unategemea mwalimu akafundishe darasa la kwanza kweli! Wale watoto wametoka huko wana elimu yao, unawachanganya pale, halafu uje ufundishe na chekechea! Walimu hawana muda huo na hawawezi kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, tubadili utaratibu huu, hii Wizara iwe na mtindo wa kuanzisha hizi *centers* kwa kila kijiji, Wananchi watajenga tu jengo lao la maendeleo pale kijijini. Lakini kuwe na utaratibu wa kuratibu ili mambo haya yaweze kufanikiwa vizuri zaidi na hawa watoto wa chekechea wawe chini ya malezi ya Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii. Kwa suala hili tutajenga tabia na maisha yanayotakiwa kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo nyuma kulikuwa na magari ya sinema yanakwenda vijijini kuwaelimisha watu, hivi yalikwenda wapi na ni kwa nini yaliondoka? Yalifanya kazi nzuri sana, maana yalikuwa vijijini yanawaelimisha watu wote na akinamama kuhusu maisha yao, mapishi, kilimo cha mboga mboga na kadhalika, lakini leo hii haya mambo hayapo, sasa tunabaki tunaendelea kulaumiana tu, hatutakwenda mahali.

Hili tusipoliangalia bado litazidi kutugawa na wenyе nafasi sasa ya kuweza kupata uongozi wa nchi hii tunaodai kuwa sawa kulingana na usomi na wasomi wako zile sehemu ambazo ziliwahi ndio wasomi wapo wengi, hata ukiangalia hapa Bungeni, wanaokuja Viti Maalum wengi wanatoka Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya Mjini, lakini nenda kule Kamsamba, nani anajua mambo haya!

MBUNGE FULANI: Ilagila.

MHE. EDSON M. HALINGA: Wananiambia Ilagila. Nani anajua mambo haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaogombana ni wasomi tu, tunapigana hapa na tunawapumbaza hawa wasio na kitu, hawana nafasi na hawatakwenda mahali. Twende vijijini mkasemee kule, muelimishe watu wabadilike ndipo mtakuwa na nguvu ya kuomba kura zao, waje wawasaidie, muwe wengi hapa. Sasa unakwenda unawaambia tuwe wengi, unasemea hapa mjini! Mimi ndiyo ninayekutana nao vijijini nawasaidia, nawaelekeza waje wakupe kura wewe unayesemea mjini, utawapata wapi? Hili ni suala ambalo inatakiwa akina mama mliangalie katika kuwezesha kulingana hapa. (*Kicheko/Makofu*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu Benki ya Wanawake. Unajua mambo mengine tunadhani kwamba, ziko mahali fedha za kuchota na kuanzisha tunavyoamua, hazipo. Ni lazima tufanye mipango wenyewe. Serikali imeandaa utaratibu huu wa *Unit Trust*, kila mtu anunue vipande. Kipande kimoja ni Sh.100/=, unalipiwa Sh.30/=, wewe unatoa Sh.70/=. Hivi kweli Wizara hii ingesimamia suala hili mpaka vijijini, mama gani atashindwa kupata *units* 50 za Sh.3,500=? Hivi hela hizi zingekusanywa zote si zingeanzisha benki yenu ya kutosha?

Leo tukikaa tunazongumza ooh, tupewe hela tuanzishe benki, huyu Waziri wa Fedha, azipate wapi hela za kuanzisha benki wakati hizi ni za wazi kabisa?

Tushawishi watu benki hii iende mpaka vijijini, mpaka kule kwangu Ilomba watu wakachangie. Kule watu wana hela, wanatengeneza pombe za kienyeji wanauza, hakuna atakayekosa Sh.70/= kwa kipande. Sasa tunatangaza mijini humu, nani anashughulika na kununua hizi *Unit Trust*? Hakuna, hii ndiyo njia pekee ya kuanzisha benki. Tukikusanya fedha nyingi itapatikana kwani michango mingapi tunachanga?

Vijijini hawa akina mama ambao hawana nafasi lakini wana imani ya madhehebu yao, wanashiriki wanajenga makanisa, misikiti, leo tunashindwa maendeleo yetu

wenyewe kwa kutegemea kuwa kuna mtu ambaye atatoa misaada! Nani atatoa misaada? Hii fikra ya kutegemea misaada iondoke, akina mama mtusaidie kuiondoa kule vijijini ili tuweze kubadili hali ya maisha yetu, si suala la kusema kwamba, kuna anayemwonea mtu. Sasa mama hahudhuri mikutano, hata akipigwa nyumbani aende wapi? Apate mawazo mahali, mumwandalie mahali ambapo anaweza akasikiliza maoni na ushauri na akipata tatizo akimbilie pale kutatua tatizo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani iko haja ya kuliona hili na kuangalia. Akina mama ninyi mna nguvu sana na mna uwezo mkubwa kabisa, lakini hamna umoja wenu, mmejenga matabaka ambayo mnavutana na kuwaacha wale wengine na katika suala hili mafanikio yake yatakuwa madogo sana kwa sababu bado hawa walio kule vijijini wanahudumiwa na waume zao na katika jadi mwanamama ni lazima amtii mumewe na ni lazima ajali maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule siyo hayo tu, hata utoaji wa mahari kule vijijini bado kuna watu wanatozwa mahari ya kununua mtu. Sasa nendeni mkawaambie vijijini kuwa hii dunia si ya kununua watu. Yakiisha haya, hakutakuwepo na matatizo. Lakini sasa ukiacha vijijini kule ambako hata ninyi hamfiki, watu ndiyo wananaunuana kule halafu muwaache hawa.

Tuondoe tabia hizi, mila za jadi hizi ziondoke, tuwape watu uhuru vijijini waweze kuwa na nguvu ya kukabili matatizo na kuweza kushauri na kukabiliana na yale yanayotolewa na watu wengine wanaoleta uonevu. Watoto wanadhulumiwa hivi hivi kwa nini watoto wadhulumiwe na sisi tupo? Ni mahali pa kusemea, wasemee wapi?

Mtoto yuko huko Mvumi ameonewa, anachezewa, aende wapi akatoe malalamiko yake? Lakini tukiimarisha sehemu hizo za vijijini ndiyo ukombozi pekee na wa haraka ambaeo nadhani utaleta maendeleo na mabadiliko katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii. Nakuomba Wizara ifikirie sana uendelezaji wa *Community Centres* ili ziwe ndiyo kiini cha kuleta hiyo na wale wataalam wa Wizara hii waende pale wakawafundishe watu Vijijini. Lakini leo hakuna Afisa yejote wa maendeleo anayekwenda Vijijini akafundisha hawa. Wako Mijini tu na hata ukimpa pikipiki atakwenda wapi? Tuondoe hili ili apange hata ratiba yake kuwa leo ninakwenda Kijiji cha Mlagila au Ilolo Mahali, ijulikane kweli alikwenda kuelimisha watu. Lakini sasa hakuna! Huwezi ukasema kwa kweli Wizara hii inajiendoleza na inaleta mabadiliko Vijijini. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambayo naiheshimu sana. Awali ya yote naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa asubuhi. Nimekuwa naifuatilia, ni hotuba ambayo inatupa matumaini makubwa. Kwa hiyo, kwa

niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, ninapenda nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Asha - Rose Migiro kwa hotuba yake nzuri. (*Makofii*)

La pili, naomba nilete salamu za wananchi wa Jimbo langu la Siha hususan akina mama. Mheshimiwa Waziri Mwaka jana 2004, alipata nafasi ya kutembelea Jimbo langu la Siha baada ya kumwomba. Alifika akakutana na vikundi mbalimbali vya akina mama. Pia, alipata nafasi ya kuhimiza harambee kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Magadini. Ni wajibu wangu Dr. Asha - Rose Migiro kukushukuru na kukuambia ahsante kwa kazi nzuri ambayo uliifanya. Alikutana na akina mama wa vikundi vya Lawate, Vikundi vya Fuka, Vikundi vya Mae, Vikundi vya Nsherehehe, Ngarenairobi na Kuboko, akakutana na Vijiji vya Lakirimuni, Magadini, Kalansi na Kandashi. Alizungumza nao akawahimiza na kuwahamasisha katika masuala haya ya maendeleo kwa ajili ya jamii. (*Makofii*)

Ninakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro. Najua kwa nafasi yako unaweza kupata nafasi ya kushinda katika Jimbo letu la Siha kwa kufanya kazi kubwa kiasi kile. Kwa kweli ulijitolea sana. Napenda niseme hapa mbele yako kwamba katika harambee ile tulikusanya si chini ya Shilingi milioni 15 na nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, hivi tunavyozungumza sasa hivi watoto wameshaingia Darasani wako Kidato cha Pili, wamehama, walikuwa wanasomea Kanisani, lakini sasa hivi *Magadini Secondary School* imeshaanza. Nakushukuru sana, nakwambia ahsante sana. Naishukuru Serikali kwa kazi nzuri ambayo imefanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Siha bado wanaendelea kukumbushia ahadi za Mheshimiwa Waziri ambazo alitoa. Kuna vikundi mbalimbali ambavyo aliviahidi pamoja na Shule yenyewe. Najua kwamba unaifanyia kazi kwa sababu tumeshawasiliana. Kwa hiyo, nina hakika kwamba hilo litatekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunazungumzia mambo ya kuipeleka jamii na haki na kutafuta usawa na mambo mengine. Ni vizuri tukajua unapokuwa katika mifumo unawaweka wapi akina mama. Mara nyingi nimewahi kuzungumza hapa na nikirudia sio vibaya. Suala la haki si suala la kuomba. Suala la haki ni suala la kuchukua. Haki haiombwi, haki huwezi kukaa ukasubiri hisani ya mtu, haki unakwenda unachukua kwa kusema hivyo wala si kwamba nataka *advocate violence*. Nataka kusema kwamba akina mama kama wanasubiri, waseme mpaka hili kundi lingine liseme ndiyo au hapana. utashindwa hilo la kwanza.

Kwa hiyo, haki inachukuliwa una-*struggle* unachukua haki. Mimi nafurahi sana kwamba walikwenda *Beijing* kwenda kuangalia usawa wa akina mama wawe sawa na akina baba na jamii iweze kusonga mbele. Wamefanya hiyo *struggle* wamekwenda nao, wame-create platform, wamezungumza na slowly tunaanza sasa kuelewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu ya Tanzania na katika Bunge hili sasa tumesema kwamba wote watakaoingia katika Bunge hili angalau asilimia 75 wawe ni akina mama; wanatoka vyama vipi, ni kitu kingine kwa sababu ya *struggle*. Ujisoma historia ya kwetu hapa kwetu Tanzania dosari mbili kubwa zilizokuweko katika ujamaa kwanza ni teknolojia ya chini, yaani ninayozungumza ile *basic contradiction* ya vitendea

kazi na maendeleo ya jamii. Pili, akina mama walidharauliwa. Iko, nenda kasome ile *Ujamaa essays* ya Mwalimu, iko pale Mwalimu amezungumza hizo *contradictions* mbili ndizo ambazo unakuta pale *history*. Kwa hiyo, una *history* katika nchi yetu ambayo ina - *confess* na kukubali kwamba mwanamke alidharauliwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisema nataka nimwondoe mwanamke katika tatizo la kudharauliwa, kwanza unaangalia mfumo wenyewe kama una umaskini. Katika nchi ya Tanzania wanawake wanaonewa, humo humo ndani kuna umaskini. Wataonewa sana! Kama nchi yako ina maendeleo ya kiuchumi wanawake wanaonewa watakuwa na nafuu. Kama nchi yako ina sayansi na teknolojia ya kisasa mwanamke katika nchi hiyo ataonewa kidogo kuliko mwananchi ambaye sayansi na teknolojia ya nchi yake iko chini.

Kama umepeleka umeme Vijijini, maana yake ni kwamba, akinamama hawana ile adha ya kuhangaika kwenda kutafuta kuni haipo, kusema kwamba mwanaume anamwonea mwanamke, haipo kwa sababu kuna teknolojia ya kisasa, kuna umeme, watatumia pasi ya umeme, jiko la umeme, wataishi maisha mazuri. Ukitaka kumkomboa mwananchi wa Tanzania mwanamke, hapa la kwanza si kutafuta haki kati ya mwanamke na mwanamke. La kwanza ni ku-*address* suala la *economics* za nchi, achana na umaskini, mwanamke hataonewa. Ukibaki na umaskini mwanamke ataonewa sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke akienda Kijijini akasema nataka mnichague mimi niwe Mbunge wenu, hatutaangalia tu kwamba kiasi gani anawatetea wanawake, tutaangalia ni kiasi gani anatetea jamii yote nzima na tunasema hapa. (*Makofî*)

Unatoka hapa unakwenda pale, mimi nataka kugombea, nitahakikisha akina mama mnapata haki sawa. Huyu wa pili atakayekuja akisema nitatafuta haki sawa wa akina mama wapate haki, watu wapate haki, maendeleo yapatikane huyu atapata. Kwa hali hii, unawapeleka katika kugombea nafasi hizi zinazozungumzwa hapa. Mimi siwezi kumchagua mwanamama kwa sababu tu ni mwanamama, hapana. Nitafute kama hivi, hapana. Ndiyo tunataka mwanamama, lakini nataka ambaye anaweza akaniwakilisha.

Kwa hiyo, akina mama wakisema sisi tunataka kupeleka mtu pale, peleka mama ambaye unajua kichwa kinapiga. Unapeleka pale, watajaa humu ndani kibao na wako humu nawasikia wanazungumza na *history* imetuonyesha Margarth Thatcher safi sana, akina Goda Mayor safi sana, akina Indira Ghandi safi sana. Sina *problem* na suala la akina mama kufanya shughuli za uongozi. Wana uwezo. Ukiwapa nafasi watafanya vizuri tu. Lakini fanya hilo. Mwanamama gani ambaye akienda katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atafanya kazi ya kutetea na kupigana na umaskini? (*Makofî*)

Mimi akipita huyo nitamchagua. Mimi hapa hata kama unanilettea mwanaume, nikimwona huyu mama ni machachari, mimi nampa kura yangu haraka sana. Ndio maana nilikuwa mtetezi wa kwanza kutetea zile nafasi za akina mama ziongezeke hapa. Akina mama msije mkafikiri hapa haki itapatikana *on a silver plate, you are wrong! You got to fight for it! You got to struggle* na kuipata. Ikipatikana namna hii, watu wote watapata

heshima, watacaa hivi wanaangalia namna hii wanasema akina mama hawa tunawaheshimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jamii zetu zina tabia ya kudharau akina mama. Hiyo *mentality* lazima wanaume wakae waseme kwamba ni vibaya kudharau akina mama na akina mama waseme, jamii yote nzima iseme. Lakini huishii hapa, utakwenda zaidi ya hapo na hii ndiyo ninayozungumza. *South Africa* pale akina Winnie Mandela walipokuwa wanazungumza habari ya kuondoa *apartheid system* hawakuwa wanasema ondoa *apartheid system* kwa sababu tunataka akina mama wasionewe.

Walikuwa wanasema ondoa *apartheid system* ili mtu mweusi asionewe. Wanaanza hapo. Ndivyo walivyokuwa wanasema. Hawakuwa wanasema akina Winnie Mandela ile *popularity* waliyonayo pale walikuwa na *popularity* na nashukuru kwamba Wizara ilikuja kuliona hili ikasema ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *That is excellent!* Ndipo unapoina ile *the basic contradiction* mwanamke katika *apartheid system* anaonewa *equally* kama anavyooneewa mwanaume. (*Makofi*)

Lazima useme hapa kuna kitu kinachoitwa *antagonistic contradiction*, hii ni mgongano wa kihasama. Halafu kuna kitu kinachoitwa mgongano (*contradiction*). Mgongano wa kihasama pale *South Africa* au wakati tunapata uhuru ni kati ya sisi tunaoonewa na adui. Adui anawaunganisha mnakuwa kitu kimoja, mnasimama wote *as a united front* mna-fight mnasema ondoa hiyo *antagonistic contradiction*. Mgongano wa kihasama lazima uondoke kwanza.

Ukimaliza pale ndipo unarudi kwenye mgongano. Mgongano sasa unakuwa ni huu wangu mimi na huyu mwana mama hapa. Ondoa hiyo, lakini huwezi ukaanza na *contradiction* ukienda kwenye *antagonistic contradiction* unaunganisha kwanza na adui, adui akishakuunganisha una-fight unaondo, unarudi unasema, hivi sasa nataka haki kati ya mimi na wewe hapa. Ndivyo wanavyojipanga. Sasa hivi *South Africa* mmasikia Makamu wa Rais wa Jamhuri ya *South Africa* ni mwanamke, baada ya huyu aliyeondona bwana huyu, wamemweka mwanamama. Wale akina mama kwa sababu walikuwa *very clear*, wamefika hapo walipofika. *Hi* akina mama. Natambua nina dada zangu na ninatambua mimi nimezaliwa na mama siwezi kuona akina mama wa Tanzania wanaonewa. Lazima nizungumze kwa niaba ya akina mama wapewe haki zao na wao watuwakilishe (watu-represent) wafanye kazi za uongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, unajiuliza sasa tunaondoka kwenye *orientation* hii ya kijamaa tunakwenda kwenye *orientation* ya kibepari. Ukienda katika mfumo wa kibepari mfumo ule katika uzalishaji uko *social*.

Watu wa leo, walalahoi wanafurahia kazi, wanawekwa kwenye *conveyor belt*, tajiri na ye ye anaingia kwenye *conveyor belt*, tajiri naye huwa anafanya. Wakina mama, watoto wote wanaingizwa pale na nia na shabaha ya mfumo ule ni kutengeneza kitu kinachoitwa faida kibao (*supper profit*) na ndiko tunakokwenda sasa hivi. Ukienda katika mfumo wa namna ile ukaingia mle ndani bila kuangalia sasa mnafanya nini pale mtapata matatizo. Mfumo wa kibepari katika uzalishaji ni mfumo unaofanana na mfumo wa

kijamaa. Tatizo la mfumo wa kibepari ni kwamba unapofika katika *level* ya mgawanyo na mapato ndipo mnapoachana. Hawa wote niliowataja wanawekwa pemberi, anatoka mtu mmoja kama Mheshimiwa Lukuvi pale anakamata kila kitu, ndiyo tatizo linakoanzia pale. (*Kicheko*)

Kama nia na shabaha ya mfumo huu ni kutengeneza faida kibao, lazima Serikali isimame imara. Itasukuma mpaka watoto wadogo wa umri wa miaka mitano/kumi/kumi na tano watapelekwa kwenye *conveyor belt* ili kutengeneza faida kibao. Ndio vita unavyoisikia. Hapa ndani wanaajiriwa akinamama, wanaajiriwa watoto. Punda ukimpakia ukampa mzigzo wa viazi au mahindi au chumvi, ukimpakia mtoto wake punda anaketi chini haendi. Punda hawezi kwenda ukimsukuma. Haendi! Profesa Daimon Mwaga naona unaniangalia, kama huna habari hiyo ndiyo hivyo. Huwezi ukambebesha punda mizigo ya viazi ukambebesha na mtoto wake akakubali hata kidogo.

Lakini Tanzania hapa watoto wanachukuliwa wanapelekwa Mererani wanakwenda kutumikishwa, kuna *District Commissioner*, kuna Katibu Tarafa, Kuna Katibu Kata, Mwenyekiti wa Kijiji, wako pale wanaangalia kuna Chama pale, kuna Serikali, wanaangalia watoto wanaoneewa. *Why?*

Mimi nilipokuwa Arusha kulikuwa kuna kitu kinaitwa chokoraa. Nikasema mimi as a *District Commissioner* there is no way naweza nikaruhusu jambo hili likaendelea, Serikali yetu ikasimama imara kama nyanja mbalimbali hizo ninazotaja namna hii *Regional Commissioner* akaweka ngumu hakuna kuajiri, mtoto. Ukiulealea namna hii, huu mfumo ni mfumo wa ajabu unaitwa a *cut throat competition*, unafanya kazi ya kukata shingo hivi inaanguka chini. Watoto wa Tanzania wanawezaje wakaajiriwa hawaendi Shule na Serikali ipo? Mimi *appeal* yangu Mheshimiwa Waziri ni kwamba simama weka, ngumu sema haajiriwi mtoto wa Tanzania hapa wakati tukiwa hai. Ukiwekwa ngumu namna hiyo, huna *problem*. Hiyo ndiyo ambayo nataka kuizungumzia hapa. Baada ya hapo utawaangalia akina mama, utaangalia *schemes* zao na nini na vitu vingine. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, maana najua sasa muda unataka kuniishia hapa, nilitaka tu niseme kwamba, bado tuna tatizo kubwa sana kwenye ule Mfuko wa Vijana na akina mama ambao wenzangu wameuzungumzia. Tulisema kwamba asilima 10 ya pesa hizi zipelekwe kule. Katika Jimbo langu la Siha tunapiga kelele kila siku tunakwenda Halmashauri tunadai hela zile asilimia 10 kwa ajili ya vijana ziko wapi?

Ninao vijana Sanya Juu, Ngalenairobi, Karansi, wako vijana Bagamoyo, Bagamoyo siyo hii ya kwetu ya Kisarawe ya Mheshimiwa Kikwete, hapana ni ya kule Sanya Juu. Wanataka mikopo hawapati. Unakwenda pale, tulisema asilimia 10 ya Bajeti iliyopatikana, iko wapi? Umepata Sh.100/=, tenga asilimia 10. Mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri utakaposimama hapa ni vizuri tukaelezwa vizuri kuhusu Mfuko huu. Iweje Serikali inapitisha Azimio inasema kwamba watu wapewe asilimia 10 kwa ajili ya akina mama na vijana na haipatikani? *Why? How do you fight poverty* kama hiki ambacho sisi wenyewe tumekiwekea Azimio hakitekelezwi?

Juzi hapa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri tuliambiwa kwamba tumesitisha kidogo tutaweka utaratibu mzuri. Hatukuelezwa tena kwamba itakuwaje. Mheshimiwa Waziri alipokuja katika Jimbo la Siha aliwasikia akina mama wakipiga kelele. Natambua kwamba kuna zile fedha zimeletwa Shilingi milioni nne, lakini hizi zilikuwa zinasaidia. Kuna zile ambazo tulisema zitengwe na Halmashauri, sikuiona hiyo. Kila siku inapigwa chenga. Mheshimiwa Waziri inabidi amwangalie *DED* pale anasema nini. Halmashauri yenye haina. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa amesimama *ana-sum up* atueleze vizuri, huu Mfuko umesitishwa moja kwa moja haupo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena kwamba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, ninaunga mkono hoja hii na narudia kusema ahsante sana Dr. Asha - Rose Migiro kwa namna ulivytusaidia. (*Makofit*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Pia, naomba nichukue nafasi ya pekee kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na hasa akina mama kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri katika kipindi chao cha madaraka, wamewahi kuja katika Makao Makuu ya Mkoa wa Ruvuma yaani katika Mji wa Songea, bahati hawajapata nafasi ya kufanya ziara kule, lakini kazi zilizowaleta kwa namna moja ama nyingine zilikuwa zinawasilisha dhana halisi ya Wizara yao katika kuleta Maendeleo ya Jamii katika nchi yetu ya Tanzania na katika Mkoa wetu kwa kadri ya walivyoweza kutembelea. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi ya kuwapongeza na kushukuru na kwa muda huu mfupi kama wanaweza pia kufanya ziara kule tungefurahi na tungewashukuru sana. Tunaendelea kuwakaribisha na kuwatachia kila la kheri katika shughuli zao. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba nimeipokea vizuri hoja ya Mheshimiwa Waziri na ninasema kwamba toka Wizara hii tuipe mtazamo mpya wa kushughulikia suala zima la jinsia na maendeleo ninadhani kwamba sasa Wizara inaanza kupata mwelekeo ambao kwa kweli unaendana na hali halisi ya mahitaji ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la maendeleo ya wananchi wa Tanzania, mimi nadhani kila siku ninapochangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri nina hakika kabisa liko katika dhamana ya Wizara hii na ninaamini kabisa Wizara hii ikiweza kuwezeshwa vizuri, ndiyo itakayoweza kuleta changamoto kubwa ya kupambana na umaskini na kuleta maendeleo endelevu katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia jinsia, tunakubaliana kwamba ni mahusiano bora kati ya wanaume na wanawake katika kujisogezza ama kuleta mabadiliko ya namna moja ama nyingine. Dhana nzima ya jinsia kwa kweli haimlengi mwanamke peke yake, inamlenga mwanaume na mwanamke katika kuleta mabadiliko ndani ya jamii yenye haina. Ninaomba Mheshimiwa Waziri na hatimaye Wilaya, Mkoa na kadhalika katika nchi nzima ya Tanzania.

Kwa hiyo, mimi ninaomba kwa kweli sasa imefikia wakati muafaka kwa Wizara hii kuanza kusimama kidete pamoja na maazimio mengi ya *Beijing* na mikataba mingi ambayo imeshashughulikiwa ya kumwangalia mwanamke katika jicho la namna ya pekee lakini kwa kweli mimi nataka kusema sasa ni wakati muafaka wa kubeba dhana ya jina la Wizara kwa maana ya jinsia ili kuielekeza jamii ileweke sasa umuhimu wa kuunganisha nguvu kati ya wanaume na wanawake na kuwaletea maendeleo endelevu kutoka kwenye kaya zao na hatimaye katika jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze kwa kutolea mfano kwenye huu mfuko wa wanawake na vijana amba Mheshimiwa Mwanri, amekuwa akiupigia kelele hapa sasa hivi na Waheshimiwa Wabunge wengine. Mimi nasema kwamba uwepo wa Mfuko huu ni kitu kizuri. Lakini binafsi yangu nasema kwamba Mfuko huu sasa hivi taratibu zake nadhani zinaanza kutokuwa zinaendana na wakati. (*Makofii*)

Mfuko huu naamini kwamba kama kwa makusudi mazima Wizara itaamua kubadilisha muundo mzima wa Mfuko huu utakwenda moja kwa moja katika dhana yenye ya maendeleo. Waheshimiwa Wabunge, wanalamika mikopo yake ni kidogo, wakati mwingine inachelewa kufika, asilimia 10 hazitengwi na mambo mengine kadha wa kadha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nashangaa, kama Wizara hii inashughulikia suala zima la maendeleo ya jinsia, ni kwa nini, ama lini tutaona kwamba sasa ni wakati muafaka wa kutumia Mfuko huu kufanya kazi ambazo zinahusika na suala zima la maendeleo moja kwa moja kulingana na mazingira halisi?

Kwa mfano katika kipindi chote ambacho tumekuwa tukipokea taarifa ya Mheshimiwa Waziri, amekuwa akituletea hapa kitita kinachoonyesha zana bora za kufanya kazi na zana bora za kufanya kazi kama zinaweza kuwafikia walengwa wakiwemo wanawake na wanaume kwa dhana hiyo ya jinsia ndani ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ina maana kwamba tutakuwa tumewafanya wanajamii hao kuendelea katika masuala yao mbalimbali.

Mimi nafikiri Mfuko huu sasa uchukue sura ya maendeleo, uchukue sura ya kuweka Bajeti maalum katika Wizara ya kununua majembe ya kukokotwa na ng'ombe ili kuwasaidia wanawake na wanaume kwa dhana ya jinsia kuondokana na jembe la mkono na kuingia kwenye teknolojia halisi ya uzalishaji katika maeneo ya jamii. Ninaendelea kusema kwamba Wizara hii ndiyo yenye kuleta maendeleo ya jamii. Sasa hata kama inakuwa na Mfuko wowote ulenge kwanza katika jinsia; pili, kuleta maendeleo na kuboresha hali ya uduni wa maisha ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo, haiwezekani na kama bado Mfuko huu unakadirwa na matatizo ya wakopaji kutokulipa mikopo ambayo inakuwa imechukuliwa katika Mfuko huu, ni kwa nini basi Mfuko huu usijiingize katika dhana ya Akiba na Mikopo kwa kusaidia Vyama vya Kuweka na Kukopa ambavyo vimekwishaanzishwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ya Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo *SACCOS* nyingi. Ziko *SACCOS* za akina mama, ziko *SACCOS* ambazo ni za jamii kwa ujumla. Mimi nadhani sasa ni wakati muafaka Mfuko huu uondoke katika kunyanyapaa huko ambako kila mwaka tukija matatizo ya Mfuko, wakati tayari ziko Asasi nyingine ambazo zingeweza kufanya kazi hiyo ya Mfuko zimeonyesha uwezo, zimejenga uwezo wa jamii, zinafanya kazi vizuri, lakini kwa nini Wizara inachelewa kufanya maamuzi hayo ya kuhamisha utendaji wa huo Mfuko kulingana na jinsi jamii ilivyopiga hatua katika kujiletea maendeleo? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposoma haya ndiyo ninasema kwamba kwa kweli kiutaratibu kama tutaendelea kuubeba Mfuko huu kwa mtazamo wa kulalamika nao kila siku, basi mimi naomba niseme kabisa Mfuko huu umepitwa na wakati na ni lazima ujibadilishe, utoke katika utaratibu huu ambao siyo endelevu uingie katika utaratibu endelevu utakaoiwezesha jamii kupambana na umaskini na kujiletea maendeleo kutoka katika kaya kwa mahusiano ya baba na mama hatimaye katika Mtaa, Kijiji, Kitongoji na vile vile Mkoa na hatimaye Taifa zima la Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri achukue ushauri wangu kwa kweli kama angeweza kuangalia jinsi ya kuboresha hayo niliyoyazungumza basi nadhani Mfuko huu sasa ungeweza kuwa na picha nyingine nzuri inayowezekana na inayoweza kutendeka. Mheshimiwa Waziri anafahamu Mkao wa Ruvuma wanawake na *SACCOS* zao, kwa muda mrefu nimemweleza na nimekuwa nikimpa taarifa hizo kila mwaka.

Sasa Mfuko huu ungewawezesha wale akina mama kukopa pembejeo, kuweka fedha kwenye ile Akaunti ya Akiba na Mikopo, kununua mikokoteni ya kuvutwa na punda na kufanya shughuli za namna hiyo. Mheshimiwa Waziri, wale wanawake wa Mkao wa Ruvuma na jamii nzima ya wananchi wa Mkao wa Ruvuma, wangkuwa wamekwishapiga hatua kubwa sana kuliko kuendelea kupiga kelele za kutokurejesha mpaka lini Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

Kwa hiyo, naomba sana Wizara yako iangalie namna gani itabadilisha mfumo wa Mfuko huu ili kuleta maendeleo kama nilivyo sema hapo juu. Mheshimiwa Waziri ninaumia sana na suala la watoto chini ya umri wa miaka mitano. Ninadhani unafahamu kabisa mara nyingi nimekuwa nikikuuliza watoto wa chini ya miaka mitano ni mali ya nani? Wamekuwa hawana mwenyewe! Kila Wizara inawahusu kwa namna moja ama nyingine. Ukiwapeleka kwenye masuala ya afya, Wizara ya Afya, itawashughulikia, kwenye masuala mengine itawaacha. Atakuja Waziri wa Kazi, atashughulikia kwenye masuala ya matunzo na nini pamoja na sheria nyingi za kuwalea hawa watoto zimeshapitwa na wakati.

Kwa mfano ile sheria ya kulipwa Shilingi mia moja kwa mwezi kama fidia ya matunzo kwa mtoto. Kwa hiyo, utakuta kwamba watoto hawa wanalelewa katika taratibu tofauti kutokana na kwamba kila Wizara ina jukumu lake la Kisekta la kuwatazama watoto. (*Makofî*)

Mheshimiwa Waziri, lakini kila siku mimi nasema, kisayansi inaaminika kabisa kipindi cha mimba mpaka miaka mitano ubongo wa mtoto ndio unakua na kufanya kazi zaidi ya maisha yake mengine yote aliyobakia nayo. Mheshimiwa Waziri, naomba suala la watoto wadogo sasa lichukuliwe kwa nguvu wajulikane wanalelewa vipi na nani anawahudumia kabla hawajachukuliwa na Mheshimiwa Mungai, wakati wa kuingia kwenye zile Shule za Awali wakijiandaa na masomo yao ya Shule za Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Mwanri. Kwa kweli amezungumzia sana uwakilishi wa wanawake. Lakini kwa kuzingatia uwezo wao wa kuwakilisha jamii nzima katika maeneo wanayotoka. Mimi kwanza niipongeze sana Serikali ya Tanzania. Serikali ya Tanzania imewawezesha wanawake wengi kwa kiasi kikubwa kuonyesha uwezo walionao katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Kiserikali, ya Kisiasa na kadhalika katika nchi hii ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisiti kusema kwamba Serikali ya Tanzania ina akiba sasa ya wanawake wenye uwezo, wanaoweza kufanya kazi mbalimbali kama wawakilishi wa Bunge katika maeneo mbalimbali, wakiwa Wabunge wa Viti Maalum, wakiwa Wabunge wa Majimbo na tunaona mfano. Tulikuwa na mama yetu Anna Abdallah amefanya kazi ya ajabu sana katika Jimbo lake, Tunamwona Mheshimiwa Mama Makinda amefanya kazi ya ajabu sana katika Jimbo lake.

Lakini wako wanawake wengine wengi wa Majimbo tumekuwa nao humu ndani Manaibu Mawaziri tumekuwa nao akina Hadija Kusaga na wengine wamefanya kazi vizuri sana. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mwanri, kwamba wako wanawake wenye uwezo wa kufanya kazi na kama wanawake hao wapo, basi Vyama vyta Siasa vione kwamba vina umuhimu wa kuwapa nafasi washiriki katika kuleta maendeleo kwenye nchi hii ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo, nikirudi kwenye dhana yangu ya mahusiano ya kijinsia, tunapokwenda kwenye dhana nzima ya mahusiano ya kijinsia, basi hatuna budi kuhakikisha kwamba hatuwaachi wanawake katika mlolongo na mbio zozote zile ambazo zitaleta maendeleo katika nchi yetu. Navishauri Vyama vyta Siasa vione umuhimu wa kuwateua wanawake katika kugombea nafasi mbalimbali kupitia Vyama vyao ili kuongeza hiyo asilimia. Lakini Vyama hivyo viangalie kwamba wanawake hawa wawe ni wanawake wenye uwezo na si kila mwanamke ateuliwe. Lakini waangalie wanawake wenye uwezo ili kuendelea kutoa mifano bora katika jamii yetu ya Watanzania na hivyo kutuwezesha kufanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi kusikia Mheshimiwa Waziri anasema ataanzisha utaratibu mzuri wa ukusanyaji wa taarifa za shughuli mbalimbali zinazowahusu wanawake katika maeneo tofauti. Mimi nimeshukuru sana, lakini naomba niendelee kusisitiza kwamba maeneo ya Vijijini yapewe nafasi. Katika maeneo yetu ya Vijijini wako wanawake, pia wako wanaume ni wagunduzi wa masuala mbalimbali ya kimaendeleo, ni wakulima bora wenye kuonyesha mifano halisi ya jinsi gani hali ya mwananchi wa Tanzania inaweza kupiga hatua katika maendeleo. Kwa hiyo, katika

kukusanya taarifa hizo, Mheshimiwa Waziri aangalie sana na ahakikishe maeneo ya Vijijini yanapewa nafasi. (*Makofii*)

Kuna siku nilimwuliza Waziri wa Kilimo na Chakula kwamba uzalishaji kupitia kilimo ni asilimia 70 katika nchi ya Tanzania. Je, wanawake wanachukua asilimia ngapi kati ya hizo asilimia 70? Lakini siku ile niliambiwa kwamba kwa bahati mbaya hatujui uwiano huo mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, ni taarifa ambayo inatupa changamoto kwamba katika mipango yote tunayoifanya tuhakikishe kwamba tunaelewa na kuona umuhimu wa kuangalia maeneo ya Vijijini yanashiriki vipi katika suala zima la kuleta maendeleo kwenye nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, naomba kumshauri sana Mheshimiwa Waziri, atakapofikia katika suala hilo aweze kulitilia maanani.

Mheshimiwa Waziri, ninaomba hiyo Benki ambayo tumekuwa tukiipigia kelele siku nyingi ianze. Mheshimiwa Waziri tunaomba Benki hiyo ianze ikiwezekana kipindi hiki kabla hujaondoka madarakani, basi hebu tuanzishie hiyo Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofii*)

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia mawili, matatu ambayo yanagusa kama mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mama Asha-Rose Magiro pamoja na Naibu Waziri Mama Shamim Parkar Khan kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya kama wanawake. Pia, niwapongeze Wataalam wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya kwa ushirikiano waliouonyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia baada ya msiba wa jirani yangu, rafiki yangu, naomba nitoe salamu za uchungu mkubwa za rambirambi kwa familia ya Marehemu kwa msiba mzito walioupata ambao hawakuutegemea na nimwombe Mwenyezi Mungu kwa huruma zake aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongea hayo, nitoe pongezi ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Mama Anna Mkapa kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwasaidia wanawake na kuelimisha wanawake kuondokana na umaskini. Nampongeza sana. Lakini pia kwa sababu ni mwanamke, ninaomba hata baada ya Mheshimiwa Rais kupumzika au kustaafu aendelee kutulea na kutafuta wafadhili mbalimbali kama alivyokuwa amezoea na pia kuwalea walemvu kama alivyokuwa amezoea. Naomba sana sana kwa salamu hizi kupitia kwa Mheshimiwa Waziri atupelekee kama wanawake kwamba aendelee kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni Wizara Mama na ni kiungo kikubwa sana katika jamii nzima. Kuna mambo mengi ambayo yanahitaji msaada kutoka kwao. Kwa mfano kuna sheria nyingi sana ambazo zinawagusa wanawake na watoto ambazo

mpaka sasa hazijafanyiwa marekebisho kama walivyozungumza Wabunge wenzangu waliotangulia. Sheria ambayo inagusa sana wanawake ni hii Sheria aliyoizungumzia Mheshimiwa Jenista Mhagama ya kiwango cha malezi ya watoto wanaozaliwa nje ndoa na ambao ndiyo wengi na ndiyo hawo ambao sasa hivi wameongeza Taifa letu kuwa na watoto ambao wanawaita Watoto wa Mitaani kwa sababu ya kutokana na malezi. Hii Sheria mpaka leo inasomeka ni Sh.100/= Kama ni Sh. 100/= kwa miaka hiyo iliyopita ilikuwa ni hela ambayo ina thamani, kwa sasa hivi haina thamani. Kwa sababu haina thamani Wizara hii sasa ndiyo ishike bango kuishauri Serikali na kumshauri Mwanasheria Mkuu alone hili kwa uchungu. Maswali mengi yanaulizwa ndani ya miaka mitano, linalozungumzwa ni kwamba bado Sheria hajakamilika, Sheria inachunguzwa. Hivi Sheria hiyo inachunguzwa, mbona Sheria nyingine zimeshabadilishwa? Kama kuna Sheria Mama zimebadilishwa, naomba sheria hii iangaliwe, inatumiza sana Mitaani na imetubana kiasi ambacho jamii nzima inashindwa kuielewa Serikali inaangalia jinsi gani ya kuweza kulitatu hili tatizo ambalo watoto wanasomeka kama hawana baba. Wana baba zao wengine wamejificha tu, hatutaki kuwataja taja. Kwa hiyo, nilikuwa naomba mwanamama, Mheshimiwa Waziri na Wizara yako itunge Sheria ambayo inaweza ikafanyiwa marekebisho na sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Sheria ambazo hazijatungwa na kama zipo hazijafanyiwa marekebisho kuhusu hawa watoto wa Mitaani wanaolelewa na *NGO*. Serikali kama imejitoa ni vyema ikaangalia tena upya suala zima la watoto ambao wanakwenda kukusanya wanawekwa kwenye chumba kimoja, tayari watoto yatima wanaitwa wafadhili na wafadhili wanasaidia. Serikali iko wapi kuhakikisha kwamba hawa watoto wanawekwa mahali maalum ambapo Serikali iombe wafadhili kutoka huko wanakopata hizo *NGOs*? Tunaona kwenye *TV* watoto wanawekwa kama 10, 15 tayari watoto yatima. Je, Serikali inafuutilia kuona kweli hawa watoto ni yatima? Kama ni yatima, wametokana na nini? Ni vizuri Serikali ikawa na takwimu za uhakika kwenye *NGO* hizi ambazo hata ukimleta mfadhili, Serikali tunashangaa kwa nini haioni aibu. Anakuja mfadhili ambaye wamesema watoto hawa ni yatima wamewekwa kwenye kachumba, watoto wanalala chini, watoto wanaangaika na wanakuja pale wanapiga picha na Serikali inaangalia. Je, Serikali inapitishaje mkono wake kwenye *NGO* hizi zinazozaliwazaliwa za kulea watoto yatima? Ni vizuri tukaweka utaratibu na sheria ambayo inaweza ikawalinda ili hawa watu wasiichukie nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema sheria hizo, pia kuna haya Makambi ya wale wasiojiweza. Niliuliza swali langu hapa kwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, nikaambiwa kwamba hivi Vituo viko chini ya Halmashauri au Manispaa. Lakini pia Serikali inasahau, karibuni kodi nyingi zimeondolewa kwenye Halmashauri hizo na bado wanapewa mzigo Halmashauri zote kwamba wakarabati au wasimamie na hii Wizara imejitoa. Hii ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kule kwenye hizo Kambi kwa mfano kuna Kambi ya Ipuli, malengo ya Baba wa Taifa hayakuwa hayo kwamba wapewe Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Kambi zile ni kambi ambazo wapo waliokuwa wagonjwa wa ukoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda pale wanatia huruma mno. Chumba kimoja kinawekwa pazia, wanalala mle wajukuu, wanalala mle watoto ambao wamezaliwa ndani

ya miaka hiyo wakati wamewekwa pale kama Kambi. Lakini unapouliza, kila mtu anatupia mpira kwa mwenzie. Wizara hii inafuatiliaje kwa kina kuhakikisha kwamba haya Makambi Serikali aidha iamue kuyaondoa! Lakini kule kuna watoto wengi sana sana ambao mimi mwenyewe kwa macho nimewaona. Wakati ule Serikali ilikuwa inamchukua mlemavu (na nilizungumza swali langu hapa), ambaye hana mikono, vidole vyote vimeisha vya miguuni na vya mikononi. Lakini kwa bahati mbaya wamesahau hao ukiwakutanisha huwezi kumweka mbuzi na majani. Haiwezekani! Matokeo yake kukatokea kitu ambacho ni familia kubwa kwenye maeneo hayo na mpaka sasa ukichukua idadi ya waliokuwa wanaingia wakati ule na idadi ya sasa ni kubwa mno, imeongezeka. Kwa hiyo, kinachotokea kwa sababu majengo hayajaongezwa wamekata pazia, baba analala huku na mama, watoto wanalala hapa. Matokeo yake itakuwa vipi.

La pili, katika Vituo hivyo hivyo, bado Wizara hii imetekeleza hajapima wale watoto wadogo kama wameathirika na yale maradhi ya wazazi wao. Kwa hiyo, tutakuwa na Taifa ambalo ni bovu, Taifa ambalo halitabebeka kwa miaka ijayo. Tusianganie tu kwa sasa hivi hapa tulipo, lakini wale pia nao ni tatizo kwa sababu hawahudumiwi inavyopashwa na kama hawahudumiwi ndiyo hao watatoka kwenda Mitaani na kama watatoka Mitaani itakuwa ni vurugu mech. Ndiyo watatokea majambazi, watatokea watu wa aina hii, lakini Serikali ipo!

Naomba Serikali, Mheshimiwa Waziri mimi nina imani utarudi katika uongozi wako na Naibu wako, lakini utakaporudi la kwanza itakuwa ni kutoka mimi na wewe kama mwanamke mpaka kwenye maeneo hayo. Hakuna ukarabati uliofanyika wa kina. Sasa wale watu kwa kweli tumewatenga kiasi kikubwa Iduguta pamoja na Kambi ya Ipuli. Kwa hiyo, hilo ndiyo nilitaka kulizungumzia kwa uchungu kwa sababu mimi natoka Ipuli Tabora na nimeshaona mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni mikopo ya akina mama. Mikopo ya akina mama ni tatizo, kwa sababu hii mikopo inalenga mjini tu kwa dhamana na ushahidi wanaoutaka, masharti yake. Mama wa Kijijini ambaye naye ni mkulima analima mazao yake madogo madogo. Kwa mfano kuna Vitengo vikubwa sana ambavyo akina mama wamejiunga kwa ajili ya kulima kilimo cha umwagiliaji. Sasa hivi kwa Mkoa wa Tabora tunakula mahindi mabichi, hatuna kiangazi hatuna masika. Hawa watu Mheshimiwa Waziri uliangalie hili tatizo. Akina mama kule ni wengi wanalima Mijini, maana yake kama ni mikopo iguse Mijini na Vijijini, kote kuna matatizo, mikopo hii haiwagusi akina mama ambao wanajitokeza, yanawagusa akisema kwamba yeze anafanya biashara ndogo ndogo amepewa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri uliangalie hilo kwa kina na wale akina mama ambao wanashughulika na kilimo cha umwagiliaji. Pia, Mheshimiwa Waziri nizungumzie kuhusu vitendea kazi kwa Maafisa Maendeleo ni tatizo. Eneo au jirografia tuliyokuwa nayo kwenye maendeleo yetu, Kata na Kata kuigusa ni kazi, sasa huyu Afisa Maendeleo ambaye yuko Wilayani hana gari, hana pikipiki atakwendaje kuangalia kule Maafisa wengine ambao ni wadogo? Naomba Mheshimiwa Waziri mnapopanga bajeti yenu mziangalie hata hizi za Wilaya. Maafisa wa Wilaya wanakata tamaa kwa kukosa vitendea kazi. Hivi hata kuwakopesha tu pikipiki muwakate mishahara yao inashindikana! Kwa hiyo, nilikuwa naomba nao waangaliwe, wapewe vitendea kazi ambavyo wao vitawawezesha kuwapatia takwimu ambazo ni sahihi. Sasa hivi takwimu

ambazo zinatolewa ni zile za mafaili tu, lakini hawaendi kwenye matukio au kwenye maeneo husika ili waone kuna kitu gani ambacho kinatakiwa wanapoanza kukushauri waweze kukushauri ipasavyo? Kuna hii asilimia 10 ya Mfuko huu wa Halmashauri, ni tazito kwa sababu mapato mengi au makusanyo ambayo walikuwa wanategemea sivyo ilivyokuwa. Je, Serikali inafidia vipi lile pengo ambalo wanakusanya na wanagawa asilimia 10? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri uliangalie hili ili zile fidia kama walivyoweza kufidia ruzuku wafidie na huu Mfuko kwa kiasi kile asilimia walivyokuwa wanapata kwenye Halmashauri zao kwa sababu ilikuwa inasaidia. (*Makofî*)

Pia, kuna fedha ambazo zinatoka kwenye Serikali Kuu, ni kidogo hazitoshelezi kabisa kufuatana na jinsi watu walivyoongezeka na hali tuliyokuanayo ya mwamko wa akina mama pamoja na umaskini tuliokuwa nao. Vinginevyo suala la UKIMWI litazidi kupamba moto kutokana na hali ngumu ya maisha tuliyokuanayo wanawake pamoja na wanaume kwenye maeneo yetu tunayotoka. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, hivi vitu ambavyo nimevichangia ni vizuri ukatusaidia kutoa ufanuzi na ufuutiliaji wake ili angalau twende sambamba na hili suala zima la MKUKUTA, vinginevyo MKUKUTA utatuacha kushoto na sisi tutapita kulia au MKUKUTA utapita kulia na sisi tutapita kushoto. Kwa hiyo, ninaomba twende pamoja na wimbo wa Taifa wa MKUKUTA kwa kuoanisha mambo machache kama haya tuliyoyazungumza sisi Wabunge na kuyachangia. Kwa kweli kwa upande wa wanawake Mheshimiwa Waziri naomba uwe makini kufuutilia hususan wale watoto wengine amba wanapata mimba Shuleni kabla ya wakati wake. Wanapewa mimba, mwanaume anaendelea kusoma, mwanamke anasimamishwa. Hili wewe umelifuutiliae? Nakushukuru na kukupongeza kwa jinsi ulivyofuutilia ile ndoa ambayo ilikuwa siyo sahihi. Nakupongeza sana. (*Makofî*)

Sasa na hili naomba ulifuutilie ili tujue wale wanaopata mimba kabla ya kumaliza muda wao unatufikiriaje mama yangu? Baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofî*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. OMAR MJAKA ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara hii mama na mlezi wa jamii yetu ya Tanzania kwa hotuba yake mzuri, yenye upeo mkubwa, ufanisi na maendeleo mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii asilimia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kweli hakufanya makosa yoyote yale kwa uamuza wake uliokuwa thabiti wa kumchagua Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kuwa Waziri wa Wizara hii na Mheshimiwa Shamim Khan, Naibu Waziri wa Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika Serikali yetu ya Awamu ya Tatu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Mawaziri hawa wawili kwa kazi zao nzuri ndani ya Wizara yao, Taifa na kwa jamii yote ya Watanzania.

Nawaunga mkono na nawapongeza sana na pia nawatakia kila la kheri katika kazi zao, majukumu yao, maisha yao na familia zao pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu sana na kwa kweli Serikali yetu haina budi kuipatia uwezo mkubwa utakaowawezesha kufanikisha majukumu yao ya kila siku kwa Taifa na kwa umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelezwa kuwa sera ya maendeleo ya jamii ni ushiriki wa watu katika kuibua, kupanga, kutekeleza na kufanya tathmini ya mipango yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara hii pamoja na Serikali yetu kwa ujumla kwa kuweka sera hii ambayo kama malengo yake yatasimamiwa na kuwezesha ipasavyo basi mafanikio makubwa yanaweza kufikiwa kama yalivyopangwa kwa jamii yote ya Watanzania na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera hii ya maendeleo ya jamii ambayo malengo yake yaliainishwa ni sahihi kwa maendeleo ya jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera inatueleza kuwa ushiriki wa watu katika kuibua, kupanga, kutekeleza na kufanya tathmini ya mipango ya maendeleo ni msingi sahihi kwa maendeleo ya jamii yoyote iwe katika familia au Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kufanikisha haya kwa kweli Serikali yetu iiwezeshe Wizara hii kwa kuipatia nyenzo mbalimbali, fedha na madaraka kamili ya kusimamia, kutekeleza na kuamua mambo mbalimbali yanayohusiana na majukumu ya Wizara hii na umma kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu lisimamiwe ipasavyo ili umma wa Watanzania waweze kufikia matarajio yao ya maendeleo na kuondokana na umaskini uliokithiri mionganoni mwao na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja kwa Serikali yetu kufanya maamuzi yaliyo sahihi na kubadilisha mfumo na misingi ya utoaji wa elimu yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa umefika wakati kwa Serikali kuiwezesha sekta yetu ya elimu kwa kubadili kutoka mwanafunzi kumaliza elimu ya lazima darasa la saba na iwe elimu ya lazima ni kidato cha nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati kwa Watanzania kupata elimu ya lazima hadi sekondari badala ya msingi darasa la saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kuwa suala hili la elimu ya lazima kuwa sekondari badala kuwa ya msingi yaani darasa la saba, Serikali italipokea na

kulifanya kazi ipasavyo. Nakiri kuwa nchi yetu ni maskini lakini pamoja na umaskini wetu huu usitufanye tushindwe kufanya maamuzi makubwa yanayolenga kuleta maendeleo makubwa ya Taifa letu hili la Tanzania hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri kwa kuona katika ukurasa wa thelathini na tatu ambao umeelezea juu ya maendeleo ya mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikanukuu hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri ukurasa huu inaeleza kuwa: “Wizara yangu inalo jukumu la kuhakikisha kuwepo mazingira mazuri yanayowafanya watoto kukua na kupata ustawi kulingana na malezi bora ya familia na jamii.”

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu hili linalo Wizara hii ni la msingi sana kwa maendeleo ya mtoto na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo Serikali yetu suala la watoto wa mitaani ilishughulikie na kulipangia bajeti maalum kila mwaka na pia kulishughulikia suala la watoto wote walioko magerezani, kuwaondoa katika magereza hayo ambako wapo na wafungwa watu wazima. Watengewe maeneo yao maalumu ambayo pia watapatiwa elimu na huduma nyingi zinazostahili kwa watoto hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimnukuu Marehemu Baba wa Taifa Mawali Julius Nyerere, alisema kuwa wajibu wa kuwalea watoto ni wa Taifa zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanalipa kodi, Serikali itunze watoto. Naunga mkono Bajeti hii. Ahsante.

MHE. ANNE S. MAKINDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Nawatakia mafanikio makubwa hasa wakati huu ambapo Serikali imeingia katika mipango wa MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo naomba Wizara ijaribu kuona ni kwa namna gani watasadida Chuo cha Wananchi cha Njombe. Wanajitahidi kubuni mambo mengi ya kuendeleza chuo. Ukweli ni kuwa wanapata maombi mengi sana ya wanafunzi. Lakini majengo yao yamechakaa sana. Hivyo naomba wachangiwe kama shilingi 5,000,000 tu kumalizia jengo ambalo wameanza. Mheshimiwa Waziri anafahamu kuhusu ujenzi huu. Tutashukuru sana iwapo Wizara itaonyesha kuwaunga mkono viongozi wa Chuo hicho cha Njombe. Wanakumbuka sana ziara yako pale chuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali Mheshimiwa Waziri tunaomba msaada wako hasa katika fungu 53 *sub vote 2001 item 6226*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakupongeza sana kwa hotuba yako nzuri yenyе ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yako.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Napenda kuishukuru sana Serikali kwa kutenga fedha katika bajeti ya mwaka 2004/2005 shilingi milioni kumi na nne kwa ajili ya ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chisalu, Wilayani Mpwapwa. Pamoja na ukarabati huo Chuo hicho bado kina matatizo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naib Spika, kwanza, upungufu mkubwa wa walimu. Walimu waongezwe, pili, vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia, tatu, tatizo la usafiri, gari lililopo ni bovu hugharimu fedha nyngi kulikarabati, litatakiwa gari jipya na nne, kwa kuwa chuo kina trekta bovu ipo haja ya kuwapatia trekta mpya. Trekta hilo litasaidia kulima mashamba ya chuo ili wajitosheleze kwa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, chuo kiwekewe simu kwa ajili ya mawasiliano na umeme wa gridi kutoka Mpwapwa Mjini ili kiwe na umeme wa wakati wote na hii itasaidia vifaa vya kisasa kama vile *Computer* na vifaa vingine kufanya kazi wakati wote, sitam kuboresha maslahi ya walimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi hapa nchini, saba, vyuo vingi vya Maendeleo ya Wananchi vianze kutoa mafunzo ya Diploma ya Ufundi na Maendeleo ya Jamii na nane, maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata wapewe mafunzo au waendelezwe kitaaluma na kupewa pikipiki kila kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ESHA H. STIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa furaha kubwa nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Waziri wangu pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Shamim Khan na watendaji wakuu na watumishi wote nchini kwa kazi nzuri wanazofanya na kuifanya Wizara hii kuwa hai na kujulikana sana Kimataifa.

Hakika hotuba aliyoiwasilisha Mheshimiwa Waziri haina mapungufu ila namwomba Waziri wa Fedha aongeze mafungu ya fedha kwa Wizara hii ili iweze kutekeleza malengo yake yote yaliyoorodheshwa kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri. Lazima tuwe wakweli Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, uwezo anao mkubwa, tatizo ni fedha anapewa ndogo. Tafadhali aongezewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa mkoa wetu wa Shinyanga kupatiwa Afisa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kama nilivyowahi kuomba ndani ya Bunge hili Tukufu. Basi mpango huu uendelee kwenye ngazi zingine Mawilayani Mkoani Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashukuru ziara ya Mheshimiwa Waziri Dr. Asha-Rose Migiro, kutembelea Shinyanga na hii ilituletea mwamko wa kazi na watumishi wengine walitutambua kuwa tuna viongozi wetu. Hivyo naendelea kuomba viongozi wengine watutembelee karibuni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa aslimia mia moja.

MHE. REMIDIUS E. KISSASSI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Asha-Rose Migiro, kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti yake na umakini wake katika kusimamia kazi za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri. *Keep it up.*

Napenda kuchangia moja tu kuhusu suala la kuwa na Benki ya Wanawake. Mimi napenda kutoa rai kuwa badala ya kuwa na Benki mahsus kwa ajili ya wanawake tu ambayo itakuwa kubwa sana na gharama kuwa kubwa basi kila benki iliyopo hapa nchini zibinafsishwe kuwa na kitengo cha kuwakopesha wanawake ili fedha hizo ziende moja kwa moja kuwakopesha wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na umuhimu huo si vibaya ikatungwa sheria au kuwepo na agizo maalum ya Serikali. Kutohana na mabenki haya kuwa tayari yana mitandao nchi nzima basi itakuwa rahisi kuwafikia wanawake wengi kuliko kuanza benki mpya kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema naiunga mkono bajeti hii. Ahsante.

MHE. DR. BATILDA S. BURIAN: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kwa uchungu mkubwa na masikitiko naomba niungane na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi na pole kwa familia na wananchi wote wa Majimbo ambayo Waheshimiwa Wabunge wake wameitwa mbele ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pole kwa msiba mkubwa tulioupata Wabunge wote na hususan sisi akinamama kwa kumpoteza Mheshimiwa Margareth Bwana, Mwenyezi Mungu amlaze pema Peponi. Pia naomba Mwenyezi Mungu aijaze amani, imani na faraja familia ya Marehemu Bwana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kutanguliza pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Dr. Asha-Rose Migiro na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Napenda kumpongeza Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Idara kwa ujumla. Wizara imeweza kutekeleza majukumu yake mengi na mazito ikiwemo ya kutayarisha Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla nina mambo machache ambayo ningependa kuchangia. Kwa kuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

ndio yenye jukumu la kuratibu na kusimamia maendeleo ya jinsia na uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera za sekta mbalimbali naomba kuelekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, malezi na afya, Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Afya ifanye utafiti kuona madhara ya dawa za uzazi wa mpango kwa wanawake wa Tanzania, kwani katika kukutana na akinamama hasa vijijini wengi wamelalamika kutokwa na damu nyingi na kwa muda mrefu na pia kuona siku zao zaidi ya mara moja kwa mwezi. Kufuatia hili, uchunguzi ufanyike kabla ya mama kushauriwa ni aina gani ya dawa anayoweza kutumia.

Mheshimiwa Naibu spika, pili, pia kumekuwa na ongezeko kubwa la vifo vyaa kinamama wajawazito wakati wa kujifungua, kwani kufuatia tafiti za hivi karibuni, takriban wanawake 16,000 wamekuja katika kipindi cha miaka miwili 2001-2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nashauri Wizara hii isimamie kuona kwamba Wizara ya Afya inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya afya ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wakunga wa jadi wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara huko vijijini. Wakunga hawana vifaa na kwa mfano, Wilaya ya Karatu mara ya mwisho wakunga wa jadi kupatiwa mafunzo ilikuwa 1992.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mwanamke aweze kutoa mchango wake katika maendeleo ya jamii ni budi afya yake ikawa imara. Hivyo, naomba Wizara ikishirikiana na Wizara ya Afya isaidie kuendesha zoezi la uchunguzi wa kansa ya titi na kansa ya kizazi (kufanya *smear test*). Kwa nchi za wenzetu kama UK zoezi hili linafanywa kila mwaka, linafanywa bure na ni la lazima kwa kila mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, haki za wanawake, hivi sasa karibu kila Mkoa kuna kitengo cha msaada wa Sheria na haki za binadamu kinachowasaidia watu hususan wanawake. Mimi nimebahatika kuwa mlezi wa kitengo cha Msaada wa Sheria, Arusha. Hata hivyo jitihada zifanye kusaidia vitengo hivi, kwani vinatoa mchango mkubwa na wa maana sana.

Mwisho, wanawake na uongozi, natanguliza pongezi zangu kwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Chama cha Mapinduzi na Serikali yake kwa kuoingenza nafasi za uwakilishi wa wanawake Bungeni kutoka 20% mpaka kufikia zaidi ya 30%.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Kwa wachangiaji wa kawaida tumemaliza sasa mchana ataanza Naibu Waziri na Waziri kumalizia hoja hii.

Baada ya maelezo haya, sasa nasitisha shughuli za Bunge, mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.43 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu. Sina budi kusema kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba nitumie nafasi hii kuwapa pole ndugu, jamaa, marafiki na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, waliotutangulia mbele ya haki, Mungu aziweke roho za zao mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafanyakazi wenzangu wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwani bila ushirikiano wao nisingeweza kufanya kazi zangu vizuri kwa kipindi chote cha miaka mitano. Naomba nichukue nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kumshukuru hasa mdogo wangu lakini ni mkubwa wangu wa kazi, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Katibu Mkuu Bibi Hilder Ausi Gondwe, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Maafisa Maendeleo ya Jamii wote, Walimu wa Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Wananchi pamoja na Wafanyakazi wote waliopo Makao Makuu ya Wizara, Mikoa na Wilayani kwa ushirikiano wao mkubwa wa hali na mali katika kufanya kazi za kuleta maendeleo ya Taifa letu. *(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa ndugu zetu wa Mikoani, Wilayani, Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Wakurugenzi wote wa Halmashauri za Wilaya, Miji na Jiji na Viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi na Jumuiya zake hususani UWT wa ngazi zote kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Viti Maalum, kwani bila ushirikiano wao nisingeweza kutekeleza vizuri Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 1995. Naomba wasinisahau waendelee kunichagua. *(Makofî)*

Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri nikiwa Mwenyekiti wa Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wote na Madiwani wote kwa kushirikiana nami vyema katika utekelezaji wa kazi zetu za kila wakati.

Kwa kuwa kipindi hiki ni cha kuagana, naomba nikiri kwamba kwa kipindi chote cha Bunge hili nimepata ushirikiano wa hali ya juu kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wote.

Pia Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii wakiongozwa na Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge na Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Bunge na Mbunge wa Jimbo la Koani Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata ushirikiano wa hali ya juu kutoka kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti akiwemo Mheshimiwa Anne Makinda. Nawashukuru pia Katibu wa Bunge, wafanyakazi wote wa Bunge wa ngazi zote kwa ushirikiano wao mzuri walionipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kujibu hoja zilizotolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimjibu Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wetu, amezungumzia kuhusu mfuko wa *WDF*, anasema, mfuko huu ni mdogo, wanawake wakopeshwe zana za kilimo badala ya kupewa fedha, viwango vya mikopo viongezwe vifikiie Sh.500,000/= kwa kila kikundi hasa kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Mheshimiwa Sophia Simba na napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa tutafanya tathimini ya kina kuhusu *WDF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba tu nitoe taarifa fupi kwamba kwa upande wa marejesho, Halmashauri kama 32 wamefanya marejesho yao, lakini hawajakwenda tena kuchukua fedha. Kwa hiyo, tunatoa wito hasa kwa Waziri kwamba wakafanye hivyo.

Lakini pia kuna Halmashauri kama tano wamefanya marejesho yao mazuri tu ya milioni nane, wanaombwa wakachukue sasa Shilingi milioni 12. Halmashauri hizo ni Arusha Manispaa, wamefanya marejesho mazuri kabisa, Biharamulo, Musoma, Morogoro Manispaa, Songea. Halafu pia Halmashauri kama saba nao tunawasubiri wakachukue milioni zao nane, Bukoba Halmashauri ya Wilaya, Bukoba Manispaa, Ulanga, Kilosa, Kilombero, Geita na Bukombe. Hawa ndio wamefanya vizuri na natoa wito kwamba pamoja na udogo wa Mfuko wetu, lakini marejesho ni muhimu.

Mheshimiwa Sophia Simba, tena amezungumzia watoto kwamba wanahitaji kupata haki zao, wazazi waelewe hilo na kwenda na wakati. Tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge na kwa kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii tutahamasisha jamii. Mheshimiwa huyo huyo Sophia Simba, amezungumzia Bodi za Vyuo kutokukutana ipasavyo, Wizara inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa baadhi ya Bodi za Vyuo hazikutani na hivi sasa Wizara inalifanya kazi tatizo hili ili kupata ufumbuzi wa kudumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba tuwe tunasisitiza katika Vikao vyetu vya *full council* na *RCC*. Afisa Maendeleo husika awe anatoa taarifa ya Vyuo hivi, kwa sababu vinasahaulika. Tukiweka agizo hilo naona Vyuo vyetu vitaendelea kuboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sophia Simba, tena amezungumzia kwamba viongozi waliopo madarakani wajifunze kutokana na jitihada za Mama Anna Mkapa, kwa kutafuta fedha za kuongoza Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono Mheshimiwa Mbunge kwa maoni yake mazuri ambayo ni changamoto kwa viongozi wengine. Tunampongeza Mama Anna Mkapa, hongera zake. Halafu Mheshimiwa Edson Mbeyale Halinga, amesema kwamba Viti Maalum ni vya wasomi tu, Wabunge waende Vijijini kuwaomba wajitokeze kupiga kura za Viti Maalum.

Upo utaratibu maalum wa kuwapata Wabunge wa Viti Maalum na kuna vigezo vimewekwa na Vyama venyewe ambavyo havibagui wasomi na wasiosoma. Wizara kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Halinga, itaendelea kuhamasisha wanawake wa Vijijini kugombea Viti hivyo Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna *cadre* ile ya Maafisa Maendeleo wa Kata zetu na Vijiji. Sasa ukitazama hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 78 jedwali ya tisa utakuta kwamba Mikoa mingi bado haijaajiri hao Maafisa wa Maendeleo katika Kata zao na tukirudi kwa Mheshimiwa Edson Halinga, Mkoa wa Mbeya wana Kata 160, lakini Kata zenyé Maafisa hao ni 70, wakati Kata 93 hazina. Hii ni asilimia 42.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba basi Mheshimiwa kwa sababu hawa Maafisa wana kazi zao katika kuhamasisha jamii na hivi karibuni wameongezewa kazi na Waziri wa Fedha kama mlisikia hotuba ya Waziri, anasema, katika mpango wa kupanua huduma za fedha Vijijini *RFSP*, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri na Idara zao za Maendeleo ya Jamii wamepewa jukumu la kuandikisha vikundi vya *SACAS* au Benki Kata. Kwa hiyo, natoa wito kwamba tuwaajiri hao Maafisa wetu waliopo ili waweze kusaidia katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Benki namuachia Mheshimiwa Waziri atajibu. Kuhusu Elimu ya Chekechea kuwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo utaalamu kuhusu watoto wadogo hauna budi kuangaliwa kwa utalaam zaidi, maana tusifikirie kwa sababu hawa ni watoto vichekechea, basi Mwalimu anatakiwa au mama mmoja wa Kijiji aende tu akasomeshe, hapana. Pale ndio *foundation*, wanaotakiwa ni *professionals* ili waweze kuwafundisha watoto wadogo toka umri huo. Kwa hiyo, ni vyema vikabaki chini ya Wizara vilipo sasa. Magari ya sinema yalienda wapi? Anauliza Mheshimiwa, kwa nini hayo mambo hayapo? Haya magari yarejeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari hayo yalichakaa na hayapo kwa sasa. Ni nia ya Wizara kufufua huduma ya sinema kadri uwezo wa kifedha wa Serikali utakavyoongezeka.

Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Tabora, alisema Maafisa Maendeleo ya Jamii wahamasihwe, wanawake wajitokeze kupiga kura. Wizara katika Kikao chake cha mwaka kilichofanyika Iringa Juni mwaka huu wa 2005 kiliwaagiza Maafisa Maendeleo pamoja na Vyuo vilivyopo chini ya Wizara *FDCs* na *CDTs* kuwahamasisha wananchi na hasa wanawake wajitokeze kupiga kura. Kwa hiyo asante sana Mheshimiwa, tayari tumezingatia wazo lako.

Pia amezungumzia Mkoa wa Tabora kwamba hauna Afisa Maendeleo. Nafasi hii inahitajiwa kujazwa haraka iwezekanavyo. Ni kweli kama alivyosema, nilitembelea Mkoa wa Tabora na niliona hivyo. Sasa naomba nimjibu kuitia Mwenyekiti. Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2004, Katibu Tawala Mkoa ndiye mamlaka ya ajira, hivyo Wizara yangu itawasilisha hoja hiyo kwa Katibu wa Mkoa Tabora kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mbunge pia amezungumzia tena kuhusu maadili, haki ya wanawake, umuhimu wa kuelewa haki za wanawake ni nini, Wizara watumie *CDOs* kuelimisha kuhusu haki za wanawake hasa wa Vijijini ambapo hakuna *TV*, *Radio*, hazisikiki, hakuna umeme, elimu ya uraia ili aweze kushiriki katika uchaguzi. Elimu ya kujua kusoma na kuandika ni muhimu wanawake wakaelimishwa kuhusu haki zao za kiraia waweze kushiriki kupiga kura. Nashukuru kwa ushauri huo.

Hata hivyo, Wizara yangu imepanga katika mpango wa mwaka 2005/2006 itatoa elimu ya Sheria zinazohusu haki za wanawake kwa Maafisa Maendeleo wa Jamii kuitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kushirikiana na Wizara kuhamasisha wananchi. Najua wengi tutorudi, kwa hiyo tuwe pamoja. (*Makofit*)

Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, tena amezungumzia kwamba masuala ya watoto hayasimamiwi na Wizara moja, yapo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na katika Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo. Naona nilijibu kwamba si vizuri kuwa na mlundikano upande mmoja kwa sababu suala hili la watoto ni mtambuka. Ndio maana tumeona libakie Wizara ya Maendeleo ya Jamii ili liweze kuratibiwa.

Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, amezungumzia tena masuala ya kusitishwa kwa asilimia kumi ya mchango wa Halmashauri katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana. Asilimia 10 ya mchango wa Halmashauri katika Mifuko ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana haujasitishwa, isipokuwa uchangiaji umeathiriwa na mapato madogo ya Halmashauri.

Mimi na Mheshimiwa Waziri tumefanya ziara katika Mikoa mingi, kuna Halmashauri nyingine wametekeleza agizo hilo. Sasa naomba nirudie kusema kwamba agizo hilo halijasitishwa. Mheshimiwa Aggrey Mwanri, naye aliuliza swali hilo hilo kuhusu usitishwaji, Mheshimiwa rudi ukadai. Je, mfuko wa Maendeleo ya Wanawake umesitishwa? Jibu kwamba hapana, mfuko wa Maendeleo ya Wanawake haujasitishwa.

Hata hivyo, baada ya hotuba ya Waziri, Waziri wa Fedha ya kusitisha mifuko, Wizara yangu ilichukua hatua ya kuweka utaratibu mpya na itafanya tathimini ya kina ili kuboresha utaratibu wa kuendesha Mfuko huu. Yaani baada ya Waziri wa Fedha kusitisha Mifuko yote, Wizara yangu ilifanya *initiative*, tuliboresha na katika maboresho hayo ndio mafanikio haya yameanza kupatikana.

Mheshimiwa Aggrey Mwanri, anasema, jamii ikatae ukandamizaji. Tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, asante. Kuhusu kuondoa ukandamizaji ili kuwakomboa wanawake, ni muhimu tukaondoa umaskini na mila na desturi zinazowagandamiza wanawake. Ndio maana Serikali Iieridhia Mkataba wa Kuondoa aina zote za ukatili dhidi ya wanawake. Aidha, Azimio la Ulingo wa *Beijing* umebainisha eneo la kuwawezesha wanawake kuwa la kipaumbele. Ahsante sana Mheshimiwa Mwanri.

Kuhusu watoto wa Tanzania kwamba wanaajirwa katika umri mdogo, wanatumikishwa katika kazi za hatari na wanakosa kwenda Shule wakati Viongozi wa Serikali wapo, Viongozi hao pamoja na mimi na wewe kwa pamoja na wale walioko Wilayani mpaka kwenye Kata, tunamshukuru Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa mchango wake alioutoa wakati akiwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha kuondoa chokoraa. (*Makofi*)

Wizara itaendelea kuhamasisha wananchi kuondokana na utumikishwaji wa watoto. Waheshimiwa Wabunge katika kitabu hiki kilichotolewa na Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 69 jedwali la tano linazungumzia idadi ya watoto walioondolewa na kuzuiwa katika utumikishwaji wa kazi zenye madhara katika Wilaya 11 chini ya programu ya muda maalum.

Kwa hiyo, ukifungua ukurasa wa 66 utaona kwamba Serikali imefanya kazi maana kama nilivyojobu kwamba suala hili ni mtambuka, kwa hiyo, utaona kwamba jumla ya watoto waliozuiliwa kufanya kazi hizo zilizotajwa hapo juu ni 11,178 na wale waliondolewa ina maana kwamba wale waliojingiza lakini sasa tayari tumewaondoa ni kiasi cha watoto 9,620. Kwa hiyo, Mheshimiwa tunaafikiana kabisa na wazo lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sophia Simba alisema watoto wanahitaji kupata haki zao, wazazi waelewe hilo na kwenda na wakati, tunakubaliana na hilo. Mheshimiwa Sophia Simba, amezungumzia Bodi za Vyuo pia tunakubaliana. Mengi yamerudiwa rudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama, alizungumzia masuala ya *data*, *Professional Women Database*. Sasa ninafurahi kusema kwamba Wizara yangu tayari aidha imegawa au itagawa fomu kama hizi Mheshimiwa *Information for professional women database*. Naomba basi tuzijaze Mheshimiwa Jenista Mhagama ili tuweze kuzifanyia kazi tuwe na *database* yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia na hoja za maandishi, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mbunge wa Vitongoji alizungumzia suala la watoto wa Mitaani lishughulikiwe na Serikali na kulipangia bajeti maalum. Naafikiana na hilo kwamba

kuna haja ya kufanya hivyo na kazi hii imeanza na tutaliendeleza kwa nguvu zote kwa ushirikiano.

Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, anasema Serikali ishughulikie suala la watoto walioko Magerezani, kuwaondoa katika Magereza hayo ambapo wapo na wafungwa watu wazima. Aidha, watengewe maeneo yao maalum ambapo pia watapatiwa elimu na huduma nyingine zinazostahili kwa watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa mawazo hayo. Naona Wizara husika ipo, imesikia na inafanya hivyo, lakini mahali ambapo ukiona hapajafanywa hivyo, basi ni tatizo la bajeti. Lakini najua tu Wizara husika ipo na itafanya hivyo tukishirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa anasema Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chasalu kilitengewa kiasi cha Shilingi milioni 14 za kukarabati, bado kina matatizo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Walimu, vifaa vya kisasa vya kufundishia, hakuna usafiri, trekta bovu, hakuna simu, maslahi duni ya Walimu, Vyuo vitoe mafunzo ya *Diploma za Ufund*, Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi za Kata wapewe mafunzo au waendelezwe katika taaluma, wapewe pikipiki, Wizara inayatambua matatizo mbalimbali yanayovikabili Vyuo vya maendeleo ya wananchi kikiwemo Chisalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara inaendelea kutatua matatizo haya hatua kwa hatua kufuatana na uwezo uliopo kuhusu upungufu wa Walimu. Wizara inaendelea na utaratibu wa kuomba vibali vya ajira kutoka Menejiment ya Utumishi wa Umma. Aidha, Wizara ina utaratibu wa kuazima Walimu kutoka Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri ambazo Vyuo visto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Chisalu kimepatiwa Walimu wawili kwa utaratibu huu na kukiwezesha Chuo kuwa na jumla ya Walimu sita. Kuhusu vifaa vya kufundishia na vitendea kazi vya kisasa, Wizara itaendelea na mkakati wake wa kununua vifaa kwa kutumia fungu linalotolewa kwa kazi hii na kuvigawia Vyuo kufuatana na utaratibu uliowekwa. Aidha, watumishi wote wa Chuo wakiwemo Walimu wanaendelea kupatiwa stahili na maslahi yao kwa kadri ya mafungu yanayohusika yanavyopatikana. Stahili hizi ni pamoja na nauli za kwenda likizo, malipo ya posho za uahamisho pamoja na kupandishwa vyeo kwa mujibu wa Sheria.

Kuhusu usafiri, Chuo kinalo gari *Land Cruiser* ambalo katika mwaka wa fedha 2002/2004 Wizara ililipatia fedha za matengenezo, gari hili ni zima na linaendelea kuhudumia chuo. Aidha, Chuo hiki kimepangiwa kupatiwa umeme wa nguvu za juu katika mwaka wa 2005/2006. Madhumuni ya Vyuo hivi ni kutoa stadi na maarifa ya kuwawezesha wananchi kujitegemea. Kwa sasa Vyuo hivi havijaingizwa katika utaratibu wa kutoa mafunzo ya ngazi ya *Diploma za Ufund*. Mheshimiwa Lydia Thecla Boma, Viti Maalum aliuliza:- Kwa kuwa Chuo cha maendeleo ya wananchi Newala kipo umbali wa kilometra sita kutoka Mjini Newala na kwa kuwa gari lililopo *Land Rover one ten*

pickup STG 7312 ni la muda mrefu, ni bovu na halifanyi kazi. Je, Wizara ina mpango gani wa kukipatia Chuo hicho usafiri wa uhakika?

Wizara inatambua matatizo makubwa ya usafiri katika Vyuo vingi vya Maendeleo ya Wananchi kikiwemo Chuo cha Newala. Hata hivyo, Wizara inao mkakati wa kukarabati mitambo ya Vyuo vikiwemo Vyombo vya Usafiri ulioanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2002/2003. Kwa kuwa bweni jipya lililojengwa kwa ufadhili wa *JICA* limekamilika, Wizara ina mpango gani wa kukitafutia Chuo Wahisani kwa ajili ya kuweka vitanda 100, magodoro 100, viti 100 na meza 100 ili kukidhi idadi ya wanachuo wanaoongezeka? Ununuzi wa vifaa vya Vyuo unakwenda sambamba na ukarabati mkubwa unaoendelea mwaka hadi mwaka pindi Chuo hiki kitakapofikiwa na huduma ya ukarabati mkubwa, mahitaji haya yatazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Makinda amezungumzia kuhusu majengo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Njombe kwamba yamechakaa. Wizara ina mpango gani wa kukarabati majengo ya Chuo hiki? Wizara inaendelea na utaratibu wa kukarabati majengo ya Vyuo kikanda kwa kuzingatia vigezo iliyojiwekea, majengo ya Chuo cha Njombe yatapatiwa huduma hii punde Chuo kitakapofikiwa. Chuo kipo kanda ya Nyanda za Juu yenye jumla ya Vyuo tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esha Stima, amesema anamwomba Waziri wa Fedha, aongeze mafungu ya fedha kwa ajili ya Wizara yangu ili iweze kutekeleza majukumu yake. Tunakushukuru sana. Nilivyoeleza wakati nikijibu hoja kama hii, naomba hili nimwachie Mheshimiwa Waziri atalijibu. Anashukuru kwa Mkoa wa Shinyanga kupatiwa Afisa Mshauri Maendeleo ya Jamii Mkoa, ahsante nimezipokea, shukrani za Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge wa Dimani, Mheshimiwa Remidius Kissassi, anasema, badala ya kuwa na Benki mahususi kwa ajili ya wanawake tu kila Benki hapa nchini iwe na kitengo cha kuwakopesha wanawake na ziwepo fedha maalumu ambazo zitakwenda moja kwa moja kwa wanawake.

Aidha, itungwe Sheria au kuwepo na agizo maalum la Serikali, kwa kuwa Benki zina mitandao nchini kote. Napokea maoni ya Mheshimiwa Remidius Kissassi, Benki ya wanawake zina umuhimu wa pekee kwa kuwa ni hatua ya makusudi ya kuwawezesha wanawake kuwa na chombo chao cha fedha. Benki zote nchi nzima zina uhuru wa kuanzisha kitengo maalum cha kuwakopesha wanawake yaani Benki zote nchini zina uhuru, wakitaka, wanaweza kuanzisha vitengo hivyo.

Mheshimiwa Dr. Batlida Buriani, Mbunge Viti Maalum ye ye anasema hivi, Wizara ishirikiane na Wizara ya Afya kuona madhara ya dawa za uzazi wa mpango kwa wanawake. Fedha za kutosha zinatengwa kwa ajili ya afya ya mama na mtoto, wakunga wa jadi wapatiwe mafunzo. Aidha, zoezi la uchuguzi wa kansa ya matiti na kizazi uwe kila mwaka na bure kwa kila mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili linaendelea la kuchunguza matiti. Sasa nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba afya ya uzazi ni eneo la kipaumbele kwa msingi wa sera ya maendeleo ya wanawake na jinsia na ulingo *Beijing*.

Hata hivyo, Wizara itashirikiana na wadau mbalimbali kuhusu msaada utakaoweza kutolewa ili kuwapatia mafunzo wakunga wa jadi na kuendeleza zoezi la upimaji wa saratani ya matiti. Jitihada zifanywe za kutoa msaada kwa vitengo vya Sheria na haki za binadamu kwa kuva vinatoa msaada mkubwa hasa wanawake. Wizara inazipongeza Asasi zisizo za kiserikali zilizounda vitengo vya msaada wa kisheria kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itashirikiana na Asasi hizo ili kuhamasisha na kuelimisha kuhusu haki za wanawake. Marejesho ya *WDF* ni magumu, kwa hiyo, mfuko uingie katika maendeleo endelevu kwa mfumo wa *SACCOS* na *SACAS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na kama nilivyowasomea hapa takwimu, ni kwamba tatizo liko katika marejesho, tumepokea ushauri wake na maelezo kuhusu ugumu, yatafafanuliwa zaidi katika hotuba ya Mheshimiwa. Tunategemea kufanya tathmini ya kina katika mwaka 2005/2006 ili kuboresha mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nigosie hoja zilizotolewa wakati wa kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu na hotuba ya Bajeti. Mheshimiwa Esha Stima, alichangia hotuba hizo mbili, alisema Serikali iongeze asilimia ya fedha inazotoa kwa ajili ya kuwakopesha wanawake. Mheshimiwa Esha Stima, tunaafikiana na wewe lakini pia kama nilivyosema hapo awali kwamba tumewapelekea lakini ni baadhi tu wameanza kufanya marejesho. Kwa hiyo, naomba tukasimamie hayo marejesho lakini pia hoja yako tutalitazama.

Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa hawa pia wamezungumzia hayo hayo, mikopo inayotolewa kwa wanawake ni mdogo na tunaafikiana. Lakini tunayatoa marejesho ndio hayo, fedha zinazotolewa kwa ajili ya kuwakopesha wanawake ni ndogo tunaafikiana, lakini kumbuka tuliapoanza mfuko huu mwaka 1995 tulianza na mtaji wa shilingi milioni 250, lakini mwaka 1993 hadi 1994 tumefika hadi bilioni 2.7. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri kwa wakati huo walikuwa wanapata 500,000 tu lakini leo tunawapelekea hadi milioni 4 wakirejesha, milioni 8 wakirejesha, milioni 12 toka 400,000. Kwa hiyo, tumezingatia, sikatai, Mheshimiwa Esha Stima, anazungumzia asilimia inayotozwa riba ipunguzwe hasa kwa yale mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kilio cha akinamama wengi na katika kutoa mifano kwa mfano *CREW* inatoa asilimia 12, *PRIDE* inatoa asilimia 35 ili yaweze kujiendesha kibiashara. Mfuko wa *WDF* yaani mfuko huu wetu unatoza riba ndogo ya asilimia 10 kwa vile unaendeshwa kwa kutumia ruzuku ya Serikali kama vile kulipia mishahara ya watendaji na kadhalika. Kutokana na hali hii riba ya mashirika haya itaendelea kuwa katika viwango vitakavyowawezesha kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Diana Chilolo, aliandika wataalam wa maendeleo ya jamii wawezeshwe kwa kupatiwa vitendea kazi kama vile, usafiri na mawasiliano kwa ajili ya kwenda kutoa mafunzo ya ujasirimali kwa wanawake na vijana. Wizara inahusika na masuala ya taaluma, Halmashauri sita zinatakiwa kutenga Bajeti ya kutosha kwa Idara hizi ili ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya ujasirimali kwa wanawake na vijana wafanyabishara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kupitia riba ya mfuko wa maendeleo wanawake, wataalam wa Maendeleo ya Jamii wamewezeshwa kutoa mafunzo kabla ya mikopo. Aidha, Bajeti ya Wizara ya mwaka 2005/2006 imetilia maanani suala hilo kupitia MKUKUTA. Hii ina maana kwamba ile riba inayotolewa ya asilimia 10 inabaki pale pale kwenu ili muweze kutumia katika masuala haya aliyoyazungumzia Mheshimiwa Diana Chilolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ruth Msafiri amesema kupunguza urasimu katika utoaji wa mikopo. Kutokana na taarifa tulizonazo, pamoja na tathmini tulizofanya mwaka 2004/2005 tumefanya tathmini suala la urasimu katika kupata mikopo limepungua kutokana na utaratibu mpya wa kuwekeana mkataba na Halmashauri ambapo zinalazimika kugawa fedha kabla hazijapatiwa nyingine na kutoa taarifa za ugawaji wa fedha za mikopo zilizotolewa Wizarani.

Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Hadija Kusaga, Mheshimiwa Peter Kabisa, matumizi ya wakala katika kuendesha mfuko wa *WDF* kwa vile tunatarajia kufanya tathmini ya kina kuhusu uendeshaji wa mfuko wa mwaka 2005/2006 suala hili pia litafanyiwa kazi ili kuona iwapo kuna umuhimu wa kuwatumia wakala hawa vinginevyo.

Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, pia anasema utaratibu wa kutoa mikopo kwa vikundi vingi kuondolewa na badala yake vipatiwe vikundi vichache vilivyoungana. Walengwa wa mfuko wa *WDF* ni wanawake wenye umri wa miaka 18 na kuendelea na walio chini ya umri huo kama wana watoto walijiunga katika kikundi cha wanawaka watano wanaojiamini na kitakuwa ndio dhamana yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kuna baadhi ya wanawake wenye uwezo wa kujidhamini ambao wanashindwa kupata mikopo kwa wakati kutokana na kusubiriana katika vikundi. Kwa vile tutafanya tathmini ya kina mwaka 2005/2006 suala hili nalo litafanyiwa kazi ili kuona uwezekano wa kubadilisha mfumo wa dhamana.

Mheshimiwa Peter Kabisa, amezungumzia mikopo isisimamishwe kutolewa kwa vile itawanyima haki wanawake, ni sera ya Serikali kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia mikopo. Kwa hiyo, tunaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbunge, lakini tunaomba marejesho. Wanawake ambao hawajarejesha mikopo hiyo wafuatiliwe na waelimishwe kuhusu umuhimu wa kurejesha mikopo. Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali inaendelea kufuutilia urejeshaji wa mikopo hiyo, pia Wizara imewezesha kufanyika kwa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake wafanyabiashara yaliyojumuisha elimu ya uendeshaji na usimamizi wa biashara. Urejeshaji wa mikopo ni sehemu ya uendeshaji wa biashara.

Kwa kweli nilikuwa na majibu mengi lakini kwa sababu ya muda umetutupa mkono naomba niseme tu na Waziri atakuja kusema mwenyewe kwamba hoja zilizobakia tutazijibu kwa maandishi na watapewa Waheshimiwa Wabunge kabla ya Bunge kuvunjwa tarehe 29 mwezi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono. Ahsante sana. (*Makofii*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha hoja yangu jioni ya leo. Napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii.

Wabunge waliochangia kwa kauli ni Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mwanne Mcemba na Mheshimiwa Shamim Parkar Khan. (*Makofii*)

Wale waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Anne Makinda na Mheshimiwa Lydia Thecla Boma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo pia waliochangia wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na hotuba ya TAMISEMI na vile vile hotuba ya Waziri wa Fedha, tungependa nao kuwashukuru sana na kutambua mchango wao. Hao ni Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Gwassa Sebably, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Isaac Cheyo na Mheshimiwa Khadija Kusaga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna wengine ambao labda tumepitiwa kuwataja tutaomba mtukumbushe ili tuweze kutambua mchango wao. Lakini kwa ujumla tunawashukuru wote hawa na tunawashukuru Wabunge wengine pia ambao hawakuwahi kuchangia, lakini tunafahamu kwamba katika shughuli zetu za kila siku wamekuwa wakitupwa maoni na wakitushauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamin Parkar Khan. Kwa kweli ye ye mwenyewe amesema alikuwa na majibu mengi lakini mimi naona amejibu hoja zote. (*Makofit*)

Kwa hivyo, namshukuru sana na ningependa tu kutumia muda huu kujibu masuala machache yaliyotokana kwanza na taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, halafu pia masuala yaliyojitekeza katika hotuba ya Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupitia Bunge lako Tukufu na kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri pia tutoe shukrani zetu za dhati nyingi sana kwa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kazi kubwa waliyofanya katika kipindi cha miaka mitano hii. Lakini tuwashukuru wakati wote kwa kuweza kuwa pamoja nasi kutuasa na kutuelekeza. Leo hii tumepokea ushauri wote waliotupatia, kwa sababu kwa kweli walichokuwa wakituambia ni namna ya kuimarisha utendaji katika Wizara yetu na tumezingatia utendaji huo hasa kuhusiana na Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake kama tulivyosema na kama majibu mengine aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri alivyoonyesha sisi tunakubaliana na ushauri wa Kamati, tunakubaliana na upungufu uliojitekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunataka kuwashakikishia kwamba tumeshaanza kuyafanya kazi yale ambayo tunaona ni ya upungufu na tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wa Kamati hii kwamba kabla ya Bunge waliweza kutupatia mawazo yao kupitia warsha tulioifanya ya tathmini ya mfuko huu. Kwa hiyo, kwa kweli tathmini imeanza, tutazingatia ya Kamati, lakini tutazingatia yote yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameweza kutushauri ili mfuko huu sasa uweze kwenda sambamba na mahitaji ya wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limejitekeza pia suala la Benki ya Wanawake, ni kweli suala hili limekuwepo na sisi kama Wizara tulifanya utafiti wa awali na tukapeleka mapendekezo yetu Serikalini na tunafurahi kwamba Serikali ilikubali kimsingi kwamba Benki hii ianzishwe. Sasa hivi kwa kweli kinachosubiriwa ni kati yetu sisi na Wizara ya Fedha kuandaa utaratibu mzuri na hivi sasa Wizara yetu imewasiliana na Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha iko katika utaratibu wa kushirikiana na Benki Kuu ili tupate mtaalam mwelekezi kuhusu uanzishaji wa Benki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata pia ushauri kutoka kwenye Kamati kuhusu suala zima la kuongezeka kwa majukumu yetu na Bajeti ambayo tunaipata. Majukumu yetu ni mengi kama ambavyo yanafahamika lakini baada ya MKUKUTA tumepata majukumu mengi zaidi. Lakini kwa utaratibu wa MKUKUTA vile vile tunategemea kwamba katika kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji wa MKUKUTA kiwango cha Bajeti kitakuwa kinakwenda kikiongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuishukuru Kamati hii kwa sababu kwa kweli hata hizi fedha zilizoongezeka katika mwaka huu wa fedha zimetokana na jitihada kubwa sana za Kamati yetu kuweza kutuzungumzia, kuweza kuishauri Wizara ya Fedha mpaka tumefikia kiwango hiki. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na maoni ya Kamati kwamba Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa kweli ni muhimu sana na sisi tutachukua ushauri huu pamoa na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wote ili tuendelee kuviimarishe. Lakini kama ambavyo mtakuwa mmeona toka mwaka wa 2000/2001 kumekuwa na kasi kubwa zaidi ya kurekebisha miundombinu, kumekuwa na kasi kubwa zaidi ya kuongeza fedha za matumizi kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo napenda sasa nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Teddy Kassella-Bantu, ambaye ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani na vile vile Waziri anayeisubiri nafasi hii endapo *UDP* watafanikiwa kuingia madarakani. Tunamshukuru kwa yote ambayo ameweza kutueleza, lakini ningependa kupitia haraka haraka yale machache ambayo tunadhani yanahitaji majibu yetu, mojawapo ni kuhusiana na suala la kuwa viongozi mchanganyiko kwenye ngazi ya juu kabisa ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni wazo zuri lakini tungependa tu kutahadharisha kwamba haitakuwa vema kuangalia Wizara moja tu, kwa sababu ziko Wizara ambazo viongozi wa juu wote ni wanaume. Kwa hiyo, nadhani kama tunataka uwiano mzuri wa kijinsia basi tuangalie mtiririko huu kwa mapana yake ili pale ambapo tutaona ni muhimu kufanya mabadiliko, mabadiliko yale yasiturudishe nyuma. Vile vile na yeze ameshauri kwamba Wizara yetu iongezewe Bajeti nadhani kama nilivyojibu kwamba tunategemea Bajeti yetu itakwenda ikiongezeka kadri tunavyotekeleza majukumu ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyumba za maendeleo nadhani itakumbukwa kwamba katika hotuba yetu kamili tumezungumza kwamba Wizara yetu katika utekelezaji wa MKUKUTA inao mpango wa kufufua nyumba za maendeleo.

Vile vile tunao mpango wa kuwawezesha wataalam wa maendeleo ya jamii waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. Hatukubaliani na hoja ya Mheshimiwa Teddy Kassela-Bantu, kwamba Mendeleo ya Jamii, Maafisa wake wanakaa ofisini. Si kweli kwa sababu hata kimafunzo hawapaswi kufanya hivyo, lakini mafanikio tuliyoyaeleza ya utekelezaji wa miradi ya kijamii yanaonyesha ni kwa namna gani Maafisa Maendeleo ya Jamii wamehusika moja kwa moja kuhamasisha wananchi huko waliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia pia suala zima la uchakavu wa majengo katika *FDCs*, lakini kama ambavyo nimetangulia kusema Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi hivi sasa vinaangaliwa kwa makini zaidi, Bajeti yao imeongezeka. Kasi ya kuvikarabati vyuo hivi imekuwa ni kubwa zaidi na tunategemea ili viweze kutimiza malengo yao kikamilifu ndani ya MKUKUTA tutaendelea kuviimarishe.

Kuhusu Benki ya Wanawake tayari nimeshalizungumza, chombo cha wanawake ndiyo upo umuhimu, umuhimu huu ulionekana siku nyingi sana. Hivi sasa Serikali imeshauri au imetoa msimamo kwamba ni kweli umuhimu huo upo, lakini kwa kuwa suala linalohusu chombo ambacho kiliundwa wakati ule lipo Mahakamani kwa hivyo

basi tusubiri matokeo yake. Kwa hiyo, pindi kesi hiyo itakapokamilika basi tutaona ni namna gani tuendelee na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*), napenda nitumie nafasi hii kwa kweli nami kuungana na Waheshimiwa Wabunge wote waliompongeza Mheshimiwa Mama Anna Mkapa, kwa mfuko huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu ni mfuko usio wa Kiserikali kama ilivyo mifuko na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali. Kwa hiyo, hatuoni kama ni busara kwa Serikali kuuchukua, kinyume chake sisi tunahamasisha viongozi, Waheshimiwa Wabunge na Watendaji wengine wote waweze kujitokeza kwa wingi ili tuwe na mifuko hii mingi. Mfuko mmoja tu kama wa Mheshimiwa Mama Anna Mkapa, hautawenza kutatua matatizo ya jamii, kwa hiyo, tunadhani uendelee kuwa mfuko siyo wa Kiserikali na endapo atakuja mke wa kiongozi mwngine ambaye atapenda sisi tutakuwa tayari kushauriana naye ili na yeze atimize wajibu wake katika eneo ambalo atakuwa amelichagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kwamba Chuo hiki sasa kiweze kuhamishiwa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya juu. Sisi tunaona kwamba viko vyuo vingi chini ya Wizara za kisekta, Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, ni Wizara ambayo kwa kweli inafanya kazi ya uratibu. Sisi tungependa kuona inakuwa hivyo ili yale ambayo tunasimamia katika sekta yetu yaweze kushughulikiwa kwa karibu zaidi. Kwa hiyo, tutaendelea kukiimarisha kama Chuo cha Kitaaluma na kitaendelea kuwa Chuo Cha Elimu ya Juu lakini itakuwa vema kama kitabaki kwetu ili tuweze kupima ile taaluma na kuboresha pale ambapo tunatakiwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameshauri pia kwamba Tengeru iunganishwe na Vyuo vingine kama Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Chuo cha Sayansi ya Jamii na kadhalika. Sisi wenyewe tunakiandaa chuo hiki kuwa na mamlaka zaidi ya uendeshaji wa shughuli zake na tunadhani kwamba kuwa na vyuo vingi ambavyo ni vyua ngazi ya kati ni jambo la muhimu zaidi kuliko kutaka taasisi zote ziwe vyuo vikuu. Kwa hiyo, tutaendelea kukiimarisha na tutaendelea kukipa nguvu ili kiweze kutimiza majukumu yake kwa ukamilifu zaidi. Lakini tunavyo pia vyuo vyua Buhare na Rungemba vyuo hivi navyo tutaendelea kukiimarisha ili viweze kufikia kiwango cha juu kama kile cha Tengeru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimejibu yote, ila kuna moja ambalo ningeweza kulizungumzia, hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Sophia Simba na linahusu asilimia 30 ya uwakilishi ndani ya Bunge. Tunadhani kweli katika kupiga mahesabu tunaweza tusikifie asilimia 30 kwa kuititia tu Viti Maalum. Lakini ni mategemeo yetu kwamba vile viti vyua Majimbo vitajazia upatikanaji wa asilimia hii 30 na hiyo haitunyimi fursa ya sisi wakati muafaka kuweza kuliangalia tena suala hili. Kwa sababu hivi kama alivyosema Mheshimiwa Sophia Simba, Katiba imeshapitishwa kwa hiyo, tuna imani kwamba na kwa kweli ni maslahi ya Wizara yetu kwamba tufikie asilimia hii 30 na hususan kwa kulenga azimio la *SADC* la Wakuu wa nchi.

Lakini tunaunga mkono sana maoni ya Mheshimiwa Sophia Simba, kuwa Vyama vya Siasa navyo viteue wanawake wengi zaidi kugombea uongozi hasa katika ngazi za majimbo. Kwa sababu jukumu la kufikia, Mheshimiwa Daniel Yona, tumbo linamuumua lakini si kitu, katika kufikia azma hii kwa kweli ni la vyama vyote vya siasa, jukumu ni la Serikali lakini pia jukumu ni letu kama jamii kuunga mkono uwakilishi wa wanawake kukiuka kwa kweli hata hiyo asilimia 30 kwa sababu hivi sasa Umoja wa Afrika upo kwenye asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine Mheshimiwa Shamim Khan ameweza kuyajibu. Kabla sijahitimisha hoja hii ningeomba kutumia fursa hii kwa kuwa sasa tunakamilisha kipindi cha miaka mitano cha Bunge hili lililoanza mwaka 2000. Niwashukuru kwanza Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Spika na pia niwashukuru kwa dhati Wenyeviti ukiwemo wewe Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kutuongoza vema na kwa ushirikiano binafsi ambao mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri tumeupata katika kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wake kwa waume ambao wametuasa na wametuongoza na wametusaidia katika kutekeleza majukumu yetu. Namshukuru sana Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Haroub Said Masoud na Kamati nzima. Wamekuwa karibu nasi wakati wote, wamekuwa ni faraja kwetu na wamekuwa tumaini letu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kunipa dhamana ya kuongoza Wizara hii. Nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, kwa kuniwezesha kutumia uzoefu wao katika kuendesha Wizara hii.

Mwisho lakini sio mwisho kwa umuhimu, napenda tena nimshukuru Mheshimiwa Shamim Parkar Khan, kwa kweli Mheshimiwa Shamim Parkar Khan, amenisaidia sana yeze ni kiongozi ambaye alinitangulia katika uongozi, lakini alikuwa tayari wakati wote kunishauri na kunielekeza. Namshukuru pia Katibu Mkuu wetu mama Hilda Gondwe, Wakurugenzi wote na wadau wote katika maendeleo kwa kuweza kuwa nasi katika kipindi chote hiki cha miaka mitano. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa hoja. (*Makofit*)

(*Hoja iamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

Kifungu 1001 - *Administration and General* 1,490,459,000/=

MHE. STEPHEN M. KAHUMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Sina haja ya kuleta maneno mengi au ukorofii, lakini nataka kupata moja tu ambalo litawasaidia Wizara hii kufuata mlolongo mwema wa utendaji. Bunge hili liligeuza jina la Wizara hii na kuipa jina jipya la Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kutoka Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto. Lakini ukitizama katika kitabu cha pili hiki kwenye *content* bado Wizara inaitwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ukisikiliza yote yanayozungumzwa hata wakijibu hoja Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Waziri na Waziri wamezungumzia habari ya wanawake tu. Hakuna jamii, hakuna jinsia sasa hii inaonyesha kwamba Wizara hii bado inashughulikia mambo ya wanawake. Labda turudishe jina lile la Wanawake na Watoto kwa sababu hakuna hata *concept* humu inayoonyesha Maendeleo ya Jinsia. Sasa ningeomba nipate maelezo mafupi. Ahsante. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana shemeji yangu Mzee Stephen Kahumbi, kwa yale aliyojasema. Lakini kwa kitabu nilichonacho mimi kinaonyesha kwamba jina la Wizara ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na hapa imeandikwa *Community Development Gender and Children*, hiki ndio kitabu nilichonacho mimi katika *Vote* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu suala la msisitizo katika yale tuliyoyasema Wizara yetu ina maeneo makuu matatu na tunayo Idara ya Maendeleo ya Jamii na kwa kweli hata katika Idara ya Maendeleo ya Jamii tumejitahidi sana kuimarisha kwa kuzingatia kwamba tunayo majukumu kwa wanawake na wanaume wa nchi hii. Yapo ambayo bado yanaendelea kupata msisitizo kwa yale maeneo ambayo wanawake wako nyuma, lakini kwa kweli kwa ujumla wake hasa katika eneo la Maendeleo ya Jamii Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vinahudumia watu wanawake na watu wanaume tumeviimrisha sana. Wataalam wa Maendeleo ya Jamii tunakusudia kuwawezesha kinyenzo, tumeweka pia mikakati ya kuwashamasisha wananchi zaidi washiriki shughuli za maendeleo na hizi zinalenga wanawake na wanaume. Ni katika maeneo yale machache ambayo yamehitaji msisitizo wa pekee ndio ambayo na sisi tumeyapa msisitizo wa pekee. Ahsante.

MWENYEKITI: Ni kweli kwenye vitabu vyetu kwenye *contents Vote 53* imeandikwa *Ministry of Community Development Woman Affairs and Children* nadhani ni *typing error*.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuweza kujibu hoja zetu kwa ufasha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo moja tu dogo kwa kuwa katika michango yangu na ninafikiri huu ni mwaka wa tatu nimekuwa nikiipa taarifa Wizara kwa juhudii zilizofanywa na wanawake wa Mkoa wa Ruvuma kwa kuanzisha vyama vyao vya Akiba

na Mikopo. Kwa hiyo basi, nimekuwa kila siku nikiomba Wizara kutupia macho suala hilo na kuona ni namna gani wanaweza kushirikisha nguvu za Wizara katika kuwasaidia wanawake katika shughuli hiyo walioianza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi wanawake hao wanataka sasa kushirikisha mahusiano ya jinsia katika vile vyama vyao vya Akiba na Mikopo walivyovianzisha. Lakini mpaka sasa hivi bado Wizara haijatusaidia kupiga hatua za ziada katika maeneo mbalimbali kwenye shughuli hiyo na hivyo kuonekana shughuli hiyo ikifanywa tu na wanawake wenyewe peke yao bila kupata msaada wa karibu kutoka katika Wizara. Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri leo atuambie kwa sababu ni Bajeti hii ya mwisho ni namna gani basi Wizara itakuja kushirikiana na sisi moja kwa moja katika maeneo ambayo tumekuwa kila siku tukiyaomba ili kusaidia kudumisha mahusiano hayo ya kijinsia ya kuvifanya vyama hivyo viweze kufanya kazi kwa mtazamo halisi unaotakiwa.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba radhi kwamba ukurusa wa 192 ambaa mimi ndio nilikuwa nauangalia ndio wenyewe maneno *Ministry of Community Development Gender and Children* na kwamba katika *table of contents* ambayo iko ukurusa wa nane namba za kirumi inaonyesha *Community Development Woman Affairs and Children*. Nadhani hili ni kosa ambalo tutashirikiana na wenzetu wa Hazina kuweza kulirekebisha nadhani linatokana na ule utaratibu wao wa kuweka *codes plans* fulani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Jesnista Mhagama kwa kweli kwa mawazo yake mazuri na labda nichukue nafasi hii kumpongeza yeze binafsi. Ni kweli amekuwa akihimiza sana masuala haya ya *SACCOS* katika Mkoa wa Ruvuma, mimi mwenyewe nimetembelea kule, nimekutana na vyama hivi lakini pia nimeona jitihada za wanawake wa Mkoa wa Ruvuma kwenye Maonesho ya Sabasaba kila mwaka, ni mkoa ambaa unaleta wanavikundi wengi sana wa Vyama hivi vya Kuweka na Kukopa.

Sasa kuhusu kupeleka mfuko huu kwenye Vyama vya Kuweka na Kukopa, labda niseme hivi kwanza upo uhuru kwa Halmashauri kuweza kuelekeza mfuko huu kwenye Vyama vya Kuweka na Kukopa lakini huu umekuwa ni uhuru ambaa hatujauweka rasmi kwenye taratibu, lakini ni uhuru ambaa tunauunga mkono sana na tungependa Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma zifanye hivyo. Lakini kama tulivyosema wakati tunahitimisha hoja hii, tuko katika tathmini ya *WDF* na sisi tunaamini kwamba mfuko huu utakuwa na manufaa zaidi kama utaelekezwa kwenye *SACCOS* na hizi zitakuwa ni *SACCOS* za wanawake na wanaume na itakumbukwa kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika hotuba yake aliyosema sasa ni nia ya Serikali kuimarisha *SACCOS* na *SACCAS* na pia huduma za fedha vijijini na tunaamini kwamba katika tathmini tutakayofanya basi mfuko huu utakuwa mchango mkubwa katika *SACCAS* hizo na *SACCOS* hizo ili tuweze kupata uwiano mzuri wa kijinsia jambo ambalo ndiyo Wizara yetu inalisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MHE. THOMAS NGawaiYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyofanya kazi yake kwa umakini sana. (*Makofi*)

La pili nataka nimkumbushe tu kwa sababu amesema kwamba safari hii tumeongezewa hela, tulikuwa naye kwenye Chuo cha Msinga, *Msinga Farmers* pale sasa kulikuwa na maombi ya nyongeza ya fedha mwaka jana.

Kuhusu suala la maji akaahidi shilingi milioni 4 sasa naona *allocation* iliyotoka hapa badala ya kuwa angalau juu zaidi ya wengine naona hata kwetu imepungua kidogo wakati wengine wana 36 kwetu naona kama 33. Sijui anasemaje kuhusu hilo kwamba Chuo hicho ambacho yeye mwenyewe alikitembelea mara mbili na mimi nikiwepo anasemaje kuhusu kuiongezea ili iweze kwenda kwa ufanisi zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya mwisho ni kweli, lakini Mheshimiwa Stephen Kahumbi, ameshazungumza kuhusu hii *gender*, mimi *gender balance* najua ni wanaume na wanawake, nilivyosikia kauli mbiu ya matiti basi nilikuwa nafikiri na kauli mbiu ya mabusha ingetajwa. Sasa kwa sababu ni *balance*, sasa hilo kama anaweza kujibu. Ahsante sana.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kwa maneno mazuri aliyosema kuhusu Wizara yetu lakini pia naomba nimkumbushe kwamba ni kweli kuna tatizo la maji katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msinga, lakini kama tulivyosema hapo awali katika siku za nyuma kuhusiana na swali aliloweza kutuuliza na pia barua ambazo tumeandikiana mimi na yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya tathmini na fedha hizi ambazo tumezitenga kwa kweli ndiyo tumeona zitatoshaleza kwa ajili ya shughuli hiyo. Lakini pamoja na hayo tunategemea pia kile tutakachokiweka kitajazilishwa na fedha za ufadhili, kwa hiyo, tunategemea kwamba tutaweza kukamilisha shughuli hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Saratani ya matiti, ni kweli tuliweza kuhamasisha wadau mbalimbali waweze kushiriki nasi katika kushughulikia masuala yanayoikibili jamii, lakini tukapata wale waliojitlea kuhusu Saratani ya matiti, kuhusu suala la mabusha tunajua ipo kampeni maalum ya shughuli hiyo, lakini kama kutakuwa na mabusha ambayo yanashukiwa kuwa na Saratani, basi nadhani hao wataalam pia wataweza kuyashughulikia. (*Kicheko*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* 243,949,000/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* 185,724,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Training and Folk Dev. Colleges* 2,161,580,000/=

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu nipate maelezo kidogo fungu 2001 programu 20, kifungu kidogo 260200, *Educational Materials, Supplies and Services*.

Tatizo lililoko katika Vyuo vyetu ni ukosefu wa vitenda kazi kwa mfano Chuo cha Lushoto kule Mabughai kina vyerehani vitatu na wakati huo tunategemea tutafundisha wanafunzi, sasa labda Waziri kwa bahati nzuri hiki kifungu kimeongezwa ongezwa, nilitaka anitamkie kwamba angalau wataongezewa vyerehani na vifaa vingine vya kufanyia kazi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Henry Shekiffu, kwa swali lake na Mheshimiwa Henry Shekiffu ni mmoja wa Waheshimiwa Wabunge ambao wamekuwa wakifua tilia kwa karibu sana suala la vyuo hivi, napenda kumpongeza na kumshukuru kwa jitihada zake na nafahamu pia pamoja na kwamba tumelizungumza hili suala la vifaa vya mafunzo yeze mwenyewe Mheshimiwa Henry Shekiffu, pia ameweza kutoa misaada mbalimbali. Tunampongeza. (*Makofi*)

Sasa kuhusu hiki kifungu 260200 ni kifungu ambacho kitagharimia vifaa vya mafunzo na kulipia chakula cha wanachuo na tunaamini pia Mabughai itakuwa ni moja ya Vyuo ambavyo vitatazamwa katika suala zima la kuvipatia vifaa vya mafunzo vikiwemo vyerehani. (*Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Community Development* 1,476,451,000/=

Kifungu 2003 - *Community Dev. College - Tengeru* 292, 415,000/=

Kifungu 3001 - *Gender Development* 603,353,000/=

Kifungu 3002 - *Children Development* 672,153,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko
yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

Kifungu 2001 - *Training and Folk Dev. Colleges* 198, 000,000/=

Kifungu 2002 - *Community Development* 508, 000,000/=

Kifungu 2003 - *Community Dev. College - Tengeru* 594, 000,000/=

(Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

TAARIFA

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2005/2006 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makisio ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.
(Makofisi)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

(Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo mawili, moja baada ya kuahirisha kikao hiki Kamati ya Maendeleo ya Jamii inaombwa ibakie humu ndani.

Lakini kesho Waheshimiwa Wabunge, akinamama mmealikwa na Mfuko wa Usawa wa Jinsia kwa ajili ya Sabasaba. Kwa hiyo, gari litaondoka kesho baada ya kipindi cha maswali. Kwa hiyo, wale ambao wanataka kwenda hawakuonyesha kwamba wanataka kwenda wafanye hivyo jioni hii kusudi tujue ni wangapi wanakwenda.

Baada ya kusema hivyo naahirisha kikao cha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.
(Makofisi)

*(Saa 12.10 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne
Tarehe 5 Julai, 2005 saa tatu asubuhi)*

